

**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR**

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

- | | |
|--------------------------------------|--|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Hamad Masoud Hamad | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdilllah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 11 Julai, 2012

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mezani Makadirio ya Mpatu na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Rashid Seif Suleiman kny/Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako kwa niaba ya Mwenyekiti, wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, naomba kuhudhurisha Mezani Hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 181

Viongozi Wakuu Kutengenezewa Nyumba zao Binafsi

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Ni kawaida kwa viongozi wakuu wanchi duniani kuishi katika nyumba za Serikali. Cha kusikitisha kwa upande wa Zanzibar viongozi hawa huishi katika nyumba zao binafsi na kupelekea nyumba hizo kufanyiwa matengenezo kwa fedha ya Serikali zierendane na hadhi ya kiongozi huyo.

- (a) Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zilizopelekea kuruhusiwa kwa kiongozi wa nchi kuishi viongozi sio kwenda kinyume na Sheria za Fedha.
- (b) Kutumiwa fedha za walipa kodi kwa kutengeneza nyumba za watu binafsi kwa misingi ya kuishi viongozi sio kwenda kinyume na Sheria za Fedha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 181 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-
Mhe. Naibu Spika, nitajibu kwa pamoja. Serikali ina wajibu wa kuwatunza viongozi wake ikiwa ni pamoja na kuwapatia huduma za Makaazi bora na yenye heshima kwa mujibu wa nafasi waliyonayo. Hata hivyo hakuna sheria inayokataza Kiongozi kukaa kwenye nyumba yake ikiwa ataamua kufanya hivyo. Kwa kadri ninavyofahamu na uwadilifu wa viongozi wetu wakuu hakuna nyumba binafsi ya kiongozi yeyote iliyofanyiwa matengenezo kwa kutumia fedha za serikali ukiacha vifaa vinavyohamishika vinavyotumiwa na walenzi na usalama.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu aliyoyotoa Mhe. Waziri mimi nina swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza nilikuwa nataka kujua serikali ina nyumba ngapi ambazo zina hadhi ya kukaa hawa viongozi wetu.

(a) Je, kwa nini huwa hawazitumii nyumba hizo ambazo zimetengwa kwa ajili ya kukaa viongozi.

(b) Kiongozi anapomaliza muda wake anapohamia kwenye nyumba kama ile mara nyingi nyumba ni lazima ifanyiwe matengenezo ili ifanane na hadhi ambayo yeye yupo nayo. Je, matengenezo yale yanapomaliza fidia zile zinalipwa kupitia utaratibu upi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme makaazi ya Rais yanayofahamika hivi sasa yaani *Official Residence* ni Migombani, pale ndio makaazi ya Rais. Ikulu pale ni Ofisi ya Rais na pale tumeweka maalum kwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano atakapokuja. Lakini kuna Kibweni *State Lodge* kuna Bwefum *State Lodge*, kuna Chakechake, kuna Mkoani, kuna Wete. Sasa pia tunatengeneza na Micheweni kwa Unguja.

Kuhusu matengenezo baada ya Rais kustaafu, nafikiri kuna haki ambazo Rais Mstaafu inabidi apatiwe. Sasa hivi sizikumbuki lakini nafikiri tulipopitisha yale mafao ya viongozi kwamba tuna wajibu wa kuwatunza, na mafao yote yale yapo kwamba wanastahiki kutunzwa kama Rais Wastaafu. Sikumbuki labda nilete ile tarifa ya pamoja ili niweze kukupatia yale mafao wanaostahiki yote. Lakini tuna wajibu wa kuwatunza kama Rais Wastaafu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Swali langu Mhe. Waziri hakulijibu katika lile swali la kwanza nililouliza kuhusu zile nyumba ambazo wanaishi viongozi, niliuliza kwa nini hawazitumii. Hakuwa amejibu hili, amejibu tu kwamba

nyumba ipo hii na hii na hii, lakini ile kwa nini hawazitumii hizi nyumba ambazo zimepangwa kwa ajili ya kukaa viongozi hakunijibu hilo swali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kwa kunikumbusha. Kadiri ninavyofahamu na mimi ndiyo Waziri wa Nchi katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais wetu wa Zanzibar anaitumia nyumba aliyopangiwa kwa asilimia mia moja. Nyumba yake ile kwa matumizi yake ya binafsi kwa shughuli zake mwenyewe nyengine anazojipangia.

Lakini nasema tena makao rasmi ya serikali ya Rais wetu wa Zanzibar ni Migombani, na anaitumia kadiri ninavyofahamu mimi, kule nyumbani kwake hayo ni maswali mengine. Kama wewe Mhe. Mtando una nyumba moja Mkwajuni, moja Kibweni, moja pengine, makao rasmi ni Migombani.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri Mhe. Waziri hakunielewa vizuri. Nimezungumzia viongozi sikutaja maalum kwamba ni Rais wa Zanzibar tu nakusudia viongozi wetu wakuu hawa. Rais, Makamo wa Kwanza, Makamo wa Pili, ndio niliokuwa nimewakusudia, yeye anamzungumzia Rais tu. Nimekusudia viongozi swali langu ndio lilivyokuwa hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, nafikiri tuwe waangalifu kidogo unapouliza swali lisiwe linajificha ficha, na hili ningelimuomba sana Katibu bora anapoyaangalia maswali yasiwe yanababaisha yaachiwe uwanja mpana. Tupate swali sahihi tuweze kujibu ipasavyo, lakini sasa itakuwa sijafahamu, vijanini unatumbukiza hapo hapo. Nafikiri huo sio utaratibu mzuri Mhe. Naibu Spika.

Sasa nieleze tu hata hao wengine uliosema kadiri ninavyofahamu Makamo wa Pili wa Rais na yeye anaishi katika nyumba za serikali na Makamo wa Kwanza wa Rais na yeye amepatiwa nyumba ya serikali baada ya ile iliyokuwepo baada ya kuonekana haipo katika hali nzuri.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya yote nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha katika siku hii ya leo kuamka katika hali ya usalama na afya njema.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu swali limeulizwa habari ya viongozi.

- (a) Je, ukimuacha Rais, Makamo wa Pili wa Rais na Makamo wa Kwanza wa Rais. Je, hawa viongozi wetu kama Mawaziri ni wangapi ambao wanaishi katika nyumba zao na ni wangapi ambao hawaishi katika nyumba zao.
- (b) Ni kwa nini hawaishi katika nyumba za serikali kiutaratibu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, ndio yale niliyosema tumetoka kwenye viongozi Wakuu sasa tunakwenda kwa Mawaziri. Mheshimiwa kwa kweli takwimu sina. Hilo tutashirikiana na Wizara husika tumjibu ipasavyo Mhe. Asha Bakari.

Mhe. Rashid Seif Sulaiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii. Kwa kuwa katika majibu yake Mhe. Waziri alisema hakuna sheria inayombana kiongozi kuishi katika nyumba ya serikali au katika nyumba yake.

Mimi nauliza kuhusu hawa viongozi wakuu wanchi kuna utaratibu uliowekwa ya kuwa inawajibisha kuishi katika nyumba za serikali au kila mmoja na yeye atakayechaguliwa atachagua kuishi katika nyumba yake au nyumba ya serikali ikiwa unasema kwamba Ikulu iliyopo Migombani ndiyo nyumba rasmi ya Rais.

Je, Rais yoyote anayekuja atawajibika kuishi pale mapaka hapo itakapoadilishwa kukaa pahali pengine au atachagua vile vile ya kuwa anao uwezo wa kuchagua kuishi nyumbani kwake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, naomba kurejea tena kwamba hakuna seheria inayombana Rais yoyote kutokuishi katika nyumba yake. Naomba kurejea tena Rais wa Zanzibar hivi sasa makaazi yake maalum ni Migombani. Lakini hafungiki kukaa kwenye nyumba yake nyengine baadhi ya siku kama anavyopenda mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, yule ni Rais ana mamlaka yake na yeye ni binaadamu anazotaratu zake. Yeye siye wa kwanza, Mzee Abeid Amani Karume tunakumbuka, Aboud Jumbe Mwinyi wote walikuwa na makaazi maalum lakini wakaishi katika nyumba zao. Hiyo ni kimataifa kwa nini tuwabane Marais wetu tu. Rais wa Marekani kila *week end* yupo *Cape –Verde*, Marais wetu kama Mkapa na Rais wengine wote walikuwa wana nyumba zao

Msasani. Kwa hivyo sio wa kwanza tumbane Rais wetu, tumuachie na uhuru wake.

Nam. 123

Tatizo la Maji Mkokotoni Tumbatu

Mhe. Panya Ali Abdalla – Aliuliza:-

Kuna tatizo sugu katika kisima cha kusambazia maji sehemu ya Mkokotoni hadi Tumbatu, wananchi wanaokaa maeneo hayo wamekosa maji kwa kipindi kirefu sasa na wala hawajui ni lini watawekewa utaratibu mzuri wa huduma hiyo.

Je, ni tatizo gani hasa linalosababisha kutokupatikana maji ya uhakika katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 123 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kisima kinachofanya kazi hivi sasa ni kimoja tu ambacho hakitoshelezi kutokana na uhaba na uchache wa uzalishaji. Taratibu zinazotumika ni za kuyakusanya maji kwa siku nzima na kuyagawa siku ifuatayo katika migao kati ya Mkokotoni na Tumbatu.

Aidha kipindi kirefu bomba lililokuwepo baharini lilikuwa limepasuka mahali pasipojulikana. Lakini bomba hilo kwa sasa limeshafanyiwa marekebisho na wananchi wa eneo hilo wanaendelea kupata huduma hiyo ya maji safi na salama.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake. Pamoja na matengenezo na mwenyewe amekiri kwamba kisima kile ni kimoja tu na mahitaji hayatoshelezi. Pia amesema kuna bomba ambalo limepasuka na limeshafanyiwa marekebisho kwa hiyo maji yanapatikana.

Mimi nataka kumwambia Mhe. Naibu Waziri bado maji hayapatikani kiusahihi katika maeneo hayo. Kuna sehemu wanapata na kuna sehemu hawapati kabisa. Ningependa kujua Mhe. Naibu Waziri Serikali inaonaje ingechimba visima vya ziada ili wananchi wakaweza kupata maji pale inapokuwa yale ya mfereji hayapatikani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Mkaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza kisima kwamba kisima chetu kilichokuwepo pale kina uzalishaji mdogo kwa hivyo Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ina mpango wa kuchimba kisima chengine kwa ajili ya kuboresha na kuongeza uzalishaji wa maji hayo.

Nam. 21

Ukosefu wa Madaktari Kojani

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Katika kutekeleza azma ya Serikali kuwajengea wananchi vituo vya Afya Mjini na Vijini kwa lengo la kuwaondolea usumbufu, Kijiji cha Kojani kimebahatika kujengewa Kituo kizuri na cha kisasa cha Afya na kupatiwa madaktari wawili wa kutowa huduma hiyo kwa wananchi wa Kijiji hicho.

- (a) Mhe. Waziri unaelewa kuwa Madaktari hao wameondolewa ghafla bila ya kupatiwa madaktari wengine mbadala. Kitendo ambacho kinaleta usumbufu mkubwa wananchi kama uliokuwepo hapo awali.
- (b) Ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kuongolewa ghafla kwa madaktari hao.
- (c) Ni lini wananchi hao watapatiwa madaktari wengine ili kuondolewa usumbufu walionao kijijini hapo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba nitoe maelezo. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu swali hili limechelewa kuja hapa Barazani na katika Kikao cha mwezi wa April swali hili lilipata majibu kwa hivyo naomba swali hili liondolewe.

Nam. 141

Minara ya Simu ya Zantel.

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Minara mingi ya Mawasiliano ya simu kama vile Zantel imejengwa ndani ya mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na wananchi. Ni takriban miaka minne sasa tangu wananchi hao walipouza ardhi zao kwa Zantel. Hivi karibuni Zantel wamebadili utaratibu wa kupata ardhi, hivyo badala ya kununua anapewa kwa njia ya kodi.

- (a) Je, Mhe. Waziri, kwa wananchi waliouza ardhi zao haiwezekani sasa kuiangalia upya mikataba yao na kuifanya ya kukodisha.

(b) Je, Wizara yako itawasaidia nini wananchi hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 141 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kama ilivyoelezwa katika swali kwamba takribani hivi sasa ni miaka mine tangu wananchi waliouza ardhi kwa Kampuni ya Zantel kwa lengo la kujengwa minara imeshatimia, kwa mujibu wa sheria za mauziano, swali la mauziano ni makubaliano ya pande mbili kati ya muuzaji na mnunuzi kwa kupeana stahiki ya makubaliano yao. Hivyo basi tokea muda yalipofanyika mauziano hayo haiwezekani kufanyika mabadiliko yoyote bila ya wenye kuhusika kuridhia mabadiliko hayo. Suala hili ni la kisheria na ni makubaliano kati ya wahusika hao na ni vyema wakaendelea kuzungumza wawili waliohusika na mkataba huo.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Wizara yangu napenda kueleza kuwa kwa wale waliofanya mauziano ya ardhi kwa lengo la kujengwa minara hawatokuwa na uwezekano wa kufanya mabadiliko ya mikataba hadi pale wahusika watakapokubaliana. Na wale ambao wameingia katika ukodishaji wa ardhi kwa Zantel ninawashauri wawe waangalifu wakati wa kufunga mikataba hiyo.

Msaada mkubwa wa Wizara yangu ni ushauri kwa wale waliouza ardhi zao kwa lengo la kujikomboa nawaomba waendeleo kuwasiliana na uongozi wa Zantel ili kuona kwa kiasi gani wataweza kuwasaidia wananchi hao.

Aidha wananchi wengine waliosalia niwaombe kwamba mambo haya ni ya kitaalamu na hata kisheria. Hivyo ni bora kuchelewa kufanya maamuzi kwa msingi wa kutafuta ushauri ili kujikinga na matatizo yanayoweza kuepukika kama yalivyowakumba wenzao.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika miaka ya nyumba Wizara iliunda Kamati ya kushughulikia minara. Je, kamati ile bado inafanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kamati bado ipo na inaendelea kufanya kazi yake chini ya usimamizi wa Mwenyekiti wake ambaye ni Mkurugenzi wa Mawasiliano aliyepo katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kamati inaendelea kufanya kazi

yake na ni utaratibu wa kawaida na wala sio kamati ya kufa na kufufuka ni kamati ya kudumu katika utendaji wake wa kazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na kwa kuwa minara ya Zanzibar imejengwa katika huduma za jamii ikiwemo katika Skuli ya Hamamni.

- (a) Je, Skuli ya Hamamni ile inanufaika kwa kiasi gani.
- (b) Kwa kuwa SMZ imeingia ubia na Kampuni ya Zantel, unaweza kutwambia mwaka 2011/2012 serikali imepata kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika,

- (a) Kampuni ya Zantel wakati ilipoanzishwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitakiwa kutoa mchango wake, miongoni mwa michango yake ni maeneo manne ambayo yalijengwa minara ukiwepo eneo la Fumba, Tumekuja, Hamamni na eneo la Vuga. Skuli ya Hamamni mnara uliokuwepo pale ni miongoni mwa michango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika uanzishwaji wa Kampuni ya Zantel. Kwa hivyo kama kuna fidia, kama kuna mapato yatakuwa yanakwenda moja kwa moja katika serikali kwa sababu ni sehemu ya mchango wa uanzishwaji wa Kampuni ya Zantel.
- (b) Naomba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kuweza kujua kilichopatikana kwa mwaka huo uliokusudia Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na wewe kunipatia fursa ya kuniuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali lifuatalo. Kwa kuwa mara baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 wananchi waligaiwa heka tatu za ardhi na kwa kuwa baadhi ya minara imejengwa katika ardhi hii. Na kwa kuwa wananchi hawaruhusiwi kuuza zile heka tatu walizopewa na serikali. Na kwa kuwa baadhi ya wananchi wamejitokeza kudai shamba zao pamoja na mali zao nyengine zilizotaifishwa na kupitia Mahakama wamepata haki zao hizo.

Je, Serikali itasaidiaje ardhi zile ambazo wananchi wameziua kimakosa na kuwauzia Zantel ili zirudi serikalini na hatimaye pengine serikali itataka kutumia kwa matumizi mengine au kama mwananchi kajitokeza kuomba haki yake akashinda Mahakamani hawezi kupata yeye haki yake ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, Kampuni ya Zantel kwa sehemu kubwa kati ya minara yake 80 iliyokuwepo Unguja, minara 53 ni viwanjwa ambavyo wamepangishwa na Serikali. Kwa Pemba karibu minara 38 wamepangishwa na Serikali. Sasa minara hii iko ya aina tatu, kwa maana ya kwamba ipo ile ambayo wamepangishwa na Serikali, ipo ile ambayo imechangiwa na serikali na ipo ambayo Kampuni ya Zantel imepangwa kwa wananchi.

Kama mwananchi alipewa hati ya matumizi ya ardhi anayo haki ya kutumia ardhi hiyo lakini hana haki ya kuuza. Miongoni mwa hii minara 13 ambayo Zantel walizujiwa ardhi, sina hakika kama ipo katika maeneo ya Mashamba ambayo wananchi walilipwa kwa ajili ya matumizi yao watakuwa wameuza, jambo ambalo litakuwa ni kinyume kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi. Lakini ikiwa minara 13 hii waliozua wananchi kuwauzia Kampuni ya Zanteli iko nje ya Mashamba nadhani ni uhuru wao na hawajatenda kosa. Msingi mkubwa wa Serikali kama tulivyoeleza tunachoweza kufanya Serikali ni kuwashauri kwamba utaratibu wa upangaji wa ardhi ni vyema wakawa watulivu, wakawatafuta watu wakawasaidia kisheria, ili kuepukana na matatizo kama haya. Migogoro hii ipo mingi kwa msingi kama huo kwamba leo wameuziana shs 5/- kesho thamani imeongezeka anataka kuuza Sh. 10/- utaratibu wa mkataba alioufunga unamzuia kufanya hivyo.

Ushauri wa Serikali kwamba wafate taratibu ziliopo na anayehisi kwamba hakutendewa haki, Mahakama ipo aende akadai haki yake.

Nam. 22

Wanyama (Mifugo) Waharibifu wa Mazao ya Kilimo

Mhe. Hassan Hamad Omar – Alijibu:-

Pamoja na juhudi za Serikali za kuboresha na kuweka kipaumbele katika kilimo, kumekuwepo na usumbufu mkubwa kwa wakulima hao kuharibiwa kwa makusudi vipando vyao na kuwakatisha tamaa wakulima hao.

Mhe. Waziri ni hatua gani zitakazochukuliwa dhidi ya wananchi wenye wanyama hao kwa kuwaharibia wakulima vipando vyao kwa makusudi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu inashajihisha ufugaji wa mifugo michache iliyobora kwa njia za kitaalamu kulingana na uwezo wao ambao unatija kuliko kuchunga mifugo mingi ambayo uzalishaji wao ni mdogo, matokeo

yake inazurura ovyo na kuharibu mazao ya wakulima na kusababisha migogoro.

Mhe. Naibu Spika, inapotokea mifugo ya mtu yeyote kufanya uharibifu wa makusudi kwa vipando vya wakulima, uongozi wa shehia kupitia masheha unachukua hatua za kisheria zinazotumika katika eneo husika na kumlipisha mfugaji husika gharama iliyofanywa na mifugo yake na kulipwa mkulima aliyeharibiwa mazao yake.

Wizara yangu huwashauri wafugaji kudhibiti mifugo yao ili isiwatie hasara wakulima na kujitia makosani.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri pamoja na majibu yako mazuri. Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko makubwa dhidi ya wakulima wa Unguja na Pemba. Waunguja hapa kuna malalamiko sana hapa Mwera na Mhe. Rais wa Zanzibar Dokta Ali Mohammed Shein aliwatolea mkazo sana wanyama kuzurura ovyo. Lakini mpaka leo ukitembea barabarani unawakuta wanyama wanatembea ovyo. Si hivyo tu wenye wanyama hawawathamini wenye vipando vyao na wanawaharibia kwa makusudi.

Je, ni lini Wizara yako itakomesha wenye wanyama kwa kuwakatisha tamaa wakulima wetu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ni kweli yapo malalamiko mengi na upo usumbufu mkubwa juu ya wakulima na wafugaji. Lakini mimi niseme tu kwamba sisi kama Wizara ya Mifugo ni wajibu wetu mkubwa kuwashajihisha kama nilivyosema awali kwamba tunachokifanya sisi ni kuwashajihisha wafugaji. Unamkuta mfugaji pengine ana ng'ombe 20 na anashindwa kuwadhibiti. Ng'ombe wale huwezi kuwatafutia majani pahali pamoja inabidi ni lazima uwatoe wende nao katika msafara pengine masafa bila shaka unakuwa huwezi kuwadhibiti na wengine ni lazima wataingia katika vipando vya watu.

Tunachokifanya hivi sasa ni kuwashajihisha wafugaji wale wale tunampa pengine ng'ombe wake wawili tu au mmoja ambaye mwenye tija zaidi kuliko wale kumi pengine. Leo kuna ng'ombe pengine mmoja tu pengine anazalisha lita 10 kwa siku. Pengine unao kumi lakini hupati hata hizo lita 10 kwa siku. Lakini huyu ng'ombe mmoja ambaye tunampa yeye hana haja ya kupelekwa hata kwenye malisho, yeye unamjengea, unamtafutia majani unamlisha pale pale. Kwanza unaepukana na ule usumbufu, halafu kuja kujitia makosani.

Ndio maana tukasema hayo makosa ambayo utayafanya huko hayo sisi yanakuwa hayatuhusu sisi, itakuwa ni yako mwenyewe binafsi, wewe na yule mkulima, mtafikishana kwa Sheha kesi juu yenu, sisi hatuingilii kesi za kibinafsi. Tunachokifanya sisi kama Wizara ni kuwashajihisha waachane na ufugaji wa mifugo mingi na tunampa mmoja au wawili kama ni kuku au bata, mbuzi au ng'ombe basi.

Tumeona mifano tele, tumetembelea mashamba tele, kuna mtu ana ng'ombe wake wawili au watatu tu, mwenyewe ana wamudu ana wadhibiti vizuri na anasema *Alhamdulillah* hivi sasa tija naiona. Kulikoni pengine alipokuwa na ng'ombe pengine 10 anahangaika.

Kwa hivyo Mhe. Hassan ni kweli kuna usumbufu mkubwa na sisi vile vile tunakaa na wafugaji zaidi na zaidi kuwapa taaluma ili waingie katika njia mbadala au njia za kisasa kabisa ambayo ina tija zaidi. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Serikali yetu imetoa wito kwa sekta ya kilimo na kwa kuwa Mhe. Waziri wa Kilimo anahangaika sana kwa kuwapatia wananchi wake nyenzo na utaalumu wa kuzalisha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya ndani ya chakula. Na kwa kuwa wanyama wamekuwa wakiharibu na hakuna hatua zinazochukuliwa, Sheha wala Polisi hana hukumu ya mwenye mnyama.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kutoa tamko kwamba mnyama ambaye amekamatwa kwenye shamba la mkulima, mnyama huyo awe ni mali ya mkulima.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, hayo sasa hivi ni masuala ya baina ya mfugaji na mkulima, kwa hivyo kama mkulima ameingiliwa ndani ya shamba lake basi ana haki ya kumpeleka Mahakamani, au kama mwenyewe wataelewana watahukumiana wenyewe. Kwa sababu sisi yale inakuwa si kazi yetu kwa kweli, sisi kazi yetu ni kumshajihisha mfugaji yule aingie katika njia bora ya ufugaji ili aepukane na makosa kama yale. Nafikiri Mhe. Hija amenielewa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi asubuhi ya leo kuweza kumuuliza Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri tena matamu mno naomba kumuuliza maswali mawili.

Swali la kwanza je, Mhe. Waziri katika kumbukumbu zako kwenye wizara yako hakuna sheria ambayo inaonesha kuwa mnyama akiharibu kitu mtu alipe

faini. Lakini kama ipo au hakuna huoni kama ipo haja sasa katika Baraza hili tukufu ukaleta sheria hiyo kali ili ikaweza kuwalinda hawa wakulima.

Lakini swali la pili, Mhe. Waziri ulipojibu katika swali ambalo la kuwa kuna wafugaji wengine wana ng'ombe wengi kabisa, lakini huoni kama kuna haja sasa hivi kule kwenye Shamba la Pangenji ukawapeleka hawa wafugaji wenye ng'ombe wengi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, sheria zipo bila shaka kwa hivyo mtu kaingiliwa ndani ya shamba lake basi una haki ya kwenda kumshtaki. Ziko kesi tele tu na watu wanalipana huko huko.

La pili, ni kweli tunayo mashamba lakini nisingependa kutumia njia hiyo, tumeona ni bora mfugaji ana mnyama wake pengine ana ng'ombe au mbuzi tunachofanya sisi ni kwenda kumsaidia njia za kiutaalamu. Pengine kwenda kupandishia ng'ombe wake au mbuzi ili apate chotara yule ambaye atampa tija. Wengi tumefanya hivyo na wengi hivi sasa wameshajiika na wanawaita wataalamu wetu mawilayani kwenda kuwapandishia mbuzi au ng'ombe wao ili wapate chotara na wapate tija. Kwa hivyo, nafikiri hiyo itakuwa ni njia ambayo inafaa zaidi kuliko kwenda kuwapeleka wote kule itakuwa haileti maana. Ahsante.

Nam. 68

Kilimo cha Migomba Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kilimo cha Migomba kimeonekana kustawi vizuri Kisiwani Pemba, lakini wakulima wake bado wanaonekana kuendelea na kilimo cha asili bila kuzingatia kilimo bora cha migomba.

- (a) Je, Wizara ya Kilimo ina mpango gani wa kupeleka kilimo bora cha migomba kwa wananchi wa Pemba.
- (b) Kwa kuwa ndizi za Pemba zinaonekana kuwa na soko kubwa Zanzibar na Tanzania Bara hasa za mkono mmoja. Je, serikali ina mpango gani wa kuimarisha kilimo hicho ili Zanzibar iweze kutumia soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- (c) Kwa kuwa vijana wengi hawana ajira Kisiwani Pemba, serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo vijana ili watumie

kilimo cha migomba katika kupambana na tatizo la umasikini wa kujipatia kipato.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa kilimo cha migomba kinastawi sana katika Kisiwa cha Pemba kama ilivyo katika baadhi ya sehemu ya Kisiwa cha Unguja. Kwa kuelewa umuhimu huo Wizara ya Kilimo na Maliasili imetoa kipaumbele kazi za utoaji wa mafunzo ya kitaalamu ya kuimarisha uzalishaji wa zao hili ili wakulima waongeze uzalishaji na tija na wajikwamue kutokana na umasikini. Wizara ilibuni miradi mikubwa miwili mradi wa *PADEP* ulianza mwaka 2004 na mwaka 2007 Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo *IFAD*.

Mhe. Naibu Spika, Mradi wa *PADEP* ulianzishwa skuli za wakulima ambapo wakulima walipewa mafunzo ya kilimo kuanzia kupanda hadi kuvuna na wakulima waliweza kuzitumia mbinu za kilimo kwa ubora waliojifunza katika mashamba yao. Mpango huo wa skuli za wakulima umeleta mafanikio makubwa katika kugeuza uzalishaji wa mazao ya chakula na wakulima wengi hivi sasa wanafanya mbinu zilizo bora.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na miradi na programu hizo, kilimo cha migomba kinaendelea kuimarika na uzalishajiwa ukiongezeka. Hili limethibitishwa na timu ya teknikali ya ufuatiliaji ya Mfuko wa *IFAD* iliyokuwepo nchini kuanzia tarehe 21 mpaka 27. Pamoja na mambo mengine imeridhika na ufanisi uliopatikana kupitia programu hizi ongezeko la tija na uzalishaji wa mazao ya muhogo na ndizi.

Ni kweli ndizi za Pemba zina masoko ya kutosha nje na ndani ya Zanzibar, hivyo ni juu ya wakulima wenyewe kuongeza juhudi katika uzalishaji na kuyatumia kikamilifu mafunzo waliyoyapata ili wayatumie ipasavyo kwenye masoko hayo.

Mhe. Naibu Spika, vijana ni miongoni mwa wale walengwa katika mafunzo ya kilimo yanayotolewa kupitia skuli za wakulima Unguja na Pemba. Aidha, wizara hizo taarifa za vijana waliojitokeza kuingia katika kazi za kilimo ambao wamefaidika kuongeza kipato chao kupitia miradi ya kilimo. Kutokana na mafanikio hayo, Wizara ya Kilimo na Maliasili imetayarisha programu na kuhamasisha vijana waweze kushiriki katika kazi za kilimo kwa kuongeza

upatikanaji wa pembejeo, kuanzisha programu za huduma za fedha na mtaji kwa Sekta ya Kilimo na kadhalika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri je, ni vijana wangapi wa Unguja na Pemba ambao wamenufaika na mafunzo hayo ya kilimo cha migomba.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, idadi kamili sina lakini akitaka idadi hiyo nitampatia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Katika kufanikisha kilimo hicho cha migomba na katika kukuza Mapinduzi ya Kilimo, Micheweni kuna eneo ambalo lilikaguliwa na Rais wa Zanzibar na Makamu wa Pili wa Rais katika Shehia ya Mjini Wingwi kukagua eneo na wakasema eneo hili wanataka kulifanya mfano wa kilimo cha kumwagilia cha migomba. Lakini kwa bahati eneo lile azma ile ghafla ilifeli, sasa namuuliza Mhe. Waziri ni sababu zipi za msingi zilizosababisha azma hiyo kufeli.

Je, kama haijafeli ni lini azma hiyo itakamilishwa ili kuona kwa sababu Micheweni ni eneo moja ambalo migomba inakubali kwa wingi sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, suala hilo kwa kuwa mimi sielewi nitapomaliza Baraza hili nitakufuata huko Pemba ukanioneshe hiyo sehemu yenyewe hasa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Subeit Khamis Mhe. Waziri kasema hilo suala halielewi lakini mkimaliza mtakwenda mkaelezane ili hili suala alitekeleze. Tatizo nini?

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, naheshimu kiti chako nakaa kitako.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana kweli kweli aliyoyatoa Mhe. Waziri lakini bado kwa utaalumu uliotolewa kwa hawa wakulima hauwendi sambamba na hali halisi ilivyo. Kwa sababu katika kutembea kwangu nilikwenda Makunduchi na nikapata kuangalia shamba la migomba la Ushirika wa Mhe. Waziri wa Kazi, Uendeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Mhe. Haroun Ali Suleiman ni la aina yake na hata mimi nikaomba kama kuna uwezekano na kule Pemba wakapewe mafunzo kama hayo.

Kwa sababu Mhe. Waziri ni mpya wa haya mambo, haoni kuwa kwa kufanikisha hili suala zima la ukulima wa migomba ni vyema akaonana na Mhe. Waziri amueleze utaalamu wa ziada alioufanya mpaka ikawa ana kilimo cha mfano cha migomba kule Makunduchi.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, sijamfahamu wala sijamsikia vizuri. (*Kicheko*)

Mhe. Naibu Spika: Anasema hivi, yeye alikwenda Makunduchi kwenye shamba la Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika akakuta migomba iko katika hali nzuri na yeye akataka apate wataalamu akafahamishiwe Micheweni au huko anakoishi yeye aweze kufuata utaratibu ule. Sasa anakwambia je, na wewe utachukua utaratibu gani wizara.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, wazo ni zuri. (*Kicheko*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013 – Wizara ya Afya

(*Majadiliano yanaendelea*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tufahamiane kabisa, hivi sasa kuna waheshimiwa 15 wanataka wachangie kwa kipindi cha asubuhi na ratiba yetu jioni tuweze kufanya majumuisho. Kwa hivyo, ningelishauri wale wanaotaka kuchangia wasitoke toke nje nikimwita mtu hayupo sirejei na watu wasirudi mle kwa mle ili tuweze kwenda vizuri tuweze kumaliza bajeti yetu hii wakati wa jioni. Nadhani tumefahamiana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha siku ya leo tukiwa hai. Vile vile nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja nianze mchango wangu kwa kuelekeza katika Idara ya Tiba ukurasa wa 23. Idara hii Mhe. Naibu Spika, inajumuisha hospitali nne za vijiji, hospitali tatu za wilaya, mpango wa damu salama, usafirishaji wa wagonjwa nje ya nchi, mradi wa afya ya akili na chuo cha madaktari Zanzibar. Kwa hivyo, mimi nitazungumzia hospitali nne tu kati ya hizi nne za vijiji halafu nitakuja kwenye mpango wa afya ya akili na chuo cha madaktari.

Mhe. Naibu Spika, nianze na Hospitali ya Chake Chake, Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Chake Chake iko katika mji wa Chake Chake mji ambao upo katikati ya Kisiwa cha Pemba. Kwa hivyo, hospitali hii inapata wagonjwa kutoka katika sehemu zote za Pemba.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nilidhani kwamba hospitali hii itatayarishwa vizuri kusudi kuweza kutoa huduma kwa wananchi kutoka pande zote, lakini Mhe. Naibu Spika, ukiiangalia Hospitali ya Chake Chake inasikitisha mno. Ukiangalia kwa wasifu wa nje ile hospitali haina tofauti na jeneza, kwa sababu jeneza mara nyingi linakuwa limepambwa vizuri huku juu na mengine huwekewa na uwa, lakini ndani kuna maiti, ni pambo la jeneza. Mheshimiwa katika hospitali iliyokuwa haina kiwango basi ni hospitali ile ya Chake Chake. Pale inasikitisha sana kuona kwamba siku za mvua mnauvu ovyo mle ndani ukiachilia lile jengo la maabara jipya, lakini wodi zote za wagonjwa zinavuja.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia pale mbali na changamoto hiyo mpaka zile zana za maabara zimepitwa na wakati, yaani pale ukileta madaktari wa kigeni wanaweza kushindwa kufanya kazi kwa sababu ni zana za tangu enzi zimeshapitwa na wakati. Inasikitisha sana kuona kwamba maabara, ukiangalia *Theatre* zana zake zimepitwa na wakati mno. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze nini kimesibu pale kuonekana kwamba maabara pamoja na *Theatre* hawakuangalii kwa jicho la rehema. Hilo moja.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika hospitali ile la kuvunja moyo zaidi ni kwamba hata wale madaktari au wafanyakazi wa pale wanapopata zile *night call* wewe hata uitwe mara thelathini mwezi mzima uwe unapata *night call* basi unalipwa siku kumi tu, kama umefanya siku thelathini ndani ya mwezi unalipwa siku kumi tu tena kwa kukopwa, hizo siku kumi unaweza ukakaa miezi mitano mpaka sita ndio ulipwe hizo siku zako kumi pengine za mwezi wa Januari ukajalipwa mwezi Juni, ni tatizo. Tunawavunja moyo hawa wafanyakazi wetu na madaktari wetu.

Sasa mimi nilikuwa nataka nijue tatizo ni nini, wamepanga kwamba mtu akienda *night call* analipwa tena kilipo chenyewe sio kikubwa analipwa shilingi elfu mbili tu, akiwa *nurse*, akiwa *AMO*, akiwa daktari analipwa shilingi elfu mbili tu. Hili ni tatizo, nadhani Mhe. Waziri katika hili panahitaji marekebisho makubwa kwa hawa watumishi wetu wa pale Chake Chake na hospitali za Pemba kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kimsigi huduma za afya Pemba ni tatizo, ni tatizo sana na napenda niwaambie hawa watendaji wa Serikali kwamba Zanzibar imefanywa

na visiwa viwili na kutenganishwa na bahari tena yenye mkondo mkubwa wa Nungwi. Sasa unapokuwa huduma huzi-*harmonise* ni tatizo unawabagua.

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda nimsifu huyu Rais wa awamu iliyostaafu ya Dr. Amani Abeid Karume na hata ile Awamu ya Kwanza. Katika ufanyaji wa shughuli zao za kazi walikuwa wakiweka mambo sawa sawa takribani japo si sawa lakini walikuwa wana-*make balance* ile Unguja na Pemba, lakini inasikitisha sana kwamba hivi sasa Wapemba wanakuwa na tatizo. Hivi tunavyosema Mhe. Naibu Spika, Mpemba akienda kufanyiwa *CT-Scan* lazima aje Unguja na vyombo anavyotumia vya kujia Unguja ni *Seagull* ambapo mimi juzi nilikuwa namubiri mgonjwa wangu hapa kumbe kaletwa kwa *Seagull* na ishakwama Nungwi ikabidi atafutwe Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ende akaivute huku na mgonjwa wangu anataka kuja kufanyiwa *CT-Scan*, ilifika sijui saa sita au nane za usiku tukashindwa tena ikabidi siku ya pili hali ikawa mbaya tukampeleka Dar es Salaam. Lazima muone watendaji, kwamba Wapemba nao ni walipa kodi wa nchi hii, tena wanalipa kodi sawa sawa na wenzao wa kisiwa chengine, ndio nikasema katika kutoa huduma kwa Wazanzibari lazima mu-*harmonise*.

Awamu ya Sita ya Amani Karume na awamu yake ile tulikuwa tuna shida hatuna gati, lakini wakatujengea lile tuta sasa tukawa tunakwenda moja kwa moja, naishukuru sana awamu ile. Mzee Karume yule Karume baba naye alikuwa hana mambo ya nini, yeye alijenga maghorofa Michenzani katujengea na Pemba, vijiji vikajengwa Mpapa kule na vijiji Pemba kajenga, maghorofa mpaka Kengeja yako kama haya ya Michenzani. Kwa hivyo, kwa nini huku kuwe na *CT-Scan* kule kusiwe na *CT-Scan*. Hili Mhe. Naibu Spika, ni tatizo kubwa, tunawavunja moyo walipa kodi wa kisiwa cha Pemba na kule Wapemba nao ni walipa kodi na wanalipa sana kodi.

Kwa hivyo mimi naishauri Serikali kwamba ifikirie suala zima la kuweka mambo kama hayo kule Pemba na kwa kweli hakuna sababu kwa sababu kile ni kisiwa chenye historia nzito, kimetoa watu makini sana. Waziri Mkuu wa mwanzo wa nchi hii katika Zanzibar huru alikuwa bwana mmoja anaitwa Mohamed Shamte Hamad Mshirazi katoka Pemba, mwana diplomasia makini na aliyebobea katika ulimwengu huu Salim Ahmed Salim katoka Pemba jamani msikidharau kile kisiwa. Hilo moja.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Chake Chake pale panatakiwa pawe ni *centre nursing care* na *medical assistant* kwa sababu ni kati. Juzi Mhe. Naibu Spika, kuna mfadhili mmoja pale Chake Chake katoa magodoro 100 mfanyabishara huyo, alipoona kenda kuangalia akaona vigodoro vichafu vichafu pale akatoa magodoro mia moja, alipotoa magodoro mia moja Wizara ikatakiwa ifanye *plastic cover* pale juu kusudi mambo ya ugonjwa yasije yakatoka siku hizi

kuna maradhi mabaya wakaambiwa wafanye hivyo, magodoro yale nafikiri karibu mwezi wa sita yametolewa pale. Sisi tukawa tunaangalia kama *watching dog* wa *public fund* tunajua kwa sababu yule jamaa keshasaidia pale Serikalini hiyo inakuwa ni *public asset* kwa vile sisi ni *watching dog* wa *public asset* tukawa tunaangalia angalia mbona haya magodoro hayafanyi kazi.

Mwanangu la kusikitisha Mhe. Naibu Spika, magodoro yale mpaka leo hayajafanyiwa *plastic covering* na magodoro yale juzi yakenda yakalala kwenye mwenge aibu. Haya ni matumizi mabaya, makusudio ya magodoro yale ni kuwapakia wagonjwa sio kwenda kwenye mwenge, kama mwenge hawana pesa walikuwa waje tu waseme sisi tuwachangie hapa, leo wanatumia mali ya nchi yaani fedha za walipa kodi ambazo tumesaidiwa kwenda kupeleka kwenye mambo ya mwenge bwana, yoyote aliyehusika na hili nadhani atupe maelezo Waziri ilikuwa kuwaje, mnatuvunja moyo, mnawavunja moyo wafadhili, wafadhili mnawadharau wenyewe wamekusudia kupata upande huu mnawapeleka upande mwengine jamani ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, tuje katika suala zima la fidia ya ile Hospitali ya Chake Chake tena, changamoto nyengine pale Chake Chake Waziri itabidi aje anieleze. Inaonekana Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya sijui wana *system* yao ya utumishi mbali au vipi, pale kuna daktari dhamana, *DMO*, lakini malipo kwa mujibu wa vile vyeo anavyoshikilia mtu hayatoki, ikiwa analipwa kwa mujibu wa ile taaluma aliyonayo tu, lakini kwa mujibu wa *post wananung'unika* sana wafanyakazi pale Chake Chake.

Kwa mfano, nilidhani kwamba daktari dhamana angeweza kuwa na japo ki *allowance* kidogo hivi kwa mujibu wa ile dhamana, lakini majibu yanakuwa hayako hivyo yako sawa kwa mujibu wa taaluma tu aliyonayo. Lakini dereva wa Afisa Mdhamini Pemba ana shilingi 80,000 kama *driving allowance* lakini huyu daktari dhamana pale hana, hebu atuwekee sana kidogo waziri katika hili. Kwa sababu wanataaluma wanapata shida kidogo wale madaktari wenyewe hapana halafu wewe unampa dereva *driving allowance* lakini huyu *medical officer* humjali, hebu tueleze kidogo kuna nini hapa.

Mhe. Naibu Spika, niende sasa katika suala zima la sera hii ya ardhi, nilifikiria katika bajeti iliyopita ile kwa sababu sera ya mwaka 1999 wamei-*review* anaipongeza sana wizara katika hili. Lakini mimi nilikuwa nafikiria Mheshimiwa Zanzibar ni nchi na katiba yetu inasema kwamba Zanzibar ni nchi, sasa sera ya afya lazima yenye kwa mujibu wa mazingira tuliyonayo sasa ya Zanzibari ni nchi. Kwa mfano, hapa Mhe. Waziri kazungumzia kwamba mazingira, kitengo cha afya na mazingira kimefanya kazi kubwa

lakini katika kuhamasisha katika ukurasa wa 21, kitengo hiki kilikuwa kina kazi kubwa kwa sababu lazima kifanye kazi kwa mujibu wa hali halisi ilivyo.

Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kuna mabadiliko makubwa ya tabia ya nchi, naomba kidogo ninukuu huu ukurasa wa 21. Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 21 ibara ya 29 amesema hapa Mhe. Waziri kwamba, “Kitengo cha Afya na Mazingira kinafanya kazi za kuimarisha, kustawisha na kulinda afya ya jamii kutokana na majanga yanayohusiana na mazingira kwa kutayarisha sheria, kanuni, miongozo na taratibu”. Mwisho wa kunukuu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, majanga ya mazingira ni pamoja na mabadiliko ya tabia nchi. Juzi tu tumepata semina nyingi zinazohusiana na suala la haya majanga yanayosababishwa kutokana na mazingira ya ongezeko la hewa ya makaa. Hata juzi katika bajeti kubwa Waziri wa Fedha katika bajeti yake ametaka wenye gari walipie shilingi elfu kumi na tano kwa mwaka kutokana na gari hizo kuwa zimechakaa zinaongeza *carbondioxide* katika anga.

Sasa Mhe. Naibu Spika, katika hili nilidhani kwamba wizara yetu kwa kushirikiana na hii Wizara ya Fedha basi tungejiweka sawa kukabiliana na majanga, kwa sababu ukiongeza *carbondioxide* kwenye hewa *possibility* ya kupata kensa ni kubwa. *Carbondioxide* inaongezeka sana katika hewa, yaani hewa ya makaa. Kwa hivyo naomba sana katika hili pamoja na mapitio ya sera ya afya lakini vile vile sera ya afya iende sambamba na hali ilivyo kimazingira.

Hivi sasa ikiwa *carbondioxide* ni nyingi katika hewa basi uwezekano wa Wazanzibari kuugua kensa ni mkubwa. Sasa ukiugua kensa, mionzi unakwenda kupigwa Dar es Salaam. Ni lini wizara Mhe. Naibu Spika, itafikiria suala zima la kuweza kuweka kitengo cha kensa pale, tuondokane na hili janga la kwamba kila siku sisi tunaelekea Dar Es Salaam kwa ajili ya mionzi. Hilo ni jengine Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika 5.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa mambo mawili. Kwanza nizungumzie hiki Chuo cha Madaktari. Kwanza niipongeze serikali kwa Serikali ya Cuba kuweza kutuwekea hiki chuo.

Lakini Mhe. Naibu Spika, vile vile kuna changamoto ambazo zinakabili vijana wetu pale, ikiwemo posho halitoshi, vijana wana tatizo la usafiri. Kwa mfano wale wanaokaa Pemba, wanaokaa Vitongoji pale kijijini kwangu kwenye Hospitali ya *Cottage* ya Vitongoji, mimi huwa ninawaona

wanahangaika sana na suala la usafiri kutoka pale *Cottage* mpaka Chake-Chake. Wana tatizo la usafiri kutoka maeneo yao mpaka kwenda katika hospitali kwa upande wa hospitali za Micheweni na hawa walioko Unguja wana matatizo la kutoka hospitali ya Mnazi Mmoja kwenda Kivunge usafiri inakuwa ni tatizo.

Kwa hivyo naomba Mhe. Naibu Spika, wizara hii hawa vijana iwasaidie sana. Ninapongeza kwa bidii yao lakini vile vile wawasaidie kuwapatia huu usafiri kusudi waweze kupata mafunzo yao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, vile vile posho la hawa vijana ni dogo sana, shilingi elfu thamanini haziwatoshi hata kidogo. Hizi shilingi elfu thamanini Mhe. Waziri basi nadhani hata tukimuuliza saa kumi atakuwa hana, kwa sababu akitoka hapo kwenye geti ndio anakutana na jamaa wanataka haki yao. Mimi ninadhani tuwafikirie hawa vijana na serikali ifikirie juu ya hili posho la kuwapa hawa vijana.

Na hawa vijana nitumie fursa hii kuwashauri kwamba serikali yao inawapenda, watulie na waendeleo kuchukua mafunzo. Kama kuna matatizo madogo madogo, mimi ninaamini serikali hii ni sikivu, nyinyi vijana tulieni mupate masomo, serikali itawafanyia marekebisho, ninawashauri hivyo.

Mwisho nimalize Mhe. Naibu Spika, kwa kuipongeza tena hii Serikali ina mpango wa kuanzisha FM radio wanaita *afya FM*. Hii itasaidia sana Mhe. Naibu Spika, niwapongeze tu kwamba hata hotuba yake katika suala zima la kupambana na malaria tumumie hizi hizi redio zetu za kawaida na vyombo vya habari tukaweza tukapata vyandarua. Kwa hivyo katika hili, mimi ninapenda sana nimpongeze sana Mhe. Waziri na timu yake ya wataalamu kwa juhudi na bidii waliyoifanya katika suala zima hili la kuweza kutoa matangazo ya kuhamasisha juu ya utumiaji na kujikinga na malaria.

Na hii imesaidia sana baada ya kumtumia yule msanii nguli katika mambo ya minungu na taarabu Bi. Kidude. Sasa ninapenda sana Mhe. Naibu Spika, wizara itakapoanzisha FM radio itumie *air time* kubwa kumpatia yule ndugu Fatma Baraka (Bi. Kidude), ili aweze kutuelezea mambo yetu, watu wanavutika sana na sauti yake na sisi tumefurahi sana katika hili.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie mwisho kwa pale Vitongoji *Cottage* hospital. Hii hospitali ya *cottage* inataka kuboreshwa lakini mungetupa *formular*. Hii katika hospitali ambayo haifai hata kuwa ya kijiji hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, pale hapana uzio, pale ukenda katika hiyo maabara ni kichocho kidogo tu hivi. Humo *laboratory* mtu aliyepo pale ana

microscope zile za wanafunzi za kufanyia mitihani. Sasa mimi ninadhani mungetupa *formular*, huu mradi wa uboreshaji wa hospitali za wilaya ukaweka kipindi gani mpaka kipindi gani, kwa sababu munatupa maneno tu. Mumeanza kusema mwaka jana, ninakwenda pale Vitongoji Mhe. Naibu Spika, feni limekatika basi limebaki makono hayamo, ninaambiwa hayo yanataka kuboreshwa, yataboreshwa vipi.

Mimi naomba Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba hospitali ya Vitongoji ikiwa munataka kuiboresha kweli kuwa ya wilaya muna kazi kubwa. Hakuna labo, chumba cha kujifungulia wazazi kina kitanda kimoja kidogo.

Kwa hivyo naomba Mhe. Naibu Spika, katika hili mutupe basi, kwa sababu kama ingekuwa ule utaratibu wa PPB tungejua programu basi bajeti yao ya kuziboresha hizi hospitali ni kuanzia kipindi hiki mpaka kipindi hiki. Naomba Mhe. Waziri atwambie hasa hizi za vijiji zitaanza kuboreshwa mwaka gani na kuwa za wilaya, halikadhalika hiyo hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa.

Kwa hekma, taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu Mhe. Naibu Spika, ninaunga mkono hii hoja ya Mhe. Waziri wa Afya asilimia mia kwa mia. (*Makofi*).

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza ninamshukuru *Allah* kwa kutupa uhai, uzima na taufiq ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu.

Pia ninawashukuru sana wananchi wote wanaoishi katika Jimbo la Ziwani, kwa kuendelea kutupa moyo na kutupa nguvu katika kutekeleza kazi zetu. Kwa hivyo kwa niaba yao naomba niwasilishe maoni yangu kuhusu bajeti hii ya Wizara ya Afya katika kikao hiki cha bajeti ya 2012/13.

Kwanza ninapenda niseme kwamba wizara hii ilikuwa ikiitwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, lakini ikaondolewa mzungo ule na ikawekewa Wizara ya Afya tu. Kwa hivyo jukumu kubwa la Wizara ya Afya lilikuwa ni mambo mawili tu makubwa. Kuweza kutengeneza afya za watu wetu, kutoa huduma ili afya za watu wetu ziweze kuwa nzuri.

Kwa hivyo kulikuwa na sehemu ya matibabu ambayo ndio mwisho, lakini mwanzo inaanza na kinga. Kwa hivyo ninapenda sana kumueleza Mhe. Waziri kwamba suala la kinga katika wizara hii ni suala muhimu sana, kwa sababu matibabu ni sehemu ya mwisho ya kuwa umeshashindwa kuondoa jamii katika maradhi na unawatibu. Lakini kabla hujawatibu unaweka kinga.

Nitatoa mfano Mhe. Naibu Spika, ambao upo hai kabisa. Tulipokuwa tuna malaria, nyinyi mulifanya hesabu ndani ya wizara ni jinsi gani Wizara ya Afya tu peke yake ilivyokuwa ikigharimika kutibu malaria. Na sio nyinyi tu Wizara ya Afya ndio iliyokuwa ikigharimika, lakini familia yenye watu akiumwa mmoja maana yake watu watatu au wawili hawana kazi siku ile kutwa kumuhudumia yule mtu kama siku mbili au tatu.

Sasa ina maana tulikuwa tunapoteza nguvu kazi, muda mrefu kwa maradhi mamoja tu ya malaria. Lakini kwa uwezo wa Alla tuliposhirikiana na nguvu zilizofanywa na wizara hii, malaria ikapungua kwa kiwango kikubwa. Nyinyi wenyewe ni mashahidi mutakapofanya hesabu ni kiasi gani wizara imepunguza kununua dawa na imepunguza msongamano wa watu wanaokuja kujitibu malaria. Sasa katika mipango yote ya wizara hii, ufuatiliaji wa maradhi yanayoweza kukingika yakapewa kinga ni kitu muhimu sana katika taifa. Hilo la mwanzo.

Lakini kabla sijaingia katika wizara yenyewe ninapenda sana niilaumu serikali kwa jumla. Tunapoingia katika mikataba ya kimataifa kuna maana yake. Wizara zote za afya zilikutana *Abuja, Nigeria* mwaka 1992, na zikapitisha azimio kwamba itakapofika mwaka 2014 bajeti za wizara ya afya katika nchi hizi za Afrika ziwe asilimia 15 ya bajeti ya serikali.

Lakini tumeona kwamba bajeti ya Wizara ya Afya inaendelea kudorora sio kwamba inapanda kulinganisha na bajeti ya serikali. Kwa mara hii kwa hesabu za chapuchapu si zaidi ya asilimia 3.5 ya bajeti ya serikali.

Sasa kwa bajeti ya aina hii tunategemea papatikane nini, wakati ulimwengu ulipokutana ukaamua kwamba angalau ikifika mwaka 2014 basi bajeti za Wizara ya Afya ziwe kwenye asilimia 15 ya bajeti ya serikali. Sasa sisi tunazongana kwenye asilimia 3.5. Hilo ni kwa upande wa serikali.

Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Waziri kwa sababu makala iliyotolewa na Umoja wa Mataifa iliwataka Mawaziri wa Afya wawe sugu katika kupigania bajeti serikalini. Kwa hivyo ninamuomba sana Waziri wa Afya anapokwenda ku-*defend* bajeti yake katika Baraza la Mapinduzi achukue data kamili za ulimwengu na izewe kuipigania bajeti ya Wizara ya Afya. Bila ya hivyo tutaendelea kudumaa.

La tatu Mhe. Naibu Spika, ninapenda nizungumze kuhusu idara mbili katika Wizara ya Afya. Kuna Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Idara ya Utumishi na Uendeshaji.

Ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja atufafanulie, hakuna mchanganyiko wa malengo katika idara mbili hizi. Tunaposoma kwenye kitabu hiki cha Mhe. Waziri wa Afya, mwanzo katika *paragraph* ya mwanzo na baadae anapoeleza kuhusu idara mbili hizi, naona kama kuna mchanganyiko wa majukumu.

Kwa mfano, Idara ya Utumishi na Uendeshaji katika ukurasa wa 53 na 54 ya kitabu hiki, imepewa majukumu ambayo sikuyaona kwamba ni ya idara ile. Kwa sababu sentensi ya mwanzo *paragraph* ya mwanzo inayoeleza kuhusu majukumu ya idara hii, inaeleza kuhusu wafanyakazi tu, nidhamu zao, uwajibikaji wao lakini baadae chini ya utawala na uendeshaji yanakuja mambo ya kushughulikia sheria, ufundi.

Sasa naona mambo haya yanaekwa katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji yanahusiana na nini, wakati haya yangelikuwa katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, ndio mambo yao ya kushughulikia mambo ya sheria, wao wangeachiwa majukumu ya wafanyakazi tu. Kwa sababu mambo mengi yanayozungumzwa humu Mhe. Waziri na Wajumbe wengi ni kuhusu utendaji wa kazi wa *staff* katika ngazi tofauti, madaktari wapo hivi, ma-*nurses* wapo hivi.

Sasa idara hii ingebebeshwa jukumu hili ikaona kwamba jee *staff* wao wanatosha, wanakwenda *training*, wanafanya kazi zao. Lakini ikibebeshwa majukumu mengine ambayo yangeliangukia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inakuwa sasa malengo yale ndiyo yanakosekana. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri katika hali hii hakuna mchanganyiko wa majukumu, halafu ikawa hawa wanapewa majukumu yaliyokuwa sio yao.

Ukitazama katika ukurasa wa 57, malengo ya idara hiyo hiyo mwaka 2012/13. Lengo la (e) Kusimamia maandalizi ya kufikisha rasimu ya sheria ya afya. Sasa hii ni kazi ya Idara ya Utumishi? Halafu lengo (f) Kuendelea na matengenezo ya miundo mbinu ya wizara kama vile majengo, vifaa, maji, umeme na kila inavyohitajika. Sasa Mhe. Waziri hapa unatukanganya. Hii Idara ya Utumishi na Uendeshaji ni shughuli yao watumishi tu na namna gani ya ku-*promote* yaani *human resources development work*.

Sasa unapowapa na majukumu mengine ambayo inayaondosha kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, afadhali ingeundwa kitengo chengine kikashughulikia mambo haya kama kuna haja hiyo, lakini kuwapa hawa hawa majukumu yao unababaisha majukumu.

Mhe. Naibu Spika, jengine nilikuwa ninazungumza kuhusu hii maabara ya Mkemia Mkuu. Mimi ningelimuomba Mhe. Waziri akajua akatueleza, sasa hivi

tunajua kwamba Mkemia Mkuu yupo, lakini jee ina wafanyakazi wangapi ambao sio wa utawala. Hii Idara ya Mkemia Mkuu ina wafanyakazi wangapi ambao sio wa utawala, ni wale wasaidizi wa Mkemia Mkuu wapo wangapi na wamepata mafunzo gani.

Lakini mimi ninamjua huyu Mkemia Mkuu wa sasa. Mwanzo alianza kuwa ni mwalimu. Jee, Wizara ya Afya ina mpango gani wa kujenga uwezo wa kujenga hawa *staff* wao kwa kumpa uwezo yeye kuwasomesha ndani *interservice training*, kwa sababu yeye anao uwezo wa ualimu wa ngazi ya juu kabisa, angeweza kuwasaidia hawa wakati wamo kazini. Jee wizara hii imetengeneza mpango gani kwa njia hiyo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, tumebahatika kuwa na Kitengo kinachoitwa Maabara ya Afya ya Jamii kiliopo Wawi pale Pemba. Sasa mimi ninamuuliza Mhe. Waziri pamoja na maelezo yaliyoelezwa ndani ya kitabu, kisheria kitengo hiki au maabara ipo wapi katika wizara? Ina *legal status* gani na ikiwa hakuna sheria iliyoiweka, jee hakuonekani kwamba imeshafika wakati sasa wa kuiweka kisheria ile taasisi.

Kwa sababu mambo ya kiulimwengu hivi sasa yanakwenda kisheria, na tumeona taasisi nyingi ambazo zilikuwa hazijawekwa kisheria inakuja moja moja humu toka tulipoanza hasa Baraza la mara hii, zinaekwa kisheria. Kwa hivyo tunaomba utueleze kwamba inayo uwezo wa kisheria, ni taasisi inayojitegemea au taasisi gani, na imeshaekwa vigezo vyake vya kisheria na kama upo mpango huo basi utafanyika lini.

Mhe. Naibu Spika, moja katika jambo ambalo lenye jukumu la wizara hii ni kwamba kuna hospitali tofauti. Nikianza hospitali ya Mnazi Mmoja ya Rufaa, kuna hospitali hizi za wilaya na nyenginezo ziliopo kwenye vituo vya afya.

Jee ni utaratibu wa aina gani unaotumika katika ugawaji wa zana za uchunguzi. Kuna vyombo vinaagizwa kwa ajili ya wizara, halafu kuna ugawaji au zinaagizwa kwa ajili ya hospitali fulani vikifika ndio vimeshafika.

Kwa mfano katika jibu lako ulisema kwamba kuna *incubators* tano zimekuja. Jee hizi zitaekwa pahala pamoja au kuna na pahali na hospitali nyengine zitapelekwa ambako hakuna. Sasa ule utaratibu wa ugawaji wa zana ni kitu muhimu sana, kwa sababu ya kuona kwamba kutokana na takwimu ambazo umeeleza humu kuwa zinapokelewa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ndio wanaoweka takwimu. Jee takwimu zile zinafuatiliwa ili kuona pahali fulani pana ugonjwa wa aina fulani unaojitokeza sana na kwa hivyo wanahitaji zana fulani?

Mhe. Naibu Spika, kabla halijatokezea tatizo la ICU kwenye hospitali ya Mnazi Mmoja, mimi katika kipindi kilichopita cha miaka mitano yote nilikuwa ni Waziri Kivuli wa Afya, na kwa hivyo baadhi ya mambo mengi tulikuwa tukiandika ninayajua chanzo chake. (*Makofi*).

Katika baadhi ya *papers* za mwisho nilikuwa nikisisitiza sana kuhusu upatikanaji wa ICU katika hospitali moja wapo ya Pemba kwa kuanzia. Nilisema moja katika hoja za mwaka jana kwamba mara hii sisemi kuhusu ICU kwa sababu *kilemba kimeroa jee mkuti*. Waswahili wanasema ikiwa kilemba kinaroo, jee mkuti. Maana Hospitali ya Mnazi Mmoja ninataka kuidai ya Pemba.

Kwa hivyo tunakushukuru sana na tunakupongeza kwa juhudi kubwa ulizozichukua hospitali ya Mnazi Mmoja ikapata ICU, na ninategemea zitakuwa mbili au tatu lakini baada ya hapo ifikirie hospitali moja wapo ya Pemba kuweka ICU.

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika 5.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, ninaendelea.

Mhe. Naibu Spika, ugawaji wa vifaa vya kila siku, kwa sababu kuna zana na vifaa vya kila siku, yaani *utilities* unakwenda njia ngani. Ikiwa ni magodoro au mabedishiti, zana za usafi zinakwenda vipi. Kila hospitali inajitegemea kwa njia yake au kunakuwa na *central system* ambayo inagawa mambo haya.

Kuna malalamiko makubwa kuhusu upatikanaji wa *anti tetanus* katika hospitali za serikali hususan Pemba. Jee Mhe. Waziri unalijua tatizo hili na wanaoathirika ni watoto pengine wanaojikwaa na misumari, mabati na mambo mengineyo. Kwa hivyo moja katika jambo ambalo na mara nyingi humalizia katika vituo vya afya vya kulipia. Jee suala likoje.

Lalamiko jengine liliopo hata katika ITV nililisikia siku moja likijadiliwa. Wale wanaopata ajali mpaka wapate PF 3 kutoka Polisi. Hii ni haki ya kutibiwa yule mtu au jambo hili limeshafanyiwa mjadala. Wakati yeye amepata ajali na damu zinamchiriza. Jee, kutibiwa kwake mpaka kupatikane PF 3 bado ni halali au kuna utaratibu gani mwengine ambao ungefanywa, ili yule mtu akatibiwa na mambo mengine yakashughulikiwa. Jee, Mhe. Waziri una kauli gani kuhusu hili.

Mhe. Naibu Spika, ninakuja katika Chuo cha Afya Mbwani. Mhe. Naibu Spika, mimi ninasema tuone fahari kubwa sana kwa kuwa na Chuo cha Afya Mbwani. Kwa kweli *system* ya uendeshaji wa hospitali bila ya kuwa na Chuo

cha Afya ingekuwa ngumu mno. Kwa hivyo ninashukuru jitihada za wizara za kukitunza kile chuo.

Sasa tunachokiomba ni uangalizi mkubwa wa ufuatiliaji wa uendeshaji wake. Jee uendeshaji unaridhisha. Kuna wale wanaosema wanalipishwa bila ya huduma zinazofaa. Jee suala hilo lipo. Kuna wale wanaosema kwamba wao tayari ni wafanyakazi wa Wizara ya Afya, lakini wanakwenda kufanya *up grading courses* bado wanalipishwa na fedha nyingi. Je, hiyo vipi kufanya *in service training* bado wewe unalipa tena fedha nyingi na tayari ni wafanyakazi, kwa sababu kuna wale ambao ni wapya kabisa hawajaajiriwa, ni sawa. Lakini je hawa ambao tayari wameshaajiriwa wanafanya *up grading course*.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba Wizara ya Afya kwa ujumla ibadilishe mikakati na kuweza kuwapatia wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya vitambulisho vya kuweza kuonekana yeye ni nani katika hospitali. Hata zile *department* basi rangi zake za vitambulisho zitofautiane. Kwa sababu Hospitali ya Mnazi Mmoja ni *congested*, kwa hivyo ukitaka kuuliza swali pengine ujue kwamba huyu ndiye wa *department* hii niliyokwenda, usimulize mtu mwingine na yeye mwenyewe akitoka katika sehemu yake ya kazi akienda sehemu nyengine iwe anaona kuwa anaonekana, kwa sababu ndio italeta ile heshima ya ile kazi.

Mwisho kabisa mimi fikra yangu ni ya zamani sana lakini bado ninayo, kwamba tukate eneo, tuanzishe *department* moja moja ambazo baadae tutaweza kwenda katika hospitali ya rufaa. Mimi nasoma katika makala nyingi zilizoandikwa hata hii ya juzi mliotupa nimesoma ndani yake imeandikwa hivi, “*review of the essential as per package*”. Wengi wanakubali kwamba hospitali ya Mnazi Mmoja ipunguziwe mzigo zijengwe hospitali nyengine, ili ile ya Mnazi Mmoja ipunguziwe mzigo iendelee kuwa ya rufaa. Lakini mimi nasema jambo hilo halitatokea, kwa sababu ya mazoea. Kwa sababu ya mazoea hata ukiifanya ile ya rufaa kwa jina lolote utakaloliita, watu wa kawaida watakwenda tu. Njia ya pekee ya kuisaidia hospitali ya rufaa ni kutafuta eneo ikaanza kweli hospitali ya rufaa. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya. Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza na Idara ya Kinga na Elimu ya Afya. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya ni moja kati ya wizara zenye vitengo vingi, ambavyo mtu yeyote kwa kuvichangia kwa wakati mmoja hawezi kuvichangia kwa pamoja. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, na mimi nitachangia sehemu moja tu ambayo nadhani Mhe. Naibu Waziri ataifahamu kwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, katika idara ya kinga tumeelezwa kwamba maradhi mengi yanayokingwa, lakini sikufahamu namna ya maradhi hayo yalivyofanikiwa katika kutekelezwa, isipokuwa maradhi ya malaria tu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano kufikia hadi Machi 2012 watu waligunduliwa na vimelea vya malaria kwa Unguja na Pemba ni asilimia 08.7. Lakini Mhe. Waziri hajatueleza kuhusu maradhi mengine yanayosimamiwa na idara hii yako katika kiwango gani, na baadhi ya maradhi hayo yakifuatia kama ukimwi, kifua kikuu, maradhi ya moyo na pia kisukari. Mhe. Waziri maradhi haya hakutupa ni asilimia ngapi ambayo imefanyika ili tupate kuielewa.

Mhe. Naibu Spika, malaria imepungua kwa kiasi kikubwa sana, ingawa hapo zamani yalionekana kama ni donda ndugu, lakini kwa kiasi kikubwa maradhi haya yamepungua vizuri sana. Naamini kupungua kwa malaria Mhe. Naibu Spika ni kutokana na juhudi za serikali na wizara, huku misaada ya wahisani ikipitia mpango wa malaria ukitoa msukumo mkubwa. Kwa hapa naamini Mhe. Waziri wamefanikiwa sana kuhusu malaria. Lakini suala langu liko hapa, ni kwa nini mpango kama huu usitekelezwe au usielekezwe kwenye kifua kikuu na ukoma, nayo tukapata ni asilimia ngapi ambayo imetekelezwa na sisi wananchi tukajua.

Mhe. Naibu Spika, kama Zanzibar inawezekana bila malaria, kwa nini Zanzibar bila ya ukoma isiwezekane.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kitengo cha upasuaji Mnazi Mmoja, kuna malalamiko mengi Mhe. Naibu Spika. Kwanza kitengo hiki kina upungufu mkubwa wa madaktari wa upasuaji, hapa wako madaktari wawili tu ambapo mmoja ni Dk. Malik na mmoja ni Dk. Yunus na huyo Dk. Malik ni Mkurugenzi. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, inapotokea dharura ya upasuaji, ikiwa hayuko Dk. Malik inakuwa ni tatizo kubwa. Pia kuna wakati mwengine anahitaji mapumziko, itabidi wakati ule Mhe. Naibu Spika, afuatiwe nyumbani, kwanza kabla ya kutibu mtu ajitibu yeye, kwa sababu wakati ule anataka apumzike inabidi aje hospitali kufanya kazi kama hiyo. Mhe. Naibu Spika, hii ndio hali tuliyonayo kutokana na upungufu wa madaktari tulionao hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, vile vile wanaofuatia ujuzi wao huwa ni mdogo sana. Ikiwa hayuko daktari huyu tumuonee huruma, ni lazima tutafute madaktari tuwasomeshe ili nchi yetu iwe na wataalamu walio bora, tukiwa na daktari mmoja jamani tutamuua kabisa, hawezi kufanya kazi hivyo, pengine kafanya kazi sana saa sita ya usiku keshapumzika anakwenda kuitwa tayari dharura imetokea aje atibu, hilo litakuwa ni tatizo kubwa Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, serikali ijitahidi kupeleka madaktari wetu kuongeza ujuzi zaidi, ili Zanzibar tuwe na wataalamu walio bora.

Mhe. Naibu Spika, wako madaktari wa kigeni katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Kama madaktari wa Kichina na wengine. Lakini madaktari hawa hufanya kazi mpaka inapofika saa 4:00 huwa tayari wameshasitisha. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana, laiti kama tungekuwa na madaktari wetu hapa, tusingekuwa na haja ya kutafuta madaktari wa Kichina ambao ikifika wakati wao wanaondoka huku wagonjwa bado wapo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kipimo cha *echo*. Hebu Mhe. Waziri nieleze kuna utaratibu gani maalum wa kulipa shilingi 20,000 na wengine hulipa shilingi 30,000, Mhe. Waziri, tueleze hiki kipimo hasa bei yake ni ipi, ili wananchi wetu wasipate usumbufu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kitengo cha *laboratory*. Kitengo hiki kwa kweli kinahitaji wakati wowote kiwe kipo wazi na kiwe kinahudumia watu. Lakini Mhe. Naibu Spika, inapofika saa sita tu kitengo hiki huwa kinasitishwa, isipokuwa kipimo cha wingi wa damu, kipimo cha mkojo na kipimo cha malaria, hivi utavikuta viko wazi. Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazofanya kusitishwa kabla ya wakati kitengo hiki?

Mhe. Naibu Spika, nije katika Hospitali ya Abdalla Mzee. Katika ukurasa wa 24 hapa Mhe. Waziri anasema, hivi sasa wizara inasubiri ujio wa wataalamu kutoka China kuja kutembelea hospitali hiyo na kufanya tathmini kamili ya gharama na maeneo yanayohitaji kujengwa na kutengenezwa. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hii hospitali ya Abdallah Mzee kwa kweli imeshazeekea sio ya leo. Hata ukiifanyia ukarabati mimi nadhani bado itakuwa na matatizo, kwa sababu hatimaye hospitali hii inaweza kuja kutokea matatizo kwa kukarabatiwa kila siku, ikabidi badala ya kujenga ufa basi tujenge ukuta. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali jitihada za makusudi zifanywe ili hospitali ya Abdalla Mzee ibadilishwe na iwe ya hadhi, ili tuondokane na majengo haya ya kizamani, hospitali ile imeshachoka.

Jengine nije kwa madaktari katika Hospitali ya Mkoani Mhe. Naibu Spika, madaktari ni kidogo sana na wafanyakazi pale ni kidogo. Kwa hivyo, wanahitaji waongezwe pale ili wagonjwa wetu wanapokwenda watibiwe

vizuri. Utawakuta wako madaktari kama nilivyosema, pia iko siku wagonjwa huzidi kupita kiasi, utaona huruma, daktari huyu anavutwa huku na kule, hatimaye na sisi tunasema kwamba madaktari hawafanyi kazi, sio kweli. Madaktari wanajitahidi kwa uwezo wao, palipo na sifa wapewe wakati mwingine na palipo na madhara pia waambiwe. Lakini madaktari wetu wanajitahidi, lakini wanazidiwa tu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kitengo cha *X-Ray* ambacho katika hospitali ya Mkoani hapana. Mhe. Naibu Spika, juzi nimepigiwa simu yuko mtoto wangu na watoto wengine sio wangu tu, wamekwenda hospitali ya Wete kufanyiwa *X-Ray*, suala hili tuone huruma. Kuna watu wengine wanao uwezo lakini kuna wengine hawana uwezo wa kutoka Mkoani mpaka kufika Wete, na akifika Wete siku nyengine anaambiwa hakuna matibabu kwa leo itabidi uje kesho, mtu yule inabidi siku ya pili arudi. Kwa kweli hili naona ni tatizo kubwa.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kuhusu gari la kubebea wagonjwa katika hospitali ya Mkoani, hili nalo ni tatizo. Baada ya hayo naomba nije katika kituo kidogo cha afya cha Kangani.

Mhe. Naibu Spika, kituo hiki hakiridhishi hata kidogo, ni tofauti na vituo vyengine, hakina nafasi wagonjwa wanakwenda pale nadhani wanakaa kama watu hata sijui niseme nini. Kituo cha Afya hiki ni kidogo sana, na wakati mwingine anatokea mzazi, inabidi asaidiwe pale, lakini hapo hapana pahala pa kusaidiwa. Kituo hiki ni kidogo sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hiki kituo cha Kangani apange siku aende akakitembelee, ili akiona hali yake ilivyo. Mhe. Waziri nadhani umenifahamu. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Afya. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataallah*, aliyenijaalia afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia hiyo afya yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumza neno afya, kila mtu anahitaji afya. Lakini ukiangalia hospitali zetu za Unguja na Pemba zina matatizo ya kimazingira, kwa sababu mazingira yake hayaridhishi. Mtu anapokwenda katika kituo cha afya, anataka ajue kama amefika kituo cha afya, lakini unapokwenda katika kituo cha afya mazingira yakiwa ni machafu, basi na ile afya inazidi kuffia. Kwa hivyo, Mhe. Waziri husika tunakuomba uliangalie suala la usafi sana katika sehemu ya afya.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu, niende moja kwa moja katika ukurasa wa 23 Hospitali ya Chake Chake. Mhe. Naibu Spika, hospitali hii kama ilivyochangiwa na wachangiaji wengi kuwa ni hospitali iliyokuwa katikati katika mji wa kule Pemba, na hata vijiji vingi huwa wanaitumia Hospitali ya Chake Chake, kwa sababu iko katikati na tunawapongeza sana, kwa sababu wananchi wanazipenda huduma zao ni nzuri, zinasifika sana huduma zao na wananchi wakawa wanaipenda sana. Pamoja na yote hayo, kuna changamoto nyingi sana, imeelezwa ndani ya kitabu hiki kwamba hospitali ya Chake Chake imepata vifaa vikiwemo, *ultra sound* na vifaa vyengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano kuna tatizo ambalo kama unapiga *X-Ray* katika hospitali ya Chake Chake, ni lazima *X-Ray* hiyo ikasomwe Mkoani, hili ni tatizo kubwa sana. Kwa sababu wananchi wengine wanaopiga *X-Ray* pale hawatoki mjini, wanatoka mashamba na hali zao ni ngumu za kiuwezo, lakini inawasikitisha kwamba ni lazima kwenda kusoma *X-Ray* hizo Mkoani. Mhe. Naibu Spika, mtu anaweza kwenda kupiga *X-Ray* pale Chake Chake, halafu akaambiwa nenda Mkoani na akakata tama, kutokana na uwezo wake. Siku nyengine mtu anakwenda Mkoani akifika kule anaambiwa madaktari hawapo, arudi nyumbani na huo uwezo wa kurudi nyumbani hana.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Mhe. Waziri amepata vifaa hivyo, tunaomba utakapokuja hapa ututhibitishie kama *X-Ray* itapigwa pale Chake Chake na itasomwa pale pale Chake Chake. Mhe. Naibu Spika, haitoshi katika hospitali ya Chake Chake katika wodi ya wanawake kuna matatizo hayo tuliyoyazungumza ya mazingira. Katika wodi hiyo ya wanawake choo ni kimoja pale, na wakati watu wanaumwa na matumbo basi utakuta foleni pale, hili ni tatizo. Mhe. Waziri tunaomba pafanywe marekebisho makubwa kuhusu mambo ya vyoo. Mtu ni mgonjwa leo anamsubiri mwenzake akifanya haja pale pale matatizo yanaongezeka. Tunaomba suala hili liangaliwe.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, tunapoizungumzia afya, mgonjwa anapofika pale anataka wale wahudumu wawe wanampa moyo, lakini kuna baadhi ya madaktari wanawavunja moyo wagonjwa, na hili tunataka ututhibitishie utakapokuja hapa kutueleza kwa kina, kama kutakuwa kuna nidhamu ya kuwapokea wagonjwa vizuri na kuwapa moyo. Hiyo ndio fani yao madaktari, lakini wanawavunja moyo kabisa. Maana mtu anaweza kwenda kwa daktari pale akamwambia umejitakia. Amejitakia kitu gani, na yeye amekwenda kwa ajili ya matibabu pale. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili uliangalie kwa kina.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, tumeambiwa ni hospitali pekee yenye vitanda 110. Tunaipongeza serikali na kuna wagonjwa 8,581

wametibiwa, wakiwemo wagonjwa wa kike na kiume. Lakini tuangalieni hawa wagonjwa wa akili ni binadamu kama binadamu wengine. Mtu anaweza kuzaliwa akawa ana akili timamu, lakini baadae Mwenyezi Mungu akamjaalia zikapotea, lakini tunawatazama vipi hawa wagonjwa wa akili.

Mhe. Naibu Spika, wakati mwengine hawa wanaleta matatizo, mtu anapokuwa mgonjwa wa akili anaweza kuwa mnyama, tofauti ya mnyama na binadamu ni akili. Mhe. Naibu Spika, utawakuta wagonjwa wa akili hawa wanatembea uchi wa mnyama barabarani na wakati mwengine hawapati hata msaada wowote wa kuwasitiri, hawa ni binadamu kama alivyo binadamu mwengine mwenye akili yake timamu. Mtu anaweza kutoka Vikokotoni anatembea uchi mpaka akafika mbali lakini hasitiriwi, hili ni tatizo, ni lazima tuwaangalie na tuwape *support* katika kuwatunza.

Vile vile wagonjwa wa akili hawa, sijui elimu gani inatolewa kwa wananchi ili kuelewa. *Sometimes* wanaleta matatizo makubwa sana. Naomba nitoe mfano hapa. Juzi tu katika mwezi wa tano, nikiwa nakwenda jimboni kwangu nafanya ziara, mara ziara ile ilikatika kwa mgonjwa wa akili aliyempiga baba yake shoka la bega na kumvuruga vibaya sana, mpaka kufika naye hospitali ya Chake Chake, kwa kweli tulipokewa nikiwa mimi na Mhe. Mbunge. Lakini ndio hayo tunayozungumzia mambo ya nidhamu, alipopelekwa *theatre* kulikuwa kuna ushindani mkubwa wa kumshona yule, kati ya daktari na daktari, mshone wewe, hapana lazima umshone wewe. Hili ni tatizo katika hospitali ya Chake Chake, ndio nikasema ni lazima kuwe na maadili mazuri na nidhamu nzuri katika utendaji wa kazi. Mhe. Naibu Spika, daktari anatakiwa awe na busara anapompa moyo mgonjwa peke yake ni kupona, lakini ukimpa maneno makali mgonjwa basi unamzidishia maumivu.

Mhe. Naibu Spika, mgonjwa yule alipata rufaa ya kwenda Mkoani, lakini hapo hapo Chake Chake kuna tatizo kwa wakati mwengine unaambiwa zile gharama za kwenda Mkoani uzilipie wewe, unamjua mgonjwa yule ana uwezo gani, hili ni tatizo na ukienda pale hospitali ya Chake Chake pamejipanga vizuri, utakuta gari tano au sita zimejipanga pale, lakini tatizo ni hilo la kulipia gharama.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunaomba uliangalie kwa kina hili na tukute mabadiliko makubwa sana katika hizo hospitali tutakapokwenda baada ya bajeti hii. Tujue kwamba maneno tuliyozungumza hapa, mbele ya chombo kikubwa hiki kama yanafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, nikizungumzia wagonjwa wa akili hapo Mikunguni, basi kapita mgonjwa huyo wa akili, kuna mama anapita hana habari kampiga ngumu ya mdomo na kumtoa meno. Sasa sijui tuwashajihishe vipi katika

kutoa elimu ili wafike mahali husika kwa mujibu wa matibabu. Tusiwaachie kutembea ovyo na badala yake kupata madhara makubwa. Tumesema ni bora kinga kuliko tiba, kama ni bora kinga kuliko tiba, basi hili lichukuliwe uzito mkubwa sana, Mhe. Waziri utakapokuja hapa utupe maelezo mazuri kuhusiana na hili.

Mhe. Naibu Spika, niendeleo na mchango wangu katika ongezeko la vituo vya afya kuzidi uwezo wa kuvihudumia. Hili ni kweli. Vituo vya afya vimekuwa vingi na tumekosa uwezo wa kuvihudumia. Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna vituo vyengine na mpaka leo hii vitazidi kuongezeka, kwa sababu ni masafa marefu wanakopata huduma, mtu akiwa mgonjwa anataka awahiwe, lakini kutokana na masafa wanayokwenda basi unaweza kupoteza maisha. Nitoe mfano kama Jimbo langu la Kojani pale Maziwani, hapana kituo cha afya, lakini wananchi wa Maziwani kwa nguvu zao zote na kwa kushirikiana na Mhe. Mbunge na Mhe. Mwakilishi wanajenga kituo cha afya, sasa vituo hivi vilivyokuwa mbali na wananchi, pamoja na kuwa hatuwezi kuvihudumia vyote, lakini tviangalie ni kipi tukiache na kipi tukifanyie kazi, tupo katika harakati hizo. Hawa wanapata huduma kutoka Maziwani kwenda Kiungoni. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ni usumbufu mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, nje katika programu ya kudhibiti malaria. Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya vizuri sana kuhusu hili, kwa kutoa tiba, kutoa kinga ya vyandarua na mambo mengine. Lakini katika upigaji wa dawa huu, hawa wapiga dawa wanapata usumbufu mkubwa sana ndani ya majumba. Mimi Mhe. Naibu Spika, ningependa kutoa ushauri tu, ushauri wangu ni kwamba ingekuwa vyema kupiga dawa katika mazalia, katika mito, karo na sehemu nyengine ambazo mazalia ya mbu yanatoka. Ingekuwa vizuri zaidi, pia mtu nyumbani kwake anapaswa kupiga dawa yeye mwenyewe. Unapopiga dawa hii huwa inawasha sana, kwa hivyo tutahadhari sana.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo katika kukomesha hii malaria. Mtu unaweza kwenda hospitali ukapimwa malaria ukaambiwa huna, lakini dalili za malaria zote unazo, na unaweza kwenda hospitali nyengine basi malaria ikagundulikana. Lakini katika hospitali zetu hizi za serikali kila unapokwenda unaambiwa malaria huna. Suala hili tunakuomba Mhe. Waziri uje utueleze kwa kina, ili tujue ni tatizo gani linalosumbua.

Mhe. Naibu Spika, mwisho niseme Zanzibar ni visiwa na kuna visiwa vikubwa vya Unguja na Pemba. Lakini baada ya visiwa hivyo vikubwa, kuna visiwa vyengine vidogo vidogo kama kisiwa cha Tumbatu, Uzi, Fundo, Kisiwa Panza, Makoongwe na Kisiwa cha Kojani. Hivi ni visiwa vinavyokaliwa na watu.

Mhe. Naibu Spika, watu wa visiwa tuna shida kweli kweli, hasa tunapotokezewa na matatizo ya magonjwa, tunakuwa na matatizo makubwa sana. Maana Mhe. Naibu Spika, ikitokezea ugonjwa ule hautibiki pale, ni lazima uvushwe upelekwe hospitali nyengine. Sisi kwa kule Kojani ni lazima twende Chake Chake au Wete. Lakini huo muda wa kuvuka unakuwa na matatizo. Mimi nashukuru sana katika vituo vya afya vya vijijini vilivyojengwa, basi Kojani wamepata kituo kizuri sana, lakini jambo la kusikitisha pale tulikuwa na madaktari wetu wawili wanatoa huduma vizuri tu. Tulikuwa na daktari wa maabara na daktari wa uzalishaji, lakini hawa wameondolewa ghafla. Kwa hivyo, dhiki inayowakuta wale Wakojani iko pale pale.

Hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri kwa kujali kama visiwa tuna dhiki nyingi sana, basi aliangalie hilo na aturejeshee wale madaktari. Kuna vifaa vizuri tu kama kifaa cha kutolea meno na kuna vifaa hivyo vya uzalishaji, lakini havina madaktari. Kwa hivyo, tunamuomba atuletee hawa madaktari na kama hakuwapata basi avichukue hivyo vifaa akavitumie kwengine, haifai vikakaa pale mpaka vikaoza. Lakini tunamuomba kwa dhati Mhe. Waziri atupelekee madaktari ili huduma hizo ziweze kutoka hapa, mpaka huduma nyengine zitakazoshindikana ndio wapelekwe rufaa katika hospitali nyengine.

Mhe. Naibu Spika, tunazungumzia afya, na afya ukiizungumza hata ndani ya masoko yetu, basi siyo nzuri. Afya ni pamoja na chakula, lakini twende tukaangalie katika mandhari, hata kwa Mama Ntilie huko, katika kipindi cha nyuma watu walikuwa wakitengeneza visanduku vya kuwekea vyakula, lakini siku hizi watu wanaweka ovyo ovyo tu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunaomba iangaliwe afya ya wananchi wetu, hili ndio taifa.

Mhe. Naibu Spika, tunamuomba Mhe. Waziri kama haiwezekani basi atoe ushauri, wenzetu Tanzania Bara kule wanauza samaki juu ya meza, hutengenezwa meza nzuri na wakitoka wanakwenda kwenye meza kufanyiwa matayarisho. Lakini pale Malindi, pale ni matatizo, samaki wanauzwa chini, kuna mitaro ya maji machafu inayopita pale, lakini wanawapanga tu, hiki ni chakula na ndio afya. Ukiangalia katika sehemu za mabusha huko. Mhe. Naibu Spika, angalia Darajani pale, utamuona mtu kabeba nyama mgongo uko wazi, na nyama ile inaliwa na binadamu. Mhe. Naibu Spika, tuangalie sana hiyo ndio afya. Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache nasema nakushukuru sana na ahsante sana.

Mhe. Mlinde Mbarouk Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa asubuhi hii na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili au matatu katika Wizara hii ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar, kwa kuwapatia mama zetu hawa angalau waweze kupata huduma za uzazi bila malipo. Suala hili nalipongeza sana kwa sababu hata wizara imeitikia kikamilifu agizo la Mhe. Rais

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nianze na hii *Program* ya Kudhibiti Malaria. Mhe. Waziri kwenye hotuba yake ametueleza kwamba wamefanikiwa vizuri, lakini kuna maeneo teuzi ambayo hata eneo langu la Bumbwini limetajwa.

Kwa hivyo, naomba nikiri kwamba Bumbwini matatizo ya malaria bado yapo. Lakini jambo la kusikitisha hapa, kwa kuwa inajulikana kwamba tatizo la malaria Bumbwini, sasa imekuwaje wakati wa upigaji dawa kuna nyumba zinaachwa. Kwa mfano, hata pale kijijini kwamba ambapo mimi mwenyewe ninapoishi kuna nyumba nyingi pale hazikupigwa dawa, pia vyandarua watu hawakupata. (*Makofi*)

Kwa hivyo, mimi naomba wakati wa upigaji dawa kuwe na utaratibu mzuri, ambao sijui kama wenzetu Masheha nyumba nyengine hawazitambui nikiwemo mimi mwenyewe, kwani hata nyumba yangu haikupigwa. Kwa maana hiyo, naiomba Wizara ya Afya hasa katika haya maeneo ambayo wameona kwamba malaria ni tatizo, basi watoe kipaumbele, ili kusudi tuweze kulitokomeza tatizo hili.

Nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 90, ambapo Mhe. Waziri amezungumzia kuhusu changamoto mbali mbali ambazo wizara yake inaikabili hasa ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri katika Jimbo langu la Bumbwini kuna Kituo cha Kiongwe. Kituo hichi kwa kweli kimejengwa miaka mingi na hichi kituo kiko katika hatua za mwisho na bado mambo madogo madogo tu kumaliza. Kutokana na hali hiyo, nimuombe kwa *nature* ya Kiongwe hichi kituo waweze kutumalizia na kuweza kutupatia vijana pale kwa ajili ya kutoa huduma. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mwisho napenda kumwambia Mhe. Waziri sijui kama anafahamu Mhe. Rais wakati wa kampeni zake alipokuwa katika Jimbo la Bumbwini aliahidi kutuletea *ambulance*. Kwa kweli *ambulance* hii imetokana hasa kijiji cha Kiongwe kiko mbali na maeneo mengine na kijiji ambacho mara nyingi huwa kinatokea maradhi ya mripuko.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kama suala hili halifahamu, kwamba suala hili Mhe. Rais aliliahidi, hivyo tunaomba hii gari ya *ambulance* tuweze kupatiwa, ili kuweza kutoa huduma nzuri tena ya haraka kwa wananchi wetu. (Makofi)

Vile vile nimuahidi kwamba kama tatizo hospitali yetu pale Misufini ile kubwa kwa sababu haina uzio na haiwezi kuwekwa, basi mimi naahidi kwamba uzio wa hospitali ile mimi nitajenga, lakini gari tuweze kupatiwa kwa ajili ya kusaidia wananchi wetu, ili waweze kupata matibabu ya haraka. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (Makofi)

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nitoe yangu machache nilionayo.

Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezeshia asubuhi hii kukutana hapa tukiwa wazima tukenda na shughuli zetu.

Pili niwapongeze wachangiaji wote hususan wale waliochangia jana, kwamba ni watu mahiri ambao wamechangia vizuri, kwa sababu Mhe. Naibu Spika katika kipindi hichi cha bajeti ukumbi huu unageuka kuwa ni ukumbi wa mitihani, tena ni Mtihani wa *Cambridge* ambao hauvuji. (Makofi)

Kwa kweli sisi sote humu wizara zinatufanya sisi ni watihaniwa, mpaka pale waziri husika anakwenda kusoma bajeti yake na sisi ndio tunapewa kitabu chake, ambacho kwa mimi naona ni mtihani, kwa ajili ya kufanya mtihani. Kwa hivyo, waliochangia jana ni watu wazuri na kwa imani yangu kwamba wao niwape *first grade*, kwamba kitabu wamepata pale na kumaliza Mhe. Waziri tu na wao wakaweza kuchangia tenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, naomba kama Kanuni inaruhusu basi vitabu hivi tupewe angalau siku mbili kama *tanbihi* ya katibu inavyoonesha, ingawa katibu haoneshi kwamba vifike Barazani au kwa Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hivyo, mimi naomba vitufike sisi Wajumbe kabla, ili huu ukumbi usiwe ukumbi wa mitihani, lakini uwe ni ukumbi wa kujadili bajeti ya serikali. (Makofi)

Mhe. Naibu Spika, nianze na mambo ya kinga, tunasema kwamba kinga ni bora kuliko kutibu. Kwa kweli nchi yetu tunayo magonjwa kadhaa ambayo yanakingika hasa yale ya kuambukiza. Kwa mfano, huko nyuma kabla ya wengi hawajazaliwa waliomo humu Zanzibar ilikuwa na ugonjwa sugu wa buba.

Serikali ilipigana na ugonjwa huu na hatimaye ulitoweka moja kwa moja, nadhani kama leo utazuka basi wengi hawatojua huu ni ugonjwa gani mpaka wafanye utafiti. Kwa hivyo, ugonjwa ule uliondoka kulingana na elimu ya kinga iliyokuwa ikitolewa na hatimaye ikafuatiwa na tiba na ukaweza kutoweka moja kwa moja. Kwa maana hiyo, kuinga ni kupunguza gharama ya kutibu.

Kutokana na hali hiyo, ningomba Kitengo hichi cha Kinga kiendeleo kutoa taaluma na elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na maradhi mbali mbali ambayo yanaambukiza na hadi pale ambapo ilikuwa hakuna budi ndio twende katika tiba.

Mhe. Naibu Spika, yametajwa maradhi mbali mbali hapa yakiwemo yale ya kuambukiza na mengine ambayo hayaambukizi, lakini yamekuwa ni magonjwa sugu. Nchi yetu hivi sasa imekuwa na magonjwa kadhaa ikiwemo *Pressure*, Kisukari na Kensa. Maradhi haya huko nyuma yalikuwa kidogo ni adimu mno, lakini miaka ya hivi karibuni magonjwa haya yameibuka kwa kasi mno. Kwa hivyo, naiomba wizara ifanye utafiti wa hali ya juu, ili iweze kubaini ni hasa nini chanzo cha mripuko huu wa maradhi haya ambayo nayo ni hatari kwa afya za binadamu, bila ya shaka kuibuka kwake zipo sababu. Kwa hiyo, ni vyema tukafanya utafiti, ili kuweza kubaini na kutoa elimu kwa wananchi wetu na kuweza kujiepusha na mripuko wake.

Mhe. Naibu Spika, zamani Kitengo hichi cha Kinga ilikuwa kinapita hata skuli zetu, kwa ajili ya kutoa elimu mbali mbali, kuwaelimisha wanafunzi, kuwaelekeza na hata huduma nyengine zilikuwa zinapatikana kule maskuli. Kwa mfano, madaktari wa meno walikuwa wakipita kwa ajili ya kuwaangalia wanafunzi na kama yupo ambaye jino lake linahitaji kutiwa risasi au kung'olewa, basi bila ya kwenda hospitali huduma hizi zilikuwa zinatolewa.

Hali hii ilikuwa inapunguza msongamano wa kule hospitali kwa magonjwa ambayo wanafunzi wanaweza kufanyiwa nje ya vituo vya afya. Nadhani katika vipindi hivi taratibu hizi ambazo zilikuwa zikifanyika hapo zamani, ambazo ni nzuri sasa zimeondoka.

Kwa hivyo, baada ya huduma zetu za nchi kukua jinsi ya miaka inavyokwenda mbele, ambavyo taifa ndio linakua sisi inaonesha huduma zetu zinarudi chini badala ya kupanda juu. Kwa kweli tulipoanza na serikali zilikuwa huduma zetu ni nzuri zaidi, lakini kila serikali ikikua huduma zake zinadhoofika na sijui kwa nini badala ya kuongezeka ikawa zinadhoofika.

Mhe. Naibu Spika, mwanzo Abdalla Mzee Hospitali hata kule nilikokulia kijijini kama atatokea mzazi usiku *just* upige simu tu na *ambulance* baada ya

dakika chache itakufika. Lakini leo hiyo ni ndoto na gari za Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge ndio zimechukua nafasi ya kuwa ndio *ambulance* katika sehemu hizo na ile ya serikali kama ipo itabidi lazima uichangie mafuta.

Kwa hivyo, ile dhana ya matibabu kuwa ni bure kidogo kidogo inaanza kuyoyoma, kwa sababu ukifika kwenye tiba na kuandikiwa dawa zaidi ya mbili basi japo moja lazima ukanunue. Kwa maana hiyo, ile dhana ya kuwa matibabu bure inaanza kupotea na lile lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kutoa huduma hii bure polepole inaondoka.

Mhe. Naibu Spika, naiomba Wizara ya Afya ifanye juhudi zake kwa ajili ya kuendeleza dhana hii na kutilia maanani kuwa watu wa visiwa hivi bado ni masikini, ndio maana Rais wa mwanzo alichukua hatua hizo kwa ajili ya kuwapunguzia mzigo wananchi wa Zanzibar katika huduma hizi za afya.

Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani ni moja katika hospitali tatu kubwa za Pemba, moja iko Wete, nyengine iko Chake-Chake na yengine iko Mkoani. Hospitali hizi kila moja ina umuhimu wake, mimi kwa sababu mtu wa Wilaya ya Mkoani nashauri sana kwamba ile tuifanye iwe Hospitali ya Mkoani ndio ya Rufaa kwa Pemba, sio kama iwe ya rufaa tu, lakini zile huduma zake. Kwa mfano, unaweza kumkuta mtu anatoka Msuka amekuja pale Hospitali ya Abdalla Mzee amepita Chake-Chake au amekwenda Wete na kuambiwa aende Mkoani, sasa huko Mkoani anapokuja kuna matatizo yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa tabia zetu sisi Wapemba kutoka mtu Msuka na kupelekwa Wete na kufika Wete akaambiwa aende Mkoani na Mkoani akaambiwa aende Hospitali ya Mnazi Moja, basi wale wauguzaji wanakata tamaa kwa huyu aaa! Wete ameshinda, Mkoani ameshinda na leo tunaambiwa aende Unguja kwa huyu aaa!

Sasa Mhe. Naibu Spika, sijui tatizo letu nini? Hatuna wataalamu au zana ama ni kitu gani? Kwa sababu kuna mambo ambayo yanayokuwa *transferred* pengine kama angekuwepo mtaalamu na zana za kufanyia kazi, basi *transfer* kama zile ingelikuwa hazitolewi hata kwenye Vituo Vidogo vya Afya Vijijini.

Kwa mfano, wanampa mtu kwenda Abdalla Mzee Hospitali, lakini kama angelikuwa zana fulani anayo, basi huduma ile angeliweza kuitoa pale pale kijini, kutokana na ukosefu za zana za kufanyia kazi *Staff Nurse* wa Kijijini anatoa *refer just* hana kile chombo cha kufanyia kazi.

Kwa hivyo, ili twende sambamba na dunia ilivyo vituo vyetu pamoja na hospitali zetu tuziboreshe, ili *transfer* ambazo si za lazima zisitokee kutoka sehemu moja kwende sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, katika Wilaya ya Mkoani Jimbo kubwa ni la Mtambile, ambalo hivi sasa lina vituo vitatu tu vya afya. Vituo hivyo, kimoja kiko Kengeja, chengine Mtambile na Kangani. Vile vile Jimbo dogo kuliko yote katika Wilaya ya Mkoani ni Jimbo la Mkanyageni, ambalo hivi sasa lina utitiri na uyoga wa vituo vya afya ambavyo vimeshakuwepo na vyengine vinaendelea kujengwa.

Katika semina tuliropewa hivi karibuni wataalamu wa Wizara ya Afya walituoonesha ule msongomano wa vituo vya afya, ambavyo walituoonesha hasa kwamba sasa katika Zanzibar hakuna haja tena ya kuongeza kituo kipya cha afya. Lakini jimbo hili limeshafanya *program* ya kuweka kituo Tasini na sehemu nyengine mbali mbali.

Je, hivi imekuwa kuna nini hasa ndani ya Mkanyageni? Ni kweli kweli vituo havitoshi au kuna kitu ambacho kimejificha na wenyewe hawataki kusema?

Mhe. Naibu Spika, ningeiomba wizara hii ifanye utafiti kwa nini Mkanyageni, ambapo vituo vilivyopo vinatosha kabisa kulingana na masafa ambayo Wizara ya Afya imejipangia kwamba mtu asitembee zaidi ya masafa haya. Kwa kweli hakuna mtu anayetembea zaidi ya masafa yale yaliyopangwa, lakini bado wakawa *wanaroromoa* vituo vya afya kadhaa na pengine wizara sina hakika kama wamevikubali au laa. (*Makofi*)

Kwa hivyo, naomba wafanye utafiti kuna nini ndani ya Mkanyageni hata iwe hivi wao peke yao, kwa sababu na mimi nimesema kwamba jimbo langu ndilo kubwa. Kwa mfano, kuna eneo ambalo linaitwa Minazini kama inaruhusiwa basi na sisi tufanye harambee, ili tuweze kujenga na tukesha kujenga wizara itusaidie kupata wataalamu pamoja na watu wa kufanya kazi pale.

Mhe. Naibu Spika, hofu yangu ni kwamba tunaweka vituo hivi kama uyoga, lakini hatimaye pengine tunashindwa kuvihudumia. Kwa mfano, hivi sasa kuna baadhi ya vituo vya Pemba ambavyo mfanyakazi wake alipostaafu, basi *Staff Nurse* mwengine wa kupelekwa pale anashindikana, lakini leo bado tunaongeza vyengine kwa kutambua hivi vilipo havina wahuduma wa kutosha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika tano.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye masuala ya kutibu kwa ujumla. Kwa mfano, baadhi ya wakati anakwenda mwanamke ameandikiwa sindano, lakini anayemuhudumia ni mwanamme, ndipo pale anapomwambia jikunjue kidogo, teremsha kidogo, anamchoma na halafu anamzuia ili asitoke damu. Kwa kweli ni kinyume kidogo na maadili yetu ya hapa. (*Makofi*)

Kwa hivyo, naiomba wizara hii iweke wahudumu wa kutosha hawa wanaopiga sindano na wala wasiwe *Orderlies*, kwa sababu takriban vituo vyetu vingi vya shamba kule Pemba *Orderlies* ndio wanaotibu kuliko hao *Staff Nurses*, kwani wao huwa ni wachache na wakiondoka, basi *Orderlies* hukalia viti.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba wizara hii ijitahidi kadri itakavyowezekana mpaka iwe hakuna budi kabisa ndio jinsia mbili hizi ziingiliane katika mambo ambayo kidogo ni ya faragha na yale ya dhahiri hakuna tatizo, lakini yale ya faragha mpaka iwe hakuna budi hata kidogo, vyenginevyo kuna watu wanaweza kukataa wake zao kuchomwa sindano.

Mhe. Naibu Spika, katika Hospitali yetu kubwa ya Mkoani, kwa muda mrefu imewashinda *X-Ray* haipo na wala haifanyikazi. Kwa mfano, hivi karibu katika jimbo langu kuna mtu alikwenda kuchuma karafuu na ilikuwa kuna kitawi kimoja tu, kulingana na karafuu ilivyo aliamua akifuata na bahati mbaya alianguka.

Sasa baada ya kuanguka nilitakiwa nitoe *ambulance* na nilitoa, yaani gari ninayotumia mimi ndio *ambulance* na kupelekwa Mkoani na kufika huko anambiwa mashine ya *X-Ray* haifanyikazi na apelekwe Chake-Chake. Kwa hivyo, niliambiwa Mheshimiwa sasa itabidi tumpeleke Chake-Chake mgonjwa, basi nilijikuna kichwa duu! Kwa mafuta ya kwenda Mkoani ilikuwa nimeyakopa, sasa safari imeshakuwa, lakini nikakubali.

Mhe. Naibu Spika, ninachokikusudia kusema kwamba mashine hii Mkoani haipo na ndio moja miongoni mwa hospitali kubwa za Pemba. Kwa kweli chombo kama hiki kukosekana kwa muda mkubwa ni hatari na haifanani. Kutokana na hali hiyo, naiomba wizara ivae njuga kuhakikisha chombo hichi kipo tena cha kisasa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa nafasi tunampa Mhe. Mohammed Mbwana Hamad na baadaye afuatie Mhe. Marina Joel Thomas na ajiandae Mhe. Subeit Khamis Faki.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia asubuhi hii kuendelea na majukumu yetu ya kitaifa.

Pili nachukua nafasi ya kukupongeza kwa kunipa nafasi ya kuweza na mimi kuchangia mawili matatu juu ya Hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya kuhusiana na makadirio na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, niendeleo kutoa shukurani zangu za dhiti kwa Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa makusudi kuwapunguzia ule udhia na uzito mkubwa wazazi kwa kutoa shilingi 40,000/=, kwamba iwe ni *free* kwao. Kwa kweli hili ni jambo zuri tena ni jambo la kupigiwa mfano kwa kiasi fulani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, akinamama tunajua uzito wao na tunajua uzito wa kujifungua pamoja na huduma mbali mbali ambazo hutolewa katika masuala haya ya kujifungua na mengineyo. Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Rais kwa kuliondoa tatizo zima hili la kutozwa chochote kwa wazazi.

Nikiendelea hapo kwa wazazi kuna tatizo ambalo linalalamikiwa sana. Kwa hivyo, kuhusiana na tatizo hili namuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina, ili aweze kujipanga vyema pamoja na watendaji wake, kwa lengo la kulitatua tatizo hili.

Kwa kweli tatizo la wakunga wa kiume kuwapokea wanawake, tatizo hili linawadhalilisha akina mama. Kwa mfano, mama mzazi anapofika hospitali ikabidi lazima apokewe na mwanamme, kwa kweli hufika wakati hata ule uchungu kwa baadhi ya wengine huwa unarudi.

Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba tatizo hili litatuke kwa asilimia kubwa sana, pamoja na upungufu wa watendaji wetu. Lakini tuangalie na mazingira yetu yalivyo, kwa sababu wakati wa kujifungua ni wakati mgumu, ni stara kubwa, ni siri kubwa pamoja na waganga hawa kwamba wamekula kiapo kutunza siri na mengineyo, lakini panakuwa si pema vyema kwa wanaume kukinga mikono kuwapokea wanawake wanaojifungua, naomba hili liangaliwe vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 4 wa kitabu unaelezea kuhusu afya na usalama wa wafanyakazi. Kwa kweli wafanyakazi ndio rasilimali kuu ya taifa katika shughuli mbali mbali zinazoendelea, kama vile kuendeleza uchumi, mafanikio pamoja na mambo yote katika nchi, yaani afya ya wafanyakazi ni muhimu sana. (*Makofi*)

Sasa inasikitisha kuona kwamba mfanyakazi kabla ya kuajiriwa anatakiwa aende akafanye *checking* ya afya yake. Lakini baada ya kupata matokeo kwamba afya yake ni nzuri na anatakiwa aendelee na kazi ile aliyostahiki nayo inamalizia siku hiyo. Mhe. Naibu Spika, nafikiri mfanyakazi anaweza kutimiza miaka 30 au mpaka kustaafu kwake baada ya siku ile ya mwanzo, basi anamaliza muda wake wa kazi anashindwa kupata *checking* ya aina nyengine.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, awe na utaratibu maalum kila baada ya kipindi fulani basi wafanyakazi wafanyiwe *checking* juu ya afya zao na wakihitaji kupewa tiba, wapewe tiba ili afya zao ziendelee na waweze kufanyakazi vizuri. Kwa kweli suala hili ni muhimu, kwani bila ya afya huwezi kufanyakazi vizuri. (*Makofi*)

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awapange wafanyakazi wake vizuri, ili kila baada ya kipindi fulani wafanyakazi wafanyiwe *checking* ya afya zao na wapatiwe tiba, ili waendelee kufanyakazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kuna utaratibu ambao ulikuwa ukifanywa miaka mingi iliyopita, utaratibu wa Mabwana Afya kupita maskuli kwa ajili ya kuwapima wanafunzi na kuwaendeleza kitiba, suala hili limepungua kwa asilimia kubwa sana. Hivi sasa madaktari labda wa Kichocho tu ndio kwa asilimia kubwa kila baada ya kipindi fulani wanapita na kuwapa wanafunzi matibabu yale ya kichocho.

Kwa hivyo, tunaomba kwamba matibabu pamoja na *checking* nyengine zipitie skuli, ili kupunguza msongomano ambao ungekuwepo mahospitali kwa kufuata utaratibu huu wa kuwachunguza na kuwatibu wanafunzi maskulini.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Wakunga wa Kienyeji hasa vijijini. Mhe. Naibu Spika, tunakuwa na wakunga wa kienyeji vijijini kwa ajili ya kuwazalisha hawa akinamama. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri, je wakunga hawa ni taaluma gani wanayopatiwa? Vile vile je, kuna angalau kijisabuni ambacho wanasaidiwa?

Mhe. Naibu Spika, nazungumza hili kwa sababu hawa wanasumbuka sana, mara nyingi tuna wahodishia milangoni kwao usiku kwa ajili ya kuwasaidia wazazi, nadhani wanahitaji kupewa chochote katika hili. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba labda utupe maelekezo juu ya wakunga wa kienyeji angalau mumewapa taaluma kiasi gani na chochote ambacho kingewasaidia angalau kwa sabuni.

Vile vile nizungumzie tena kuhusu suala zima la upungufu wa madaktari katika nchi au Serikali yetu ya Zanzibar. Kwa kweli tunavyo vituo vingi vya afya Unguja na Pemba, mjini na vijijini, kilio kikubwa tulichonacho ni ukosefu wa wafanyakazi madaktari katika vituo vyetu vya afya na hili ni tatizo. Lakini nadhani ni vyema tukajipanga vizuri, yaani tubadilike na tubadilishe mfumo tulionao na tuingie kwenye mfumo mpya wa kuweza kuzalisha madaktari katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika hili naomba kutoa ushauri kwa kuwa tunayo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wizara ambayo kila mwaka inafanyisha wanafunzi mitihani ya darasa la saba, la kumi na la kumi na mbili tuisubiri wanafunzi waliomaliza darasa la kumi na mbili (12), tusidowee wanafunzi waliomaliza darasa la 12 tukawataka wawe na pasi za sayansi tu. Bali Wizara ya Afya hivi sasa labda ibadilishe mfumo, iwatege wanafunzi wanaopasi michipuo wale wanafunzi bingwa wa masomo ya sayansi pale waingizwe katika chuo cha Afya waanze kupewa taaluma ya udaktari kuanzia pale. Nafikiri hili linaweza likapunguza upungufu mkubwa tulionao wa madaktari katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, wanafunzi wa Darasa la tisa wenye vipawa vya juu kabisa kutoka mazingira tofauti ya Zanzibar kama tutawakusanya katika Chuo cha Afya, na wapewe utaalumu wa udaktari kuanzia *form one* hata wakimaliza miaka yao minne hawa watasaidia kwa kiasi kikubwa sana kupunguza suala zima la upungufu wa madaktari katika nchi yetu ya Unguja.

Mhe. Spika, nikiendelea kidogo niende kwa akina mama ambao wanakuwa na matatizo ya matumbo. Wanawake wengi hivi sasa wanakuwa na usumbufu wa maradhi ya tumbo, na wengi hufanyiwa upasuaji kwa hospitali mbali mbali. Wanawake hawa hufikia hospitali yetu Kuu ya Mnazi Mmoja. Wanapofika pale wanachunguzwa, wakionekana wana matatizo labda ya kufanyiwa *operation* wanapewa uhamisho pale na kupelekwa hospitali moja Saateni ile hospitali ya kiraia.

Je, labda nimuulize Mhe. Waziri, kuna tatizo gani la wagonjwa hawa kutowahudumia pale Mnazi Mmoja na badala yake kupelekwa hospitali ile ya kiraia wakati pale kuna malipo yalikuwa makubwa kidogo. Je, kuna tatizo gani la msingi ambalo linawafanya madaktari wa Mnazi Mmoja kuwapeleka wagonjwa hawa hospitali ya mtu binafsi, badala ya kuwahudumia wao na kuwapunguzia ile gharama kubwa ambayo wanaipata pale Saateni.

Mhe. Spika, baada ya hilo niende kidogo katika kituo changu cha Afya kilichopo jimboni kwangu katika Shehia ya Chambani. Kuna kituo cha Afya kimejengwa muda mrefu sana. Kituo ambacho kuna bao pale limewekwa la

ufunguzi wa kituo kile karibu miaka minne au mitano iliyopita nyuma, lakini kituo kile mpaka leo hakijafunguliwa. Labda nimuulize Mhe. Waziri lini kituo kile cha Afya cha Shehia ya Chambani kitafunguliwa. Zaidi ya hayo nashukuru na mimi kutoa mchango wangu mchache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii, pia nampongeza Mhe. Waziri wa Afya pamoja na wataalamu wake kwa kuandaa hotuba hii nzuri, hongereni sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitachangia katika ukurasa wa 19 naomba uniruhusu ninukuu:

“Kuanzia Julai 2011 hadi Machi 2012 sampuli nane za maji kutoka kwenye visima, maji ya majumbani na kwenye mahodhi zilichukuliwa na kupelekwa maabara kwa uchunguzi zaidi. Matokeo yalionesha kwamba sampuli tatu kati ya hizo zilionekana kuwa na vimelea vya maradhi”

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli matokeo haya sio mazuri, ukipiga kiasilimia tu unapata karibu asilimia 40, hii ni hali mbaya sana. Matokeo hayo ni kwa ajili ya sampuli nane tu. Ukizingatia wananchi wengi katika maeneo yetu wanahifadhi maji katika mahodhi, takriban wananchi wengi, wengine wana mahodhi mawili, matatu. Hii inatokana na uhaba wa maji hatuwezi kulaumu. Lakini sasa mtu anaweza kutumia maji miezi mitatu, miezi sita, hajui katika maji yale yana usalama kiasi gani.

Mhe. Naibu Spika, hapa ningemshauri Mhe. Waziri aendelee kufanya uchunguzi katika maeneo mengine, naamini uchunguzi unahitaji gharama kubwa lakini aendelee kidogo kidogo, ili kuweza kuidhibiti hali hii. Hata hivyo niitake Wizara ya Afya na Waziri wa Afya waendelee kutoa elimu ya afya. Elimu inaendelea kutolewa na wanafanya kazi nzuri tu, lakini wazidi kuendelea ili tatizo hili liweze kupungua.

Pia namuomba Mhe. Waziri ambae anayeshughulikia na maji waendelee kufanya utaratibu wao kutia maji zile *chlorine* katika vianzio vya maji. Zamani sisi tulikuwa tunakunywa maji vile ukiyafungua tu kwenye bomba basi unaipata ile harufu, na unajua kwamba maji haya yametiwa dawa. Naomba wizara inayoshughulikia na maji iendelee na utaratibu huo kwenye vianzio vya maji waweke hiyo *chlorine*. Pia waelimishe jamii kuhusu kutumia *water guard* hizi ambazo zitaweza kupunguza vimelea vya maradhi.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, mchango wangu si mkubwa naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa na mimi fursa ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa sana kwa leo. Kwanza naomba nichangie katika kitengo cha lishe. Mhe. Waziri ametueleza kuhusu lishe na watoto wambao wana utapia mlo. Siku za nyuma ninavyokumbuka kitengo hiki kilikuwa kinafanya kazi nzuri zaidi kuliko sasa hivi. Sijui kwa sababu tulikuwa na wafadhili au tulikuwa tuna wahisani. Lakini ilikuwa kitengo hichi kinafanya kazi, na watoto walikuwa wanapewa chakula cha lishe. Lakini kwa muda mkubwa sasa hivi naona kitengo hichi sijui kwa kuwa hatuna tena wafadhili au vipi nguvu yake imerudi.

Wakati huo huo kuna watoto kama tunavyozungumza kwamba wanakosa lishe na wanakuwa na utapia mlo. Ningeomba Mhe. Waziri aone kama kazi ile nzuri iliyokuwa ikifanywa, ya kupita na kuwatafuta wale watoto waliokuwa kidogo hali zao sio nzuri wakawa wanasaidiwa chakula cha lishe, ni vizuri sana kitengo hichi kikaendelea kufanya kazi yake, kitapata wale wahisani wa kusaidia. Serikali ifanye jitihada kuendeleza kwa sababu ni kazi nzuri iliyokuwa ikifanywa. Hiyo inapunguza ile kasi ya kuwa na watoto wengi wenye utapia mlo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ninalotaka nilizungumze nataka nisewe mpungufu wa fadhila, nizungumzie kuhusu hospitali ya Micheweni. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuona kama azma ya serikali ya kuondosha hospitali zile za Micheweni, Kivunge, Vitongoji na nyenginezo kuzifanya kama ni hospitali za Wilaya. Nimpongeze sasa hivi Micheweni tunajengewa kituo cha Maabara. Azma hiyo ya kuibadilisha hospitali ya Micheweni kuwa ya Wilaya ni dalili moja ya kuwa kweli Waziri amekusudia kuiboresha hospitali ya Micheweni kuwa Hospitali ya Wilaya.

Pamoja na azma hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kama kuboresha kwake kutakuwa hakutoshelezi, kama itakuwa hakutupelekea madaktari ambao watakuwa wanafanya kazi kwa wakati wote. Pia hapa nimsifu kasema kama katupelekea Micheweni Daktari mmoja wa kigeni ambae anashirikiana na wale madaktari wazalendo waliokuwepo pale, ili kuboresha huduma ya matibabu katika hospitali yetu ya Micheweni. Lakini Daktari mmoja hatoshi, kwa sababu kabla ya azma hiyo ya serikali kuiboresha kuwa kama Hospitali ya Wilaya, basi kwa mandhari ilivyo Micheweni basi imeshakuwa Hospitali ya Wilaya kabda ya Serikali kuazimia kuiboresha kuwa Hospitali ya Wilaya.

Kwa nini niseme hivyo? Kwa sababu katika eneo lote la Wilaya ya Micheweni kulikuwa hakuna hospitali, kuna vituo vya Afya tu vya kuwasaidia watu. Lakini Micheweni kabla ya kuja azma hii basi ilishajiweka

wenyewe kama ni Hospitali ya Wilaya. Wilaya nzima ya Micheweni na Wilaya ya Wete baadhi ya maeneo jirani wote wanatumia Hospitali ya Micheweni. Kwa hii azma ya serikali ya kuja kuboresha, basi ni bora zaidi tu na itakuwa zaidi. Namuomba Mhe. Waziri aone kama kuna umuhimu kwa sababu ile hospitali inabeba watu wengi watuboreshee na kutuongozea madaktari, ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Inafika saa 3 saa 4 watu wanahitaji daktari watibiwe bado hawajaanza kazi kwa sababu gani. Daktari ni lazima akiamka asubuhi kwanza apitie wagonjwa waliolazwa, awaone halafu baadae ndio aje afanye kazi zake. Mtu hawezi kupewa dawa kama kwanza hajaonana na daktari. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aone kama bado Micheweni tuna matatizo ya madaktari, aone jitihada ya kuwa kituo chetu hiki ni muhimu sana, kwa hivyo afanye msaada wa kutupelekea daktari zaidi.

Suala jengine ninalotaka nimuombe Mhe. Waziri kila bajeti inayokuja nalizungumza na leo tena nalizungumza. Nimemwambia Mhe. Waziri kwamba Micheweni wodi za kulazwa wagonjwa ni ndogo sana, tunahitaji kuongezewa wodi za kulazwa wagonjwa. Kwa sababu kuna kipindi kimoja kulitokezea maradhi ya mripuko, pale Micheweni ikabidi mpaka skuli zote ziwe ni sehemu ya kulaza wagonjwa. Hata vile vyumba vya madaktari ilikuwa ni vyumba vya kulaziwa wagonjwa. Namuomba na hili Mhe. Waziri alione. Ingawaje nilipiga kelele sana kwa ajili ya chumba cha wazazi lakini sasa hivi Alhamdulillah, namshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na Wizara yetu kuona kama, hata kama ni kutafuta wafadhili lakini sasa hivi wazazi wanastarehe Micheweni.

Hili namuomba Mhe. Waziri aone kama kuna haja ya kuiboresha zaidi ili zile wodi za kulaza wagonjwa ziongezeke. Ukizingatia wodi ya kulaza watu wazima na watoto zipo pamoja. Kuna haja ya kuongezewa, aidha watoto wawe na wodi yao iliyotenganishwa na wazee, kwa sababu hii ipo pamoja, wazee, akina mama, akina baba ndio inayotengana kidogo. Namuomba Mhe. Waziri alione hili na alizingatie alipe kipaumbele.

Suala jengine ninalotaka nilizungumze ni suala la tiba asili. Tulipitisha Sheria ya Bodi ya Vipodozi na Chakula, namuomba nizungumze kuhusu suala hili. Azma hii ya kuwa na madaktari au watabibu asili ni nzuri sana. Katika kitabu hichi cha bajeti ametwambia kwamba watu wanaofika 19 tayari wameshapewa leseni kwa ajili ya kufanya hizi tiba asili. Wakipewa leseni ni kwamba tayari wamesharuhusiwa kufanya kazi yao.

Nimuulize Mhe. Waziri je, katika hao watu waliopata leseni ambao tayari wamesharuhusiwa kufanya kazi yao hii ya tiba asili. Je, wizara yake tayari

imeshakagua hizi dawa zake na ikazifanyia utafiti ikaona kwamba hizi dawa hazina matatizo yoyote kwa binaadamu. Je, baada ya kwisha kuzikagua, hivyo namuomba Mhe. Waziri pia atusaidie kutueleza kama baada ya kwisha kukagua je, hizi dawa wameshawekewa vipimo kwa sababu dawa za Hospitali huwezi kula dawa kama hujajua kipimo cha mtu. Kama huyu kutokana na uzito wake anahitaji kula dawa fulani ndio kiwango chake ambacho ndio zitakuwa hazimdhuru kwenye mwili wake. Ikiwa atazidisha kipimo kile basi anaweza akapata madhara.

Je, na hawa watu waliopewa leseni ya kufanya dawa asili tayari wana kipimo maalum juu ya hizi dawa au mtu avukutizwa tu kama ni chupa mbili, chupa tatu, vikimpatia madhara haya tu, au kuna kipimo maalum. Namuomba Mhe. Waziri atusaidie kutueleweshwa zaidi au mtu kama anapewa kikombe kama kutoka babu wa Loliondo pia tujue.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze kuhusu hili hili ni kuhusu vyakula vyetu ambavyo vimo katika maduka yetu. Mara nyingi hata katika kitabu cha bajeti wamezungumza kama kuna mchele uliorudishwa kutokana na kuonekana una madhara kwa wananchi. Lakini hata hivyo tunasikia mara kwa mara kwa wenzetu pamoja na hapa, kama kuna duka limekamatwa linauza vipodozi vilivyokuwa vinadhuru maisha ya watu au siku nyengine vina madhara. Siku nyengine tunasikia hata maziwa ya watoto karibuni nimeona Tanzania Bara kule Dar-es-Salaam yalikatwa maziwa ambayo kuwa ni feki ya watoto.

Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri, kutokana na hiki kitengo cha Bodi ya Chakula je, wana mpango gani wa kuwa wanapitia mara kwa mara kuangalia hivi vitu vya madukani. Mara nyingi tunauziwa vitu ambavyo vimeshakwisha muda wake. Unaweza ukenda dukani unanunua dawa ya mswaki basi ukija kuitumia ukaitupa kwa hali ilivyo. Kitengo hichi je, kinapita mara kwa mara kuangalia hivi vyakula ili wananchi wetu wasidhurike. Kama mpango huo haupo namuomba Mhe. Waziri aangalie kuboresha zaidi kitengo hiki, na kisikae muda mkubwa ikawa hakijapita madukani kuangalia. Wauza maduka wetu wanatabia saa nyengine wanakuja na vitu vimeshakwisha muda wake, tayari tunauziwa sie tunakula. Na hili namuomba Mhe. Waziri alipe uzito wa hali ya juu.

Suala jengine ninalotaka nilizungumze ni suala la hawa madaktari wetu au watendaji wetu kazi. Naomba na hili ili uzungumze na watendaji wetu. Wewe Waziri ni mmoja lakini wewe huwezi kupita hospitali zetu zote zilizokuwepo Zanzibar. Kwa hivyo na hawa wawajibike ipasavyo, mtu akiwa kapangiwa kuanza kazi saa 3:00 basi aanze kazi saa 3:00, ikiwa kapangiwa aanze kazi saa 2:00 aanze kazi muda huo aliopangiwa. Tunapata malalamiko kwa

wananchi kutokana na wakati. Watu wanakwenda hospitali wanataka kutibiwa wanakaa muda mkubwa, bado madaktari hawajaanza kazi, hilo nalo lifanywe muhimu.

Kila mtu aliyekuwa na wajibu wake tuache jamani, si kila siku Wazanzibari tusiambiwe kama sie kazi yetu ni kula urojo. Tuache kazi za uvivu, tukifanya kazi tuwajibike kikweli kweli. Ili kuondoa matatizo ya wananchi. Nakuomba na hili uwe na kitengo chako ambacho kitakuwa kina mambo marefu kuangalia nani hawajibiki. Kama hawajibiki basi wewe unayo nafasi ya kumuwajibisha. Lakini wewe kama Waziri mmoja hutoshi kuwa kila hospitali iliyokuwepo katika nchi yetu upite wewe. Wafanyakazi na wao wawe ni imara, wao wenyewe na kila mmoja ajue wajibu wake na ajali kazi yake, aipende ile kazi yake anayopewa. Tukifanya kazi vizuri tunapata sifa nzuri na ndio wajibu wetu unakuwa mkubwa zaidi na ndio maslahi ya nchi yetu yanaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, ni suala la hizi gari zetu za *Ambulance*, kuna kipindi tulikuja tukazungumza hapa kwamba hizi gari kwa nini hazipangiwi mafuta yakuja kuchukulia wagonjwa. Mara nyingi mtu akenda na mgonjwa anaambiwa gari haina mafuta. Kwa nini humu mnatupitishia vifungu vinavyohusu mafuta. Humu kuna mafuta ya dizeli, kuna mafuta ya petroli kwa ajili ya gari ya kuchukulia wagonjwa na mambo mengine. Lakini leo mtu atakwenda hospitali na mgonjwa anaambiwa gari haina mafuta, aidha uchangie mafuta au si hivyo basi gari haiwezi kwenda, kwa nini iwe hivi na tulikuja kuzungumza hapa Mhe. Waziri akatwambia mtu akiwa yupo na akiwa hajafanya hivyo tuletteni.

Basi Mheshimiwa hili lipigie kelele bado linaendelea, gari za Waheshimiwa ndizo zinazochukua wagonjwa wakipeleka. Ni wajibu wetu sisi kuchukua wagonjwa tukiwapeleka lakini na hizi gari za hospitali zinapatikiwa saa nyengine ya Mheshimiwa basi ziwe zinapatikana. Hili nalo Mheshimiwa nakuomba lisimamiwe ili Wizara yako ipate sifa zaidi.

Suala jengine nataka nizungumze kwa ufupi kabisa, ni suala la kuwaenzi madaktari. Madaktari ni watu muhimu sana katika nchi ni viungo muhimu kweli kweli. Juzi tumeona kwa wenzetu sisi Mwenyezi Mungu asitujalie madaktari wetu kugoma, lakini juzi tumeona Tanzania Bara kwa wenzetu wana mgomo, mpaka imesababisha daktari mmoja kuhujumiwa. Maana alikwenda akapigwa mpaka akaathiriwa vibaya kweli kweli kwa mgomo ule wa madaktari. Hawa ni watu muhimu kwa hiyo tuwaenzi.

Mhe. Naibu Spika, kuwaenzi kwake kwamba Mheshimiwa kuna baadhi ya madaktari wanalalamika kwamba hawapati posho za likizo wanapokwenda

likizo. Maisha wao wanakwenda likizo hajakwenda hata kipindi kimoja kupewa pesa za likizo. Wakilalamika hawa wanakutia dosari. Tunawaomba wahusika wanaohusika kila mmoja apate haki yake kwa mujibu wa utendaji wa kazi yake, wasiwe wengine wanapata pesa za likizo wengine hawapati pesa za likizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache mimi naunga mkono hoja mia juu ya mia.

Mhe. Shawana Bukheti Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uwezo na uhai wa kuweza kusimama kwenye Baraza lako hili tukufu.

Pili nikushukuru wewe mwenyewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii adhimu na muhimu, ili kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya inayohusu makadirio na matumizi ya Wizara ya Afya Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, pia niichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake nzuri, yenye uchambuzi wa kina na inaonesha kuwasaidia wananchi wetu katika mustakbali mzima wa afya zao.

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara hii na Watendaji kwa maandalizi mazuri ya hotuba ambayo imemuwezesha Mhe. Waziri kuweza kuwasilisha kwenye Baraza lako hili tukufu na wao tunawapongeza. Naamini yeye peke yake asingeweza bila ya mashirikiano yao.

Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa, madaktari, wauguzi na wafanyakazi wote kwa kazi zao nzuri, nzito, pamoja na mapungufu waliyokuwa nayo ya hapa na pale, lakini wanajitahidi kwa kadiri ya uwezo wao kuweza kutoa huduma kwa wananchi wetu. Tunawashukuru na tunawapongeza kwa hilo na tunawaomba waendeleo na moyo huo.

Pia tunawapongeza kwa dhati kabisa madaktari wetu pamoja na matatizo waliyokuwa nayo, lakini tunawapongeza kwa uzalendo wao kwa kuwa yale yanayofanywa kwa wenzetu wao hawayaigi. Tunawaomba wasiyaige waendeleo na kazi zao, serikali yao ipo, itawaona, itawashughulikia na mambo yatakuwa mazuri. Zaidi kubwa katika yote Mwenyezi Mungu atawalipa kama tunavyolipwa sisi, na sisi tulikuwa huko huko.

Mhe. Naibu Spika, pia shukurani za pekee ziweze kumuendea Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa wetu mpenzi

Dokta Ali Mohammed Shein, kwa kusimamia uzuri utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi katika sehemu zake zote, lakini hasa katika masuala ya afya. Tunamshukuru na tunampongeza na ndio maana pamoja ya juhudi yote iliyofanywa kipindi cha nyuma, vituo vya afya vimejengwa vijijini katika maeneo mbali mbali. Lakini kubwa zaidi kaona kwa kuwa Wizara ya Afya safari hii aivalie njuga kweli kweli na kwa kipindi hichi kwa juhudi zake Wizara ya Afya imevuta hatua zaidi, tunampongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi na shukurani hizo sasa nianze mchango wangu kwa kuchangia Wizara ya Afya kwa kuanzia Mnazi Mmoja Hospitali. Wengi wamesema na wengi wamezungumza lakini naamini kwamba Hospitali ya Manazi Mmoja sote tunasema ndio kioo cha nchi yetu na ndio kioo cha Wizara ya Afya. Zote hospitali tunazo lakini mwisho tunaishia Mnazi Mmoja Hospitali. Mimi napongeza sana wale waliosema kwa kuwa sasa hivi tuitizame kwa jicho la huruma Wizara hii na hasa Mnazi Mmoja Hospitali, ili lile lengo na azma iliyokusudiwa ya kuwa Hospitali hii iweze kuwa Hospitali ya Rufaa iweze kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini lengo na azma waliyokuwa nayo bado wanayo na naamini wana hamu leo kwa kesho hili jambo likamilike. Kutokana na hali nzima ya mazingira ya fedha tunazozipata inashindikana. Ningeiomba serikali kwa makusudi kabisa, juhudi wamefanya sana wizara. Vitengo vingi pale vilikuwa vina uhafifu wa huduma sasa hivi zinapatikana. Ukiangalia katika EMT pale ilikuwa mpaka mgonjwa wa kufanyiwa *tinseling* na mambo mengine lazima upelekwe sasa hivi EMT wanafanyiwa huduma zote, kitengo cha macho nao halikadhalika wanafanyiwa huduma zao pale. Kwa hivyo hii safari ni ndefu kidogo, lakini tungeomba kwa juhudi ya serikali tusiiwachie Wizara peke yake.

Tukitizama Wizara Mhe. Naibu Spika, fedha wanazozipata ni chache sana, kwa hivyo ile *speed* yao ya kutaka kwenda hatua kubwa zaidi usoni bado inawarudisha nyuma. Ningeiomba kwa kuwa serikali, Wizara ya Fedha, iwasaidie sana Wizara ya Afya ili lengo tulilokusudia la Mnazi Mmoja Hospitali iwe ni Hospitali ya Rufaa iweze kufanikiwa. Mimi ningeliomba mambo mengine pamoja na fedha lakini pia ningeliomba pale pale Mnazi Mmoja Hospitali pamoja na mapungufu tuliyokuwa nayo ya wafanyakazi lakini bado kuna haja ya kujipanga zaidi. Tujipange kwa wale wale *staff* wetu waliyokuwepo wachache lakini tuwajibike vizuri sana. Pamoja na Hospitali ya Manzi Mmoja kuwa ni kioo, lakini kioo zaidi Mhe. Naibu Spika, ni *OPD*.

Mhe. Naibu Spika, *OPD* hali kidogo sio nzuri mimi ningeliwaomba wenzangu wapaangalie sana, mambo mengine yapo ndani ya mikono yetu kama nilivyosema tunao *staff* wetu ambao wanahusika na mambo ya usafi,

basi kidogo pale *OPD* wajiandae vizuri. Kuna haja ya utaratibu baadae hata ule ukaaji wa pale *OPD* uje ubadilishwe, lile eneo zamani walikua watu wanakaa kupanga mistari kwenda kuchukua vyeti mimi nadhani kule kungefanywa utaratibu maalum pakabadilishwa badilishwa basi ma-*bench* yakawekwa kule au viti maalum vikawekwa kule hapa penye mlango wa kwendea kwa daktari angalau kidogo pakawa wazi.

Mhe. Naibu Spika, unaweza kukuta watu pale msongamano wanavyosukumana kuingia chumbani kwa daktari kama watu wanasukumana kuingia kwenye daladala, haipendezi Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, utaratibu uandaliwe ili mgonjwa mmoja mmoja analetwa kwenye sehemu ya chumba cha daktari.

Kubwa zaidi katika *OPD* kuna Mjumbe mmoja jana alizungumza na mimi natilia mkazo. Tuhakikishe tunapata *emergency room*, tunawachanganya sana madaktari wetu wa *OPD* anakuja mgonjwa wa kawaida hapo, lakini hapo hapo tayari anakuja huyu bahati mbaya amepata tumbo la kuendesha, huyu anakuja majeruhi, sasa anakuwa anachanganyikiwa na yule aliyetangulia mle ndani hawezi kutolewa na wale wote wanajazana mle. Kwa hivyo, mimi nadhani kunge andaliwa ule utaratibu hawa wanaokuja hali yao kidogo ni *serious* basi wapelekwe huko *emergency room* washughulikiwe ili wawe wana malizao kule kama wa kulazwa na nini waende na huku kuwe na utaratibu wa kushughulikia wagonjwa wa kawaida.

Mhe. Naibu Spika, mchango mimi kwa hapo ulikuwa ni huo sasa niendeleo ukurasa wa 30 katika mchango wa fedha wa kinamama wanaotaka kujifungua. Mimi nilikwihalizungumza kwenye bajeti ya mwanzo tulipoanza lakini hakuna nyongeza mbaya ambayo ni nzuri kumpongeza tena Rais wetu kwa hili na hili kwa kinamama wote hasa wa jimbo langu wamelifurahia. Kwa sababu na wao walikuwa wanapata mitihani mingi na hapa nadhani Mungu akijali mwaka 2015 mimi naona hana tatizo kwa hili Rais wetu Dr. Ali Mohammed Shein na Mwenyezi Mungu amzidishie.

Mhe. Waziri alisema hapa katika ukurasa wa 31 changamoto kwa watendaji. Unajua Mhe. Naibu Spika, mtu anaweza kuona ah, mwanya huu sasa umezibwa nitafute mwengine, mimi mwenyewe changamoto hiyo nilipata. Ilikuwa anayekwenda pale anaambiwa alipe shilingi 40,000 lakini kwa bahati anaongezewa na 20,000 anaambiwa shilingi 60,000; akitoa zile shilingi 40,000 anaandikiwa shilingi 20,000 anaambiwa bado shilingi 20,000 ili atapokwenda kutoa zile shilingi 20,000 ndio anapewa risiti na ishirini zile zinafanyiwa vyenginevyo. Ilikuwa si jambo zuri na hilo halikuwa siri nililizungumza mpaka Baraza la Wawakilishi na nikawaomba Wajumbe wa

Baraza la Wawakilishi wanawake wenzangu wakanisaidia sana kwa hili mpaka nikakipata kithibitisho nikamkamata mtu mkononi aliyefanya hivyo.

Kwa hivyo, hapa kuondoshwa hiki kweli inaweza ikapita mbinu nyengine, mara kuambiwa sijui ongeze dawa, sijui ufanye hivi, mbinu na vichochoro vitakuwepo. Sasa ninacho ona katika hili wale wanaofanyiwa mambo haya wawe wazi kuweza kuripoti, kuna hofu kweli maana yake mtu anahisi kama sikufanya hivi ana hofu huenda mgonjwa wangu asihudumiwe vizuri. Kwa hivyo, mimi namuunga mkono sana Mhe. Waziri kwa hili kwa kuwa wale wanaohisi wanafanyiwa hili wapige simu na ziwekwe simu maalum japo za siri wawe wanapiga ili kuona kuwa hili linafanikiwa. Hii hapa naungana kabisa na suala la kwamba watu wapewe vitambulisho chenye jina na kila ajulikane yule aliyemfanyia kitendo kile ni nani aweze kuripotiwa.

Nikija ukurasa wa 41 alitoa changamoto katika wito wa madaktari uliopo ndani na nje warudi ili kusaidia nchi yetu katika huduma. Mimi naungana na yeye kabisa huduma zile tuziboreshe mambo yetu yale ya kuwaenzi madaktari wetu ili wafanye kazi kwa nguvu zote, kwa sababu wako ambao si wazalendo wameondoka wanasahau mtu kwao na mtu hata kama ukipata kidogo lakini ukipata uradhi wa wazazi wako basi unaweza kufanikiwa na hata ukipata hicho kingi kama huna uradhi wa wazazi wako unaweza usifanikiwe, warudi. Lakini mimi nilikuwa naomba kumuuliza tu Mhe. Waziri, hivi wanaohitajika ni madaktari tu wauguzi hawahitajiki? Mbona wauguzi nao ndio wanaochukua kazi kubwa pale katika huduma zetu. Daktari akishaandika ni muhimu kweli tunamthamini akishaandika anaondoka, muuguzi ndiye anayefanya kazi kubwa iliyobakia na bila ya muuguzi mgonjwa hawezi kupona. Daktari utaandika wende mhudumu akisema mimi nitampa hii na hii simpji mgonjwa hatopona.

Kwa hivyo, nadhani si hili tu la kusema warudi lakini hata na katika haya maslahi na wao waangaliwe vizuri. Kwa sababu jamani wauguzi wanafanya kazi kubwa, uuguzi kazi sote tunajua, tunauguza wazee wetu nyumbani wakati mwengine mnaweza mkafikishana mahali mkaanza kugombana, sasa hili ni jambo kubwa na zito. Kwa hivyo ningeliomba sana na hao wauguzi kama wapo warudi na wao muwaangalie sana kwa maslahi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niende kwenye Hospitali ya Mwembeladu. Hospitali ya Mwembeladu mimi ningeomba jamani mfanye jitihada kwa hali yoyote, hao hao madaktari wachache tuliokuwanao madhali wako *gynecologist* basi tuwagawe japo kidogo wawe wanakwenda kule kupunguza *crowded* ya Mnazi Mmoja jamani. Mnazo Mmoja sasa hivi wagonjwa wako wengi na wengi sasa hivi wanakuwa *scissor* halafu wakati wa sasa hivi ndio hali tunajua kinamama wanashiba, watoto wanakua matumboni, wanafika

wakati mwingine wanashindwa, mana wa kujisaidia au *pressure* na nini tunakula machipsi mtu anabeba mamba yake mwezi wa kwanza mpaka anazaa anapiga chipsi na zege. Sasa wakati mwingine *pressure* inapanda sasa matokeo yake wanashindwa.

Sasa ile hali ya Mnazi Mmoja Hospitali inazidiwa tungeomba sana jamani wenzangu wa Wizara ya Afya nikisema wenzangu wa Wizara ya Afya nadhani mnanitambua kwa sababu na mimi ni mdau wenu, mjitahidi katika hili apelekwe daktari madhali *theatre* imekamilika hili jambo liweze kupungua.

Mhe. Naibu Spika, niendele katika ukurasa wa 45 katika suala zima la Mfamasia. Mimi nipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sababu niliangalia bajeti iliyopita imeonekana kwa kuwa bajeti ile kweli ilipangwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ichangie na *DANIDA* ichangie. *DANIDA* 1.5 lakini walichangia shilingi bilioni moja, SMZ wao ndio kabisa walichangia asilimia 35 kwa kiwango kilichopangiwa ni kidogo. Lakini na hapa nataka kumpongeza Mhe. Rais kwa kusema sasa masuala ya dawa tutajikita sisi wenyewe. Kwa hivyo, nimefurahi kuona mchango wa *DANIDA* 1.5, mchango wa SMZ 1.5 sawa kwa sawa. Hili napongeza na naomba sana kuwa hiki kilichopangwa safari hii tuiombe Serikali unajua Wizara peke yao jamani hawataweza.

Serikali mimi naiomba basi hiki kiwango tunachokipanga tunakaa hapa jamani tunapoteza muda, tunaeleza mambo, lakini wakati mwingine hizi fedha wenzetu hawazipati wafanye kila hali ili tujikimu kwa dawa.

Mhe. Naibu Spika, “mtegemea cha ndugu hufa masikini” kwa hivyo naomba sana niende haraka haraka katika suala la upungufu wa wafanyakazi nimesoma kipengele nambari 56 nimesoma idadi, lakini mimi nilisema na sasa nitasema. Pamoja na watalamu, lakini wataalamu bila ya kuwa na wasaidizi mambo hayendi, ukiacha wataalamu wa madaktari, wa wauguzi, wa lebo, wa nani bila ya wasaidizi hawendi na wasaidizi wa hapa ni ma-*orderly* Mheshimiwa. Lakini inaonekana nafasi ya *orderly* kama, haina nafasi kabisa tutaalamu kila siku mana si watu kidogo.

Mimi niliwahi kwenda pale Mhe. Naibu Spika, imetokea ajali haki ya Mungu namuonea huruma nesi, pale mgonjwa kaja yuko *serious*, huyu wa mwanzo anataka kuhudumiwa *nurse* mmoja, sasa *nurse* huyo kweli atafanya kazi ya kufanya shughuli zile zote afanye na usafi? Tuone jamani jipangeni Serikali, hii Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na kuona sisi jamani lazima wengi wataalamu lakini wataalamu bila ya wasaidizi hawendi na hospitali inahitaji usafi, usafi ndio kitu cha mwanzo. Watu

wanatoka wanakwenda *private* kufuata mambo ya usafi tu, anafika pale anahudumiwa mpaka ataondoka japo kapewa *aspirin* lakini karidhika na usafi, hebu tujitahidini tuone umuhimu wa ma-*orderly* jamani tuwajirini.

Mimi nimekwenda hospitali moja ya India wanaiita Chinai pana aina tatu ya ma-*orderly*, kuna *orderly* wa kupeleka mgonjwa tu na kurudisha lebo, *X-ray*, *theatre* basi, kuna *orderly* kazi yake asafishe makabati tu na madirisha, kuna *orderly* kazi yake kusafisha kitanda tu na kufanya usafi wa chini. Kwa hivyo mimi ningeomba sana jamani hili jambo tulione. Mengine nayaacha Mhe. Naibu Spika, namalizia la mwisho.

Nilikuwa na mengi nitauliza maswali huko usoni lakini hili kidogo Mhe. Waziri kakaangu, ndugu Mhe. Naibu Waziri na wapenzi wangu, Makatibu Wakuu kina Dr. Jidawi, Dr. Malik, kina Bwana Juma wote wapenzi wote wa Wizara ya Afya, lakini kwa hili mimi kidogo sitosema ninakubali au ninakataa mpaka nipewe jibu la kuridhisha.

Nina Kituo cha Afya tena ni *first line* tu, huwahudumia pale watu wanaopata mambo huyu katafunwa na nyoka huyu nini kipo Bumbwisudi. Toka mwaka 2010 huu mwaka wa tatu Katibu Mkuu aliahidi mbele ya Makamu wa Rais kwa kipindi kile sasa hivi Rais wa Zanzibar, kwa kuwa hatua tuliyofikia mpaka ya kuezeka atakimalizia, lakini jii mpaka hii leo. Nimekwenda kishoga, kirafiki kimya, sasa hata kuna maneno nimepenyezewa penyezewa lakini nataka niyasema hapa hadharani kila mmoja ayasikie mchana huku kuna ndege anashuhudia. Niambiwe kituo kile kitamalizwa lini, mwezi gani na mwaka gani na wenyewe watu wa Bumbwisudi wasikie limekuwa kero. Kwa sisi viongozi wa kule mpaka Rais wetu imekuwa bughdha haifai tumaliziwe.

Mwisho kabisa ningeomba pamoja na mikakati iliyopangwa kwa kuwa sasa hivi tusingeze tena vituo hatuungezi, lakini tunaomba tulivyoanza tumaliziwe. Kuna mazingira magumu katika maeneo yaangaliwe mazingira. Nitatoa mfano Jimbo la Konde kuna mahali tulijenga vituo kule karibu vitatu papo kwa papo, Mkia wa Ng'ombe sijui wapi na wapi, lakini sasa kutokana na hali ya mazingira, kwa hivyo yale maeneo ambayo mazingira yetu sio mazuri mtusaidie tuvimalize. Mimi sitoongeza lakini naomba nilivyofikia nivimalize hicho nilichokuwa nimeshafikia hatua ya kuezekwa cha Bumbwisudi, ahadi imetolewa na Makamu wa Rais kimaliziwe ningeomba na hivyo vyengine viwili ambavyo kimoja kiko Kianga na chengine kiko Kinuni Mhe. Naibu Waziri alikuja pia akakiona ningeomba hivyo, kama hata sera yenu au utaratibu wenu hauko kwenye kumalizia tutafanya jitihada sisi wenyewe tumalizie lakini mturuhusu tuvimalizie.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana lakini kama nilivyosema kwa kuwa sitoi kauli ya moja kwa moja ninakubali au ninakataa mpaka nipewe jibu. Ahsante sna Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi fupi kabisa leo ya kuzungumza machache katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nitoe shukurani zangu za dharti kwa wale wote waliohusika na utungaji wa kitabu hiki cha bajeti kwa sababu kimeandikika vizuri, kinafahamika na kimeeleza ukweli ulivyo; penye matatizo pameelezwa na kadhalika.

Halafu mwisho nitoe shukurani za pekee kwa Mhe. Shawana Bukheti Hassan, huyu alikuwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii wakati huo, huyu ndiye aliyesababisha nikajenga kituo pale Bwagamoyo na mmeshuhudia ametoa mchango mzuri sana. Mwisho Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii.

Kwa kuanzia Mheshimiwa naomba nianze na programu ya kudhibiti maradhi ya malaria. Kwanza niishukuru wizara kwa juhudi kubwa waliochukua kwa kupambana na malaria kwa upande wa kutia dawa majumbani, ugawaji vyandarua na kwa tiba nzuri ya vidonge vya dawa mchanganyiko.

Mhe. Naibu Spika, takwimu inaonesha kuwa asilimia 85 ya ugawaji wa vyandarua imekamilika na vyandarua vyenye dawa tena vizuri laki moja na sitini elfu vimegawiwa, nataka kujua hii asilimia 15 ambayo imo katika hali ya afya hatarishi itashughulikiwa namna gani.

Pili, nishukuru pia kwa namna walivyofanya kazi ya uchunguzi wa malaria, kuna uchunguzi ambao wametumia darubini, kuna uchunguzi ambao ni wa haraka na kwa jumla jumla ukichanganyisha kwa chunguzi zote wastani wa asilimia 0.87 ya maradhi ya malaria ndio iliyobakia. Mimi suala langu hapa ni kuwa hii njia ya haraka ya kuchunguza malaria ambayo hutumii darumini ni njia gani na ina ufanisi gani. Pia katika vituo hivi hakuhitajiki nako kwenda darumini.

Halafu jengine Mhe. Naibu Spika, ili malaria iondoke pia kuna ulazima wa kupambana kwa kuviondoa zile sehemu ambazo mbu wa malaria huwa wanazaana kwa wingi. Kuna mito iliyokuwa maji yake hayendi mbali sana au hayendi kwa nguvu, kuna maziwa, kuna na mahodhi yamekaa ovyo hayatumiki na siku za mvua yanajaa maji pamoja na maeneo mengine. Hizi ni sehemu ambazo mbu huwa wanazaana kwa wingi, sijui Mhe. Naibu Spika, Wizara imechukua hatua gani ikaona kuwa sehemu hizi haziwi chanzo cha

uzalishaji wa mbu wa malaria tena kutokana na kuwa Serikali inatumia fedha nyingi kwa kupambana na maradhi haya.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ninaloomba kuzungumza kwa ruhusa yako ni kuhusu kitengo cha afya bandarini. Tumeona namna ya kitengo hiki bandarini kinavyofanya kazi kwa uchunguzi wa abiria wanaoingia hapa Zanzibar kwa kupitia ama usafiri wa baharini au wa angani. Lakini nimeona hapa katika taarifa moja ambayo nataka nipewe maelezo ni kuwa kwa upande wa Uwanja wa Ndege kuna watu 615 ambao ni watu kutoka nchi za nje na hawakuwa na vyetu vya kuonesha kuwa wamechanjwa hii homa ya manjano na kuwa wanaohusika walisema kwa sababu nchi wanazotoka au maeneo wanayotoka si maeneo hatarishi.

Mimi nataka nipewe maelezo hawa ni wasafiri wamekuja Zanzibar kutoka nje tukiachilia mbali hayo maeneo wanayotoka kuwa si maeneo hatarishi lakini hawa ni binadamu wanatembea kila pahala, haina maana kwamba maisha walikuwa katika maeneo hayo ndio wakaondoka kuja hapa Unguja. Je, kwa kuchukulia tu maeneo wanayotoka kuwa si hatarishi inatosheleza kuwa wasichukuliwe hatua za kupata chanjo ya homa ya manjano.

Halafu (b) kuna wasafiri wanaingia kwa njia za panya katika sehemu chungu nzima za Unguja na Pemba. Masheha wanapewa mamlaka gani ya kuona kuwa watu hawa wanaoingia kutoka nje ya Zanzibar wana uhakika wa kuonesha kuwa huko wanakotoka wameshughulikiwa kwa matatizo haya ya maradhi ambayo ni hatarishi kwa kuingia hapa kwetu.

Pia nimeona kuwa wote wanaofanyiwa uchunguzi ni wale watu ambao wanatoka nje ya Tanzania, hivyo tuseme huko Tanzania Bara hakuna maradhi hatarishi nchi kubwa ilivyo, kuna wengine hawatoki Tanzania Bara lakini kuna wanaotoka Tanzania Bara wa mbali zaidi kuliko hao ambao hawatoki kwa kutizama ukubwa wa ile Tanzania Bara ilivyo na mazingira yake, maziwa na kadhalika na maradhi waliyonayo mengine hatuna huku ilikuwa kuna sababu gani wao wakaachiwa *free* na hawa ndio wale wengine wanaoingia kwa njia wanayoitaka.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ninaloomba kuzungumza hapa kwanza natoa pongezi kwa Mhe. Waziri kujielezea hali halisi ilivyo katika Wizara yake, Mheshimiwa tukiangalia kiambatisho nambari 10 kilichoko ukurasa wa 107 kule kuna maelezo yanayoonesha kuhusu hali halisi ya wafanyakazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ndio hospitali yetu kuu tunayoiita Hospitali ya Rufaa ina mapungufu makubwa namna hii

hiki ni kielelezo tosha kuwa hospitali zetu pamoja na vituo vya afya vyengine tulivyonavyo vya Serikali viko katika hali mbaya nchi nzima. Kwa hesabu zangu za haraka haraka ni kuwa katika kada 26 mbali mbali Mhe. Waziri alizoziingiza katika kiambatisho hiki mahitaji halisi ni wafanyakazi 732 kwa kada hizi 26. Kama sikukosea katika hesabu zangu za haraka haraka waliopo ni 349 na upungufu ni 383. Hii ni hatari kubwa sana.

Sasa katika mapungufu kuna kada 11 katika hizi 26 hakuna hata daktari mmoja anayehusika na kada ile, tuseme kama watu watakuwa na matatizo ya maradhi na kada hizi hazina madaktari watu hawa wanatibiwa vipi na hii ni jumla ya wafanyakazi 168 wanaohitajika katika wale ambao hapana hata mmoja katika zile kada 11 ambazo hazina hata mmoja. Hivi ndivyo hospitali yetu kuu ilivyo.

Sasa ikiwa kule jikoni kwenye Hospitali Kuu hali ni hii Mhe. Naibu Spika nina hakika huko kwengine kazi inakwenda kwa kudura ya Mwenyezi Mungu tu. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri afanye kila inavyowezekana aweke mikakati ya hali ya juu na kuona kuwa hii hali inabadilika na ni vipi atabadilisha naomba aje atueleze.

Halafu jengine Mhe. Naibu Spika, ni Kituo cha Afya Mbweni ambacho hiki jadweli yake iko kwenye ukurasa wa 115, hiki ni kituo na ni kimoja tu kwa hapa Zanzibar ambacho tunategemea kitatusaidia kuondoa upungufu wa madaktari na wahudumu wengine katika Zanzibar hii.

Kuna mambo katika kituo hiki naomba nipatiwe maelekezo, mfano kwenye kada ya *nursing* wako wanafunzi 79 wa mwaka wa mwanzo lakini wa mwaka wa pili hapana hata mmoja, ina maana mwaka wa nyuma hawakuchukuliwa au vipi naomba nipate maelezo.

Halafu kwa mwaka wa tatu wako wanafunzi 98 na mwaka wa nne kuna wanafunzi 13 ambao ni wanawake tu hao wanaume wote waliokuweco huko walifeli au ilikuwaje? Na kwa nini kama mwaka wa nyuma hawakuchukua kulikuwa na sababu gani, watoto hawaku-*qualify*, nafasi zilikuwa ndogo au kulikuwa na sababu gani.

Halafu tena kuna kada hizi ambazo mfano ni *clinical medicine, dental* na kadhalika na kuendelea zote mwaka wa nne hakuna mtu hata mmoja. Naomba nijue kuwa hizi zinachukua kozi kwa muda wa miaka mitatu tu na nyengine miaka miwili tu, naomba nipewe maelezo.

Halafu la mwisho kuna kada ya mwisho hii wameandika *PHL "B"* (*Pre-service*) mwaka wa kwanza hamna, mwaka wa pili hamna mwanamme hata

mmoja ni wanawake tu, Nikitaka kujua kuwa na hiyo wanaume haiwahusu na kadhalika. Hapo ndio ilivyo.

Nikirejea tena Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako Mwenyezi Mungu katujalia tumepata chombo kikubwa cha uchunguzi wa maradhi kadhaa hapa Zanzibar tunaita *CT-Scan*. Kwa bahati mbaya wala si kwa bahati mbaya lakini ni kwa ufanisi wa matibabu baadhi ya wagonjwa kule Pemba hulazimika kuja hapa Unguja kwa kupata uchunguzi wa kutumia chombo hiki. Lakini mimi binafsi labda kiasi watatu washarudi Pemba kwa kushindwa kuwasaidia kutokana na kuwa walikuwa lazima walipe mwanzo ndio wafanyiwe huo uchunguzi.

Mimi Mhe. Naibu Spika, ninavyojua tuliambiwa kuwa kwa wale ambao hawana uwezo watafanyiwa bure, sasa sijui mtu aseme hana uwezo namna gani mpaka akubalike ndio tena aweze kufanyiwa. Na hata siku moja nilikuwa na Mhe. Abdi Mosi tulikwenda kule tukamkuta jamaa ambaye aligongwa na gari alikuwa *totally unconscious*, lakini kawekwa kule katika kile chumba hafanyiwi matibabu mpaka alipiwe na ikabidi wale jamaa zake waweke rehani simu zao wapate pesa ndio afanyiwe mambo ya uchunguzi. Kwa hivyo, ningeliomba kama hali hii Mhe. Waziri hajui haya mambo mimi niliyashuhudia na naamini kuna mengine zaidi ya haya yametokea, atufanyie utaratibu kile chombo kimewekwa makusudi kwa kutusaidia sisi vyenginevyo ilikuwa fedha nyingi zitumike kwa kwenda nje. Vipi itawezekana mtu aliyekuwa hana uwezo aweze kufanyiwa uchunguzi kwa kutumia chombo hiki.

Mhe. Naibu Spika, ..

Mhe. Naibu Spika: La mwisho.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Kasoro moja mhesimiwa basi hili ninasema tu. Niliwashukuru Mhe. Waziri na Naibu Waziri wanavyotembelea katika vituo vya afya Pemba na Unguja, lakini ninasikitika kuwa mtendaji mkuu wetu yaani Katibu Mkuu hatujamsikia sana kuja kule Pemba. Kwa hivyo kutokuja kwake kuna mambo mengi yanatuharibikia. Tunamuomba aje.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, kwa hilo. Kumezungumzwa hapa ukurasa wa 92 kuwa kuna vituo vimeongezeka kiasi ambacho serikali haina uwezo wa kuvihudumia. Pia imezungumzwa katika ukurasa ambao nimeusahau kuwa moja katika miradi ambayo itakayofanywa na wizara ni kuvifanyia matengenezo baadhi ya vituo na kutoa samani kwa mule ambamo wamefanya matengenezo.

Kimoja kati ya vituo hivyo ni kituo cha Mzambarauni. Mhe. Naibu Spika, kituo hiki kipo katika hali mbaya sana na sidhani kuwa kinaweza kikafanyiwa matengenezo badala ya kuwa kijengewe kipya. Kwa hivyo naomba na vile hivi sasa tunatumia nyumba ya kukodi, wizara ijitahidi kwa hali ya kituo kile kilivyo kutengenezeka na kwa sababu wataalamu walisema hali ya ardhi ilivyo na vile kilivyojengwa hakiwezi kikaishi kwa muda mrefu afanye kila inavyowezekana pale watujengee kituo kimoja kikubwa.

La mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya shida ya matibabu na kwa sababu ya ushauri ya Mhe. Shawana Bukheit alipokuwa ni Naibu Waziri wa Afya, tuliamua kujenga kituo chetu wenyewe pale Bwagamoyo kwa ushauri wa wizara, tumetumia pesa nyingi sana kituo tumekwishakukiezeka, tumeshapiga plasta nje na ndani, tumeshatia milango na madirisha, nguvu hatuna tena na ukitizama pamoja na kuwa wizara imeeleza kuwa kwa mujibu wa msambao wa vituo vyake vilivyo haifiki kilomita tano watu wanapata huduma. Lakini kwa vipimo ninavyovijua mimi kutoka Makongeeni mpaka Uwondwe ni zaidi ya kilomita kumi, kutoka Makongeeni mpaka Mzambarauni au Bahanasa ni zaidi ya kilomita kumi na kutoka Uwondwe kwa kupitia njia ya zamani hali ndio hiyo hiyo.

Ndio maana tukaona tujenge hiki kituo hapa kati kati. Kwa hivyo tuifanye hii ni special case na Mhe. Waziri aone huruma tumepoteza pesa na tumetumia kwa sababu ya kuondoa shida na kituo kimefunguliwa na Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itakuwa ni aibu kuendelea kuwa ni kituo cha kuuzia karafuu.

Sasa basi ningeliomba awaambie wananchi wa Mtambwe baada ya juhudi yao kwa kituo hiki ameweka msimamo gani. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na mengi ya kueleza lakini kwa sababu ya wakati si haba hapo nilipofika. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana mhesimiwa. Sasa Waheshimiwa waliobakia ni watatu, naomba nusu saa kila mtu apate dakika 10. Kwanza ni Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Wanu Hafidh Ameir na mwisho Mhe. Bikame Yussuf.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Allah Subuhana Wataala kwa uwezo wake kunijaalia mchana huu kupata nafasi hii adhimu na mimi kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya.

Pili sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kukushukuru kwa kuniwezesha kupata nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu utaanza katika ukurasa wa 32 kifungu cha 3.8 pale “Matibabu ya nje ya Zanzibar kwa wale ndugu zetu ambao kesi zao haziwezi kumalizika hapa nchini”.

Kwanza niishukuru hii bodi ya Medical Board katika uangalizi wao wa kuwapatia fursa hawa ndugu zetu walio na maradhi haya sugu. Mhe. Naibu Spika, ninataka niambie bodi kwamba moja wamuogope Mwenyezi Mungu sana, jukumu walililopewa kubwa. Kuna wagonjwa kati ya hawa elfu moja na thamanini na sita ambao waliowachunguza na wakawaona kwamba hawa wanastahiki kwenda nje ya nchi, lakini pia uwezekano wa kuwapeleka wote haikuwezekana, wakati huo karibu watu mia moja na hamsini na saba.

Mhe. Naibu Spika, hapa pana kazi ngumu sana. Inawezekana katika watu hawa elfu moja na thamanini na sita, kuna baadhi yao waliitaka fursa hii ya kwenda kupata matibabu nje. Lakini pengine kutokana na umasikini wao na kutokana na udhaifu wa kutokuwa na watu wa kuwashughulikia imebidi watu wameganda. Mwanadamu ni uzima, mwanadamu anapokuwa na maradhi basi hana tabasamu nzuri, hata zile fikra zinakuwa ni ndogo.

Hivyo ningeliomba sana hii bodi kufanya haki zaidi, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, dunia hivi sasa inaendeshwa na mambo mawili, umaarufu na pesa. Kuna baadhi ya wagonjwa wetu hawana umaarufu, hawana watu wanaowajua katika idara kama hizi basi wasiendeleo kusota wakabakia katika maeneo yao ya kupangiwa tarehe za kila siku, kila mwezi na kila mwaka, maradhi yanaweza yakawachukua haraka. Kwa hivyo ni vyema waangalie kuripoti kwa wagonjwa hao katika vituo vyetu ili na wao waweze kuwajua zile hali zao. Ningeliomba sana bodi hili walifikirie sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kila ukiangalia kwamba hili tatizo la kupeleka wagonjwa nje ya nchi kila tukiendelea linakuwa ni sugu sana hasa ukiangalia kuna watoto karibuni sitini na mbili; watoto wadogo hawa wamepelekwa kwa tatizo la moyo, ni tatizo kwa kweli na inawezekana yakawaingia matatizo haya haya ya moyo lakini kutokana na uwezo wa serikali bodi ikaamua iwapeleke watoto hawa sitini na mbili. Kwa kweli hili ni tatizo mimi ningeliomba sana wizara kwa kushirikiana na serikali kwamba tutafute wataalamu tunusuru pesa nyingi kuzipeleka nje ili wataalamu hawa waweze kuja kutoa tiba hapa hapa nchini.

Ningeliishauri sana wizara kupitia serikali kwamba kutokana na maradhi haya yapo kwa wananchi kila mara na yanazidi yanatutesa, basi kuanzisha mfuko huu wa kuwasaidia hawa wagonjwa waliotaka kwenda matibabu nje ya nchi. Kwa sababu tukitegemea tu pesa kutoka serikalini, hii itakuwa ni ngumu sana

kwa sababu serikali ina mambo mengi na inahitaji kupeleka katika maeneo mbali mbali.

Lakini tukianzisha mfuko wa maradhi haya kwa ajili ya wagonjwa wetu wanaokwenda nje basi unaweza kusaidia badala ya kupeleka watu mia moja na hamsini na saba, siku nyengine tukaweza kupeleka wagonjwa wote wanaohusika na maradhi haya. Kwa hivyo ningeliomba sana wizara kuanzisha huu mfuko na kuwasaidia wagonjwa wetu hawa wanaopata matatizo kutoka nchini kwenda kupata matibabu nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo kuna suala zima la kudhibiti malaria. Kwanza hapa ninaipongeza sana serikali kwa jitihada kubwa waliyochukua ya kuweza kuyadhibiti kiasi fulani maradhi haya ya malaria. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, serikali ilichukua juhudi ya kutafuta wataalamu nchi mbali mbali ili kutoa elimu kwa baadhi ya madaktari ili waweze kusaidia maradhi haya ya malaria. Kwa hivyo kumetayarishwa hapa matibabu ya malaria kwa watoto wa siku hadi kufikia miaka mitano kwa Pemba Kaskazini na kwa hapa Unguja Kaskazini vile vile, na madaktari hawa wakachukua mafunzo nchi ya Sweden ili iligharamia kuwasomesha hawa madaktari wetu ili tu-save hawa watoto waliozaliwa kuanzia siku moja hadi kufikia miaka mitano na wakaahidi hawa kwamba gharama zote zitakuwa ni juu yao na wale watakapasi katika masomo yao watawazawadia vyeti vyao.

Mhe. Naibu Spika, inasemekana kwamba hivi vyetu tayari vimeshaletwa hapa nchini toka waliposoma vijana hawa 2010 hadi kufikia leo 2012/13 vyeti hivyo vimeganda, vimeshindwa kupewa wale wanaohusika.

Ningelimumba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze kama taarifa hii anaijua au vipi, lakini tujue ni sababu gani iliyozuia kwa wahatimu hawa kutopewa hivi vyeti vyao.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo kwa haraka haraka kwenye ukurasa wa 82 kifungu 11.5 kinachohusu kupandisha daraja hospitali za vijiji zikiwemo hospitali za Vitongoji, Kivunge, Makunduchi na Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la faraja sana na serikali imeleta maamuzi mazuri katika hospitali zetu hizi hasa ukiangalia kwamba katika Wilaya ya Micheweni, hospitali peke yake ni hospitali hii ya Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hospitali hii ya Micheweni haikidhi haja. Kwanza harufu ya hospitali hii ni mbaya, inanuka. Mhe. Naibu Spika, mgonjwa anaweza kuja na maradhi yake moja tu pale hospitali lakini kutokana na uchafu uliopo pale anaweza akapata na maradhi mengine

ambukizi kutokana na harufu mbaya iliopo katika hospitali ile pale. Kwa hivyo mwanadamu aweze kuishi vizuri, kwanza unaangalia ni mazingira ya usafi.

Mhe. Naibu Spika, usafi wa pale hapana, ndani ya majengo yale munafugwa kuku humo humo hospitalini, kuku wanatembea huku na kule wanachafua mazingira mule, wanakunya ovyo ovyo. Sasa yala mazingira kwa hospitali kwa kweli hayapendezi na haya kwa kweli ni mambo ambayo yapo muda mrefu na Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na wengine wanakwenda katika hospitali hizi na wanawaona, lakini mambo haya ya kufumbiana macho ndio yaliyotufikisha pahaya.

Kwa hivyo ningelimuomba sana Mhe. Waziri suala hili linahitaji kukemewa sana bila ya usafi katika maeneo haya ya afya yanaweza kuambukiza maradhi mengine mbali mbali. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, na vile vitanda wanavyolalalia wagonjwa ni vitanda vya muda mrefu na haya magodoro ni juzi tu wamebahatika kupatiwa, lakini Mhe. Naibu Spika, akitokezea mgonjwa kuharibikiwa pale basi kitanda kile kitaweza kubakia hivyo hivyo mpaka godoro lile likoshwe likauke na ndio kitanda kile kinaweza kikapata mgonjwa mwengine huduma. Hili ni tatizo Mhe. Naibu Spika.

Hivyo ningeliomba sana wizara wakati wamesema hizi wanataka kuzifanya ni hospitali za Wilaya, basi ni vyema tuanze haya maeneo tuliyonayo yaridhishe, kutokuridhisha sehemu hizo basi tutakuwa tumepamba jina tu. Mhe. Saleh asubuhi alisema hapa itakuwa tumeandaa jeneza, nje zuri lakini ndani matatizo.

Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri suala la vitanda kuwa na shuka moja, kitanda kuwa na godoro moja, hili ni tatizo ni vyema vikaboreshwa vitanda vyetu vikawa vya kileo vya kisasa na angalau vikawa na magodoro na mashuka mawili, kinyume na hivyo malengo hayo yatakuwa ni ndoto.

Mhe. Naibu Spika, ...

Mhe. Naibu Spika: Muda.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, kwa kumaliza nije katika vituo viliopo katika Jimbo langu la Tumbe.

Mhe. Naibu Spika, Tumbe tunavyo vituo vitatu, Shumbaviamboni, Sizini na Tumbe yenyewe. Lakini Mhe. Naibu Spika, kituo cha Sizini hatuna daktari ni kituo kipo tu. Kituo hiki ni kibovu, inawezekana kuanguka wakati wowote kituo hiki kutokana na mashambulizi ya mchwa.

Mwaka jana nilijaribu kupiga dawa mara moja lakini mchwa ule ni kama mti uliotiliwa mbolea, umetafuna makechi yote, wakati wowote kituo hiki kuanguka na kinawezekana kikapoteza uhai wake. Hakina daktari. Daktari aliyeopo na watoto wote walioanza kuzaliwa siku moja hadi kufika miaka kumi na tano, hawa waliowengi hivyo wamekosa daktari wa kuhudumikia watoto katika kituo cha Sizini.

Lakini pia hapa Tumbe, kituo chetu ni kidogo mno Mhe. Naibu Spika. Hiki kituo kimekaa kama nyumba ya ndege. Mhe. Naibu Spika, nyumba ya ndege ina mlango mlango, huku nyuma hakuna mlango na hiki kituo ndio kilivyo. Kwa hivyo ikitokeza emergency pale kwenye kituo, umeme ukaleta short pale basi kuna uwezekano watu wakauawana wao wenyewe bila ya kuguswa na huo umeme kwa hali halisi ilivyo.

Lakini pia kituo hiki hata fensi hakina. Mwaka jana hapa nilisema kwamba kituo hiki ni kidogo kutokana na population ya watu wa Tumbe; Tumbe pana watu kumi na tatu elfu na ziada na wanategemea kijibanda hiki. Kwa hivyo ningeliomba sana wizara kutuangualia sisi watu wa Tumbe pale, Tumbe ndio city ya jimbo, lakini ukija katika mazingira ya utibabu hawana maana ya aina yoyote.

Hivyo ninasema tena kuhusu suala hili na hata mwaka huu ukiuliziwa kwamba Tumbe tutafanya nini hakuna na mwaka jana tulisimama tukapiga kelele kuhusu kituo chetu hiki cha Tumbe angalau kiboreke Mhe. Naibu Spika, na sisi tujione kwamba tunachangia kweli katika nchi hii na serikali yetu imetujali watu wa Tumbe. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache kutokana na muda wako naunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Afya Mhe. Juma Duni Haji.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia ninaanza kwa pongezi za kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake lakini pia nimpongeze Waziri kwa kuchukua jitihada kubwa ya kuifanyia matengenezo ICU.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza na Idara ya Hospitali ya Mnazimmoja ukurasa wa 36 na ninaomba nianzie na Hospitali yenyewe ya Mnazimmoja. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Rais kwa kuondoa malipo ya akinamama waja wazito wanapopata huduma ya kujifungua. Mhe. Naibu Spika, lakini mimi nitoa indhari kwamba kufanyiwa huduma hizi bure isiwe tena ndio mwanzo wa kunyanyaswa akinamama. Hili Mhe. Waziri ameliona na katika hotuba yake nimeona amegusia kwamba mtu yeyote ambaye

atakayefanyiwa harassment asisite kuonana na uongozi wa juu wa wizara. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo mimi naomba nizungumzie wodi ya maternity. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kwa kweli wodi ya maternity wodi hii ni ndogo haitoshi, vitanda vyenyewe havitoshi. Kwa kweli akinamama wawazito wanapata shida, wanalala watatu mpaka wanne, kwa kweli wanapata taabu sana.

Lakini ukiachia hilo Mhe. Naibu Spika, idadi ya wazazi wanaofika pale kwa kweli ni kubwa kuliko huduma zinazopatikana pale. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri hilo aliangalie kama alivyojitahidi kuimarisha ICU, ajitahidi na wodi ya maternity kwa kweli inahitaji kuimarishwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hili haliathiri akinamama tu linaathiri pia wale wahuduma wa pale, kwa sababu na wao inawawia vigumu kutekeleza majukumu yao, wanafanya kazi katika mazingira magumu kweli kweli. Hasa pale wanapooona kwamba kazi wanayoifanya kwa kweli hailingani na malipo wanayoyapata. Hivyo zile frustration zao za kufanya kazi katika mazingira magumu kwa kweli zinaishia kwa akinamama na wanapata taabu sana.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo naomba nizungumzie usafi wa wodi ile. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli usafi ni sufuri hamna kabisa. Mhe. Jussa alipochangia alisema kwamba kumeekwa kibao kinasema weka usafi lakini hicho kibao chenyewe pia kichafu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, inaonesha ni jinsi gani kwamba pale usafi pale hamna.

Mhe. Naibu Spika, harufu zimetawala hospitali ile kiasi kwamba zinawazidishia hata maradhi hao wagonjwa ambao Mhe. Rufai Said amesema, kwamba zinawazidishia maradhi hao wagonjwa. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli usafi wajitahidi kama kuna vifungu vinavyohusiana na kununua detergent basi zinunuliwe na zitumike na kwa sababu zile zinasaidia angalau kuweka ile hali ya mandhari safi. Lakini utakuta mtu ana dondoo ya kupigia deki na maji na lile tambara tu basi anapiga deki. Kwa kweli ile haisaidii kitu.

Mhe. Naibu Spika, kitoka hapo katika maternity naomba Mhe. Waziri wakati anaposoma hotuba yake alituelekeza katika kiambatanisho nambari 8 ambacho kinaonesha idadi ya wawazito waliolazwa, waliojifungua na vifo vya akinamama vilivyosababishwa na uzazi.

Mhe. Naibu Spika, penye mama pana mtoto lakini Mhe. Waziri mbona hakutuoainishia watoto wanaozaliwa wangapi wanakuwa hai, wangapi

wanakufa ili tujue ile sijui wanaita mortality rate ya watoto wangapi wanakuwa hai na wanaofariki. Lakini Mhe. Naibu Spika, katika hotuba yake pia Mhe. Waziri wakati mimi ninapitia niliona kwamba kwa kweli maradhi mengi wanawake tunaongoza.

Sasa mimi nilikuwa ninataka ufafanuzi kidogo japo yeye sio daktari lakini ninajua anajua madaktari wanamuelezea haya kwamba ni sababu gani hasa ni almost yote niliyoangalia humu wanawake tunaongoza ni lini. Lakini ninashukuru kwamba kiambatanisho nambari 10 wanaume wanaongoza kwa vifo kuliko hata sisi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo naomba nizungumzie Hospitali ya Mwembeladu kwenye ukurasa wa 42. Mhe. Naibu Spika, niunge mkono dhamira ya wizara ya kupunguza msongamano katika Hospitali ya Mnazimmoja kwa kutaka kuimarisha hospitali ya Mwembeladu ili kuondoa ule msongamano. Kwa kweli hili walifanyia kazi haraka sana na mimi ninaamini kwamba Mhe. Waziri ni mtendaji, kama alivyoliamulia ICU naomba na sisi akinamama kwa kweli atutizame maternity awapeleke hao mabingwa wanaotakiwa Mwembeladu ili angalau ule msongamano katika Hospitali ya Mnazimmoja uondoke Mhe. Waziri kwa kweli akinamama wanapata taabu sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo naomba niingie kwenye Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi.

Mhe. Naibu Spika: La mwisho hilo.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Nitajitahidi.

Nizungumzie Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua kwamba hii bodi inaangalia usalama wa afya zetu na sio ndani tu lakini pamoja na nje. Mhe. Naibu Spika, vipodozi vingi vya akinamama vinavyoingia nchini vime-expire vinatuumbua.

Mimi ninashukuru alhamdulillah ninatunza ngozi yangu ya asili lakini hao wengine wanaotumia hivyo vyengine, vipodozi vingi vinavyokuja vime-expire Mhe. Naibu Spika, kama haiwezekani tuachiwe na mafuta ya nazi yetu, tuendeleo otherwise vipodozi vinavyoingia ndani ya nchi yetu vitatuumbua. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jengine katika bodi hii nilikuwa ninataka ufafanuzi tu mdogo. Kwanza bodi hii ni lini watapatiwa eneo la kujenga ofisi wakati pale

walipo sasa wameshapata notice kwamba mwakani wahame kupisha utanuzi wa hospitali, hilo ni moja.

Lakini pili kuna wafanyakazi walikwenda short course China ya bye technology in development countries. Hawa wafanyakazi walitumia pesa zao. Mhe. Waziri ni lini mutawalipa pesa zao mpaka leo hamujawalipa, wakati kuna wafanyakazi wenziwao ambao walikwenda nao pamoja wa utalii na Wizara ya Biashara alhamdullih wao wameshalipwa, hawa wa Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi hawajalipwa kwa hivyo ni lini mutawapatia malipo yao.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo ninataka ufafanuzi kama tunavyojua kwamba bodi inatizama usalama wetu, lakini inawawia vigumu usafiri walionao hauwatoshi. Kwa hivyo Mhe. Waziri uwatizame juu hili ili angalau wanapopita humo madukani unajua wanakweda mwahala kwingi, atleast wawe wanagawana. Lakini jengine pia katika hii bodi wafanyakazi wa lab ni wawili tu, hawana off wala on, wao siku zote wapo kazini, nalo hili Mhe. Waziri alitazame.

Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mkemia Mkuu haiendani na hadhi yake, jengo ni dogo hadi kuna mashine nyengine wanashindwa kufunga pale, ninasikia wamefunga katika Chuo cha Afya Mbweni. Kwa hivyo wakitaka ku-test samples watoke kule Mwanakwerekwe walipo waje Mbweni kuja ku-test samples. Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba hili aliangalie, anaweza hata akatafuta eneo akajenga jengo moja akaweka upande mmoja Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi na upande mwengine Afisi ya Mkemia Mkuu pia itasaidia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya vijana na niaba ya wanawake wenzangu naunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Bikame Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya njema mchana huu na mimi nikaweza kusimama hapa.

Lakini pia ninakushukuru wewe kunipa nafasi hii ya mwisho katika kuchangia kwenye Wizara ya Afya ingawa nilikuwa nimeshachangia kwa maandishi, lakini kupata hii nafasi naona bora nieleze machache ambayo kuwa pengine yatakuwa yana umuhimu wake.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nikianza na mimi niende katika hiki Kitengo cha Elimu ya Afya. Kitengo hiki kina wajibu mkubwa wa kuelimisha, kuhamasisha na kutoa ushauri kwa jamii kuhusu afya na kinga ya maradhi

kwa kutumia njia mbali mbali ya kubadilisha tabia hatarishi ili kuweza kufikia lengo la afya bora kwa kila mwananchi. Hivyo ndivyo tunavyoeleza mwanzo kabisa.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kitengo hiki kazi yake ndio hiyo lakini sasa jambo la kushangaza, wao katika wizara yao wanashindwa kujisimamia katika suala zima la usafi. Hili Mhe. Naibu Spika, tutalizungumza hata kila mmoja atakayesimama, tutazungumza kutokana na kuwa kila mmoja anakielelezo chake ambacho kuwa kakiona katika anapozunguka.

Mhe. Naibu Spika, mimi karibuni nilikwenda katika Hospitali ya Chake-Chake. Hospitali hii ni centre ya Pemba na ni hospitali ambayo kuwa inakimbiliwa na wagonjwa wanaotoka maeneo mbali mbali. Lakini la kusikitisha Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri vile vyoo pale viliopo nje ambavyo wanatumia wanawake na wanaume, yaani wagonjwa, munatoka funza.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikwenda hivi nikaona kwa macho yangu si jambo la kuhadithiwa. Sasa ndio nikasema lazima tuyazungumze haya musituone kwa sababu tunayarejearejea lakini ni mambo muhimu, ni mambo ya kusikitisha. Mtu anatoka Makangale anakwenda anakwenda hospitali pale, leo ana uwezo gani wa kuweza kukaa pale tangu pengine saa kumi mbili za asubuhi anapofika pale mpaka saa saba akawa hajataka pahala pa kwenda kujisaidia.

Sasa jambo hili linasikitisha sana na jambo moja ambalo kuwa wananchi wetu munawadhalilisha. Mwanamme anaweza kwenda kutafuta angalau bomba akajisitiri lakini mwanamke jee? Vyoo vinatoka mafunza Mhe. Waziri na ninakuomba sana Mhe. Waziri watendaji wako hili walione ijapokuwa wagonjwa nao wana matatizo yao, lakini wao ni wajibu wao, anataka pahala mtu aende akajisaidie. Hilo ni moja Mhe. Naibu Spika.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, kuna hiki Kitengo cha Afya bandarini kwenye ukurasa huu wa 11. Kitengo hiki kina jukumu la kuzuia na kuchukua tahadhari juu ya uingizwaji wa maradhi ya kuambukiza kutoka nje ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, naona usimamizi huu unafanyika katika maeneo mawili tu, aidha bandarini hapa Unguja au uwanja wa ndege hapo.

Sasa Mhe. Waziri kuna maeneo ya bandari nyengine za ndani ndani. Kama Pemba kuna watu wanaotoka Kenya wanapoingilia bandari zile, jee Mhe. Waziri hawa umewaweka katika fungu gani, pengine mtu kakaa huko miaka kumi lakini anaingilia kwa njia ile. Sasa isiwe katika maeneo haya ya

bandarini pengine Unguja au ni uwanja wa ndege unaojulikana hapo. Kwa hivyo hilo Mhe. Waziri nalo pia ulifikirie.

Mhe. Naibu Spika, nikisogea mbele kidogo kuna kwenye ukurasa wa 14 kuna programu ya maradhi yasiyopewa kipa umbele. Mhe. Naibu Spika, kuna maradhi yaliyokuwa hayataki kupewa kipa umbele. Mhe. Naibu Spika, hakuna mwili wa binadamu wowote unaohimili maradhi hata dakika moja. Wazee wa kale wamesema ukidharau chungu mguu utaota tende.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ukisema kuwa unakidharau kichocho au hukipi kipa umbele kichocho basi hatimaye kitazaa maradhi mengine. Lakini ukisema hulipi kipa umbele suala la minyoo ndio linalosababisha pengine watoto wadogo kuwa na matatizo ya mtapia mlo. Lakini ukisema kipa umbele watu wenye mabusha Mhe. Naibu Spika, itakuwa hivyo vijio watu watakwenda kuvitafuta, aah! kwa hili Mhe. Waziri mwanadamu hakuna maradhi yoyote ambayo hayataki kupewa kipa umbele, maradhi yote yanataka kupewa kipa umbele kwa ajili ya kupatiwa tiba au kinga. (*Kicheko*).

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele kidogo

Mhe. Naibu Spika: La kumalizia hilo.

Mhe. Bikame Yussuf: Kuna suala zima hili kitengo cha mwenendo wa kufuatilia maradhi ukurasa wa 19. Mhe. Waziri hapa umetutajia samples 8 za maji kutoka kwenye visima ambavyo kuwa kitengo hiki sijui cha nini, ufuatiliaji za kutafuta samples hizi za nini. Mhe. Waziri nakuomba tuna kisima hapa hukutaja ni maeneo gani pengine ulikwenda lakini pale Tumbe pana kisima chetu ambacho kuwa yale maji hayapo ndani ya usafi, lakini pia hayapo katika hali ya kuridhisha.

Kwa hivyo ninakuomba hawa jamaa utupelekee pale wachukue ile sample ya yale maji ili tuangalie yana matatizo gani au yana kitu gani kwa wananchi. Halafu Mhe. Waziri mimi nikitaka niende katika Hospitali ya Micheweni.

Hospitali hii kwanza ninashukuru wizara kwa kuwapatia akinamama hii utra sound pale ambacho kuwa matatizo mengi yanayowakabili akinamama, lakini hatimaye kupata kifaa kama hichi ninaona kitatupunguzia usumbufu kiasi fulani.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna suala moja nilisikia hapa kuwa pale Hospitali ya Micheweni pana chombo cha X-ray. Hii ninakumbuka kama nilifuatilia mimi, nilikwenda pale hospitali Micheweni nikawa nina matatizo, tukaambiwa twende Wete kwenda kufanya X-ray, lakini tulipokwenda Wete

daktari hayupo, tukenda Chake-Chake lakini Chake-Chake tulipofika daktari yule alikuwa mkali akasema nyinyi kwa nini Micheweni sio munacho hiki chombo? Hebu njoo Mhe. Waziri unipe ufafanuzi ni kweli au ni maneno ya kitaalamu tu

Mhe. Naibu Spika: Malizia muda umekwisha.

Mhe. Bikame Yussuf: Haya. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunashukuru michango ya Wajumbe na ratiba yetu ya jioni atatangulia Naibu Waziri kuja hoja na baadae tutamwita Waziri amalizie na tupitische hotuba yetu.

Baada ya matangazo hayo mafupi naakhirisha kikao hadi saa 11.00 za jioni.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa hapa Barazani, ili Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi wapate kuelewa mambo yalivyo.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kuanza kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote wale ambao walichangia na waliokuwa hawakuchangia, kwa sababu najua kwamba nia walikuwanayo na yakusema walikuwanayo isipokuwa muda haukutosha. Kwa hivyo napenda niwashukuru sana.

Vile vile napenda niwashukuru kwa michango yenu mingi na mizuri na yenye maelekezo na kutaka ufafanuzi. Kwa vile nimepewa sehemu ya haya nitajibu yale ambayo yako katika nafasi yangu.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, nimepewa kujibu swali la Mhe. Makame Mshimba napenda nimshukuru Mhe. Mshimba kwa kufuatilia mambo yanavyopaswa, kwa bahati mbaya hayupo, lakini hata hivyo salamu mtampa. Swali lake la mwanzo lilikuwa linahusiana na vifaa vya maabara, ambalo nililitlea ufafanuzi. Suala hili lililetwa wakati Ofisi ya Makamu wa Pili ilipokuwa inawakilisha hotuba yake. Nakumbuka alii-refer hii karatasi ambayo inakichwa cha habari kinachosema ‘vifaa vilivyokuwa

havikukamilika katika kitengo cha *histopathology*, hicho ndio kichwa cha habari. Lakini kama angekuwa kaisoma hii karatasi ya mwanzo, kuna sehemu ambayo mwisho wake huyo aliyepelekewa barua alisema naomba ninukuu kwa Kiingereza, maana ndivyo ilivyoandikwa na Mhe. Mshimba simkatalii kusoma sio lazima shule, unasoma hata katika maisha.

Kwa hivyo, anasema anafahamu, hivyo twende leo kama kitaalamu. Maana siku ya mwanzo niliposema, nilisema kwa lugha laini ya Kiswahili fasaha ili kila mtu afahamu. Lakini leo itabidi niende kwenye utaalamu, kwa sababu ndicho kinachohitajika.

Mhe. Naibu Spika, sentensi ya mwisho inasema, '*considering the length of time passed after the delivery, it is no longer our company accountability for this missing part or accessories and scratches*. Nilichokuwa nataka ku- *insist* hapa ni *scratches* na ndicho nilichokisema, ni mikwaruzo kwa tafsiri ya Kiswahili. *One of items as mentioned in your letter*. Ina maana kwamba haya ndiyo yaliyokuwa yameandikwa na wao wanasema hawana dhamana hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nilichokuwa nataka kuongezea baada ya yale niliyosema nyuma ni kwamba kwenye utaalamu wa vifaa kama hivi *handling* ni kitu kimoja muhimu sana. Kwa vile vilikwenda vikapandishwa, vikashushwa kama nilivyokuwa nimesema kuna baadhi ya vifaa vilichunika, ndio maana ya *scratches*. Katika vifaa kama vile ukitaka uhakika na usahihi, kama mwenyewe anavyosema kwamba hivi vifaa vina-*check* masuala ya *cancer*. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, havi-*check* masuala ya *cancer* tu, bali vina-*check* mambo mengi, lakini moja kati ya hayo ni *cancer*.

Mhe. Naibu Spika, unapompa mtu uamuzi wa kwamba ni lazima uwe na uhakika, kwa sababu hicho sio kitu chepesi. Wewe unayetoa jibu lile hulichukulii kwa wepesi wala unayempa halichukulii kwa wepesi. Sasa kama hatuna kifaa ambacho kina uhakika wa angalau asilimia 95 basi huwezi kumwambia mtu kitu kama hicho na vifaa vilivyokuwepo vilikuwa vimechunika. Kwa hivyo, kama kimechunika kile kifaa kimoja, ina maana kwamba kifaa hicho kizima hakitofaa, kwa sababu hawatengenezi vipande vipande kule. Kwa hivyo kilichopo ni kuwa ile mashine nzima inatakiwa iwe *replaced* na mashine nyengine na hilo sio jambo la siku moja wala siku mbili. Nilikuwepo wakati wanayazungumza hayo, wakasema kuanzia wiki mbili zijazo tutakupa jawabu. Sikusema vitakuwa *installed* tayari, haviwezi kutoka vinakotoka kwa wiki mbili vikafika. Kwa hivyo, hivyo ndivyo nilivyojibu.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Makame Mshimba afahamu kuwa niliyoyasema nilikuwa nina uhakika nayo wala sikuwa na sababu ya kumdanganya, hainisaidii mimi, haimsaidii yeye wala haimsaidii mtu yeyote.

Suala la pili la Mhe. Makame Mshimba lilikuwa linazungumzia kituo cha Kitope kukosa umeme. Nakubaliana na yeye kwa sababu mimi nimekwenda mpaka katika kituo cha Kitope na nilikwenda katika ziara za kutembelea vituo vyote, sio kwa sababu yake yeye. Wakati analizungumza hili mimi tayari nilikuwa nimeshapita Kitope. Tulichokuta Kitope walilalamikia umeme. Lakini pale tulikuwa na daktari wa Wilaya, tukamuuliza. Tena huyo daktari wa Wilaya tuliyekuwanaye, kama kuna daktari wa Wilaya ambaye yuko *best* kwa Unguja na Pemba basi ni huyo daktari aliyekuwa Wilaya ya Kaskazini B. Kwa bahati mbaya mmemkosa sasa yuko Kaskazini A. Lakini katika Wilaya ambazo zilitenda vizuri, katika kuzifuatilia Wilaya basi Kaskazini B ilikuwa ni *best* nampa hongera sana Dk. Rahma. Mwenyewe nimemwambia na wengine wote nimewaambia.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tulichokwenda kukikuta pale Kitope ni kwamba wakati ule yale ambayo yalizungumzwa jusi, umeme ulikuwa unakatwa katika vituo kwa sababu ya madeni. Kwa hivyo, na vituo vyetu viliathirika na ukatwaji wa madeni ya umeme. Baadae watu wa *district* wakachukua jukumu wikalipa, lakini kilichofuata ilikuwa sasa wenye vituo waende zao Shirika la Umeme, wakachukuwe kile kidubwana kilichocholewa pale, wanakiita *cut out*. Wale sijui hawakufahamu wala hawakuwa na taarifa sielewi. Lakini ni wao tu lililowakuta kwamba hakukifuata kule, lakini kituoni kwao umeme ulikuwa umeshalipwa, kwa hivyo tukawafahamisha kwamba jamani nyinyi mnachotakiwa msisubiri hapa, wale wakishakukukatia hawakurudishiini wao, ni nyinyi wenyewe mnakifuata kule. kwa hivyo, ni matumaini yangu kwamba walikifuata, kwa sababu DMO wao walikuwepo pale na wao walikuwepo pale. hayo ndio maelekezo tuliyowapa.

Jengine lililojitokeza kwake ni tatizo la kuwaenzi wataalamu wetu. Hilo sote tunalikubali na tulilifanyia kazi vya kutosha, na tumelieleza vizuri hata hotuba ya waziri wetu alieleza hili vizuri. Kama mimi natakiwa nijalize hapa, nitasema kwamba tumelifuatilia, madaktari tumeanza kuwalipa na wengine tunaaza kujipanga kuwalipa, sio kwamba ni madaktari tu, kama walivyosema wajumbe wengine, watu wote pale tunafanyakazi kama *team work*. Lakini tunakwenda hatua kwa hatua.

Mimi nimefanyakazi miaka yote niliyofanya, lakini sikuwahi kupata *call allowances*. Sasa hivi kama sisi tumefanya jitihada na *call allowances* zinapatikana, tunapaswa kupewa *credit* jamani. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, watu wameanza kupata tena za tangu nyuma, tangu mwezi wa Oktoba wamepewa mpaka *April* na madeni yao yaliyobakia tutawalipa.

Kwa hivyo, tunawaenzi wao na wengine wote na yale yote ambayo yanastahiki, tunayafanyia kazi na tumeshakubaliana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rasi Utumishi wa Umma na Utawala Bora, watalipwa kuanzia sasa hivi na kuendelea. Kwa sababu tunajua kwamba hizo ni stahiki zetu. Kwa bahati mbaya mimi siko huko, *I wish* na mimi ningekuwepo nikazipata.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu pingamizi ya jengo la afya ya uzazi ya jengo la hospitali ya wagonjwa wa akili. Mhe. Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mhe. Mshimba kwamba ile sio hospitali ya kuzalia, sio *maternity ward*, wazazi hawatakwenda kuzaa kule. Lile ni jengo la utawala wa kitengo cha mama na mtoto. Kitengo kile cha mama na mtoto kitatengwa na ukuta wa kule *mental* hawatoingiliana, wao wana mlango wao na *mental* wana mlango wao. Kile ni kitengo shirikishi cha mama na mtoto, ambako kuna vitengo vinne.

Kwanza ni mama na mtoto, chanjo, maradhi ya watoto, IMCI pamoja na watoto ambao wameambukizwa ukimwi. Kwa hivyo, hapo nyuma kilikuwa kitengo kimoja kimoja, sasa vimeunganishwa ni lazima wapate jengo na tulikuwa tuna fedha kwa ajili ya kujengea. Sehemu ambayo tulikuwa tumeitafuta mwanzo, ilikuwa haiku katika maeneo yetu. Kwa hivyo, *mental* ni eneo letu na tuna uwezo wa kujenga. Kwa hivyo, tukaamua tukajenge pale ili fedha zisije zikapita muda wake. Lakini pale pako salama kwa sababu hakutakuwa na mama wala mtoto ni wafanyakazi wa Wizara ya Afya.

Nafikiri hayo ndio masuala ambayo nilikuwa napaswa kumjibu Mhe. Makame Mshimba. Hata hivyo, masuala yako ni mazuri. Mimi huwa napenda *challenge*, sipendi maswali laini laini. Natumai mtaridhika.

Mhe. Mjumbe mwengine ambaye nimepewa jukumu la kumjibu ni Mhe. mama Asha Bakar Makame. Kwa bahati mbaya aliniaga hatokuwepo, lakini salamu zake atazipata na *Hansard* zipo. Mhe. mama Asha Bakar Makame, alikuwa anazungumzia kuhusu madaktari wanaofanyakazi *private* kama ndio hao hao, lakini kama ndio hao hao mbona tabia zao zinakuwa tofauti wakiwa katika hospitali za kawaida na wakiwa kwenye *private*. Sasa nafikiri suala hili tumjibu hivi. Kwamba wafanyakazi wanaofanyakazi katika hospitali za binafsi wengi wao ndio hao hao wanaofanyakazi katika hospitali za serikali, huo ndio ukweli na wanakwenda kufanyakazi zile wanapokuwa na nafasi zao. Mtu labda alikuwa usiku, katoka mchana anakwenda kufanyakazi kule kama *part time*, mtu labda alikuwa na kazi ya mchana katoka anakwenda kule.

Lakini *nature* ya kazi ya hospitali ya Mnazi Mmoja na *private*, kwanza ni vitu tofauti. Mnazi Mmoja kwa siku unaweza ukatibu wagonjwa pale mpaka

ukaingia kizunguzungu, wagonjwa ni wengi na madaktari ni kidogo. Ndivyo tunavyozungumza, hiyo ndio changamoto yetu. Mtu akienda kule *private*, wagonjwa anaowakuta sio wengi hata hivyo. Kwa hivyo ubora wa huduma itakayopatikana pale ambapo pana wagonjwa wengi, na ubora wa huduma itakayopatikana pale mtu atakapokuwa na wagonjwa kidogo, bila shaka ni tofauti. Sikuambii tena ni *private* anapokea na pesa za ziada, bila shaka huduma itazidi. Lakini siwezi kusema kwamba kilichofanyika kule kilikuwa kibaya hapana. Ni wingi wa wagonjwa, kwa sababu wagonjwa wako pale na wanalazimika kwamba wakae na waondoke kwa wakati. Lakini kwenye *private* ana muda wake wa kuchukua anavyotaka yeye mwenyewe na mgonjwa anaridhika, maana kenda *private*. Kwa hivyo, ni hicho tu, lakini madaktari ni wale wale hakuna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jengine ambalo Mhe. mama Asha Bakar Makame alizungumzia kuhusu watoto kuondoshewa malipo ya huduma. Mimi nataka niseme hivi Wizara ya Afya inafanya mambo kwa mipango na tunatakiwa tujipange. Tukisema tuyachukuwe yote tuyabadilishe, mwisho tutajikuta kwamba hatuna tutakachoweza kukifanya. Bajeti zetu ndio hizo mnazona, nyinyi wenyewe mnazilalamikia seuze sisi. Watoto tunawapenda kama mama zao, na baba zao pia tunawapenda na tunapenda kwamba watoto nao pia wapate huduma zinazostahiki. Kuna baadhi ya dawa tunajitahidi watoto wanapata, lakini kuna vitu ambavyo viliwekwa kuchangia, vitu hivyo havichagui mtoto wala mtu mzima. Tukipima mkojo katika hospitali ya Mnazi Mmoja, hicho kimekubalika kichangiwe. Kwa hivyo, mtoto atachangia na mtu mzima atachangia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa dawa tunataka kuhakikisha kwamba watoto wanapata dawa, kwa sababu pesa za dawa zimeongezwa na utaratibu wa dawa unaombwa na wale wanaotoa huduma kwa yale mahitajio yao. Kwa hivyo, kama wanatibu watoto hamsini, basi wataomba dawa za watoto hamsini, labda huko wanakozinunua ziwe hazipatikani. Kwa hivyo, hayo mengine mimi nafikiri hili ni ombi jipya na kwa mujibu wa wachangiaji, itabidi tuchangie mpaka hapo tutakapojikusanya na kupata uwezo, tuombe tupate mafuta, tukipata mafuta tutakuwa na mapesa mengi na tutafanya viwe bure. Lakini kwa sasa hivi kuna vitu ambavyo vimekubalika vichangiwe, kwa hivyo hapo tutafanya. Lakini tujuwe kwamba katika watu ambao hawatakiwi nao kulipa watoto nao wamo, hivyo tutajitahidi na ikifika siku hiyo tutafanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya suala hilo, nimepewa ruhusa ya kujibu swali jengine la Mhe. mama Asha Abdu Haji, yeye alizungumzia sana suala la Hospitali ya Vitongoji kwamba iko karibu na Chake Chake na hospitali ile iko pale, lakini hospitali hali yake ni ngumu kidogo, ukilinganisha na hospitali

nyengine. Mimi nakubaliana na Mhe. mama Asha Abdu Haji, aliyoyasema ni kweli kuna upungufu wa wafanyakazi, kama ulivyo upungufu wa wafanyakazi katika hospitali nyengine. Wafanyakazi wanaokuja pale mara nyingi wanapangiwa ratiba kutoka Chake Chake.

Kwa mfano mtu wa *X-Ray* anakuja pale mara mbili kwa wiki, hatuna mtu wa kumuweka pale wa kudumu. Ukija kwa wafanyakazi, pale katika kituo ambacho kina wafanyakazi wengi wa kujitolea ni Vitongoji, pana *Red Cross* wengi tu ambao wanaingi ili kujaribu kuondosha hilo tatizo liliopo pale, ili kusaidia na wafanyakazi kwa yale ambayo wao wanayaweza. Kwa vile Vitongoji imo katika hospitali ambazo zinatakiwa zipandishwe daraja kama zilivyo hospitali nyengine. Tumesema kwamba tuanze mambo kwa utaratibu, kwa vile Micheweni iko mbali huku, kwa hivyo tunaanza kule. Kwa vile Kaskazini ndio iliokuwa kama ni ya Mkoa basi tunaanza kule. Hospitali ya Makunduchi tulikuta imeshaanzwa na sisi tumeendelea kuimalizia. Lakini Chake Chake na Vitongoji ziko karibu, hivyo watu wakikosa pale ni karibu kwenda kule, hata kilomita 10 hazifiki, lakini baadae na Vitongoji pia itapandishwa daraja na itafikia kama hizo hospitali nyengine kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la likizo ambalo ni katika mambo ambayo tumeyazungumza ambao Wizara ya Afya kwetu ilikuwa ni ndoto, lakini hata hivyo, sasa hivi imefikia wakati baada ya kuliona na baada ya Mhe. Rais kusisitiza jamani walipeni haki zao, likizo ni haki yao. Wenzetu Pemba walijipanga vizuri na walianza zamani kidogo. Unguja tumeanza safari hii na kama unataka ushahidi, karudi kwa huyo aliyekuambia, tumeweka utaratibu kwa watu wote walioanza likizo kuanzia mwezi wa Julai. Tena nika-*insist* jamani asijetoka mtu wa Juni mwaka huu akajakupata kabla wa Julai mwaka jana hajapata. Kwa hivyo, kama *list* ilivyoletwa tumeshaanza kuwalipa, tumeanza kuwalipa watu 50 na waliobakia tutawalipa miezi miwili ijayo. Baada ya hapo likizo itaendelea kwa kila atakaye kwenda likizo atapata pesa yake kwa wakati, hilo limeshatatuka.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe mwengine ambaye nimepewa jukumu la kumjibu ni Mhe. Saleh Nassor Juma. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe alizungumzia mambo mengi, kati ya hayo alizungumzia suala la Hospitali ya Chake Chake na hasa idara ya tiba, alisema ni nzuri kwa nje. Tena akatoa mfano mzuri tu, kuwa jenea nje linapambwa vizuri, lakini ukiingia ndani kilichomo hakipendezi kwa sababu ni kifo. Ni kweli hospitali iko hivyo, kwa sababu inakuja, sikatai. Lakini kilichotokea pale waliogongomelea lile bati, siwajui kina nani, toba. Isipokuwa mabati yenyewe ni yale ya Kichina ambayo yana sehemu maalum ya kugongomelea misumari, hawakugongomelea humo na ni hospitali nzima iko hivyo. Sasa kwenye ile

michirizi ambapo mabati yamegongomelewa ndimo mnamopita maji yakakaa, hivyo yanapenya kwenye zile tundu, hivyo kuiziba sio kazi ndogo. Hata hivyo, tutaifanya kazi ya kuhakikisha kwamba tunayaziba matundu na tutatizama gharama zilivyo ili tuweze kuziba. Kuna sehemu nyengine walijaribu kuziba sio kama hawakufanya, lakini ni vitu ambavyo vinaganduka na baadae unakuta kwamba maji yanapenya.

Vile vile Mhe. Mjumbe amesema kuna zana kongwe maabara. Mimi nataka nimuulize Mhe. Saleh hivi kapita huko hospitali karibuni, maana pale ICUP imejenga maabara ya kisasa, kuna kila kitu cha kisasa. Labda alipita zamani, hivyo namuomba apite akatizame halafu aje anihakikishie hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kitu changine kilichokuwa kikifanywa pale ni *night call allowance*, yeye anasema zinahesabiwa siku 10 tu. Unajua linapokuwepo tatizo watu huwa wanajaribu kutafuta njia tutoke vipi. Wenzetu wa Pemba kwa kuwa wafanyakazi ni kidogo, basi wanafanyakazi kutwa kucha. Mtu aliyeko pale hawakuwa wana *on call* na pesa wa *on call allowance* hazikuwepo, uongozi wa pale ukaamua kwamba kila mtu akija hajaja, tutatenga shilingi 20,000 katika fedha tulizonazo, ili tuwape *on call allowance*. Kwa hivyo, ikawa kimewekwa kile kitu kama *fixed* kwao. Hata katika haya mambo ya sasa hivi ya kupanga *on call allowance*, ambayo sasa hivi kwa siku daktari atapewa shilingi 20,000 na daktari msaidizi shilingi 15,000. wao waliweka *fixed* kwamba angalau ukitoka pale baada ya mwisho wa mwezi ule hata ukifanya *call 100*, angalau uwe nacho kidogo cha kukupa, ndivyo ilivyotokea huko, kujaribu angalau kuwafanya wale watu wajihisi hivyo. Lakini sasa hivi kitakachoendelea ni kwamba siku zao watakazopangiwa watalipwa na walishalipwa katika hao madaktari wa Pemba walishalipwa kama tulivyowalipa wenzao wa Unguja.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, alilochangia Mhe. Mjumbe ni kwamba hapa panatakiwa pawe na *CT Scan*. Mimi nakubaliana nay eye kwa kitu kimoja. Kwa utaratibu *CT scan* ni vitu ambavyo vinawekwa katika *level* ya juu. Ukiangalia Tanzania Bara tu *CT scan* ziko katika hospitali za resel. Kama Bugando, KCMC, Muhimbili na hospitali za *private* kwa zile *private* kubwa zenye uwezo. Kama Hindu Mandal, Agakhan, Regent huko ndio ziliko. Sasa tulianza kuweka *CT scan* Mnazi Mmoja hospitali kwa sababu hapa kwetu Mnazi Mmoja ndio tulikuwa tunai-*focus* iwe hospitali ya rufaa, kwa hiyo tumeweka pale. Kile chombo kwanza ni ghali, matengenezo yake sio ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwa jambo moja kwamba nchi yetu imegawika katika visiwa, kwa hivyo ukisema unaweka *CT Scan* Mnazi Mmoja tu, mtu aliyeko Pemba asafiri kuja huku, kwa kweli ni mtihani. Kwa hivyo, mimi nakubaliana naye, tumezungumza tukasema sasa

sikilizeni tupange tupanguwe, lakini ifike siku angalau na Pemba nayo iwe na *CT Scan* yake, hivyo tutajitahidi ili iweze kupatikana. Siwezi kumwambia ni lini, lakini iko siku hilo litakuwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Mjumbe alizungumza suala jengine linalohusu magodoro ambayo yamepelekwa hospitali ya Chake Chake pamoja na shuka. Hizi zilitolewa na Mbunge mstaafu pale. Lakini magodoro yale sio magodoro ya kihospitali, ni magodoro ya kawaida ambayo yana kitambaa chepesi. Kwa hivyo, ushauri uliotolewa pale kwamba jamani hili godoro tukiliweka hapa kwenye kitanda, kwa hali hii lilio mgonjwa ndio mgonjwa baada ya siku chache tu yataharibika, tusiyaweke kwanza, tutafute mifuko ambayo tutaitia ya plastiki ili yasije yakachafuka. Kwa hivyo, wakati magodoro yalipoletwa na bajeti tulionayo ni ya mwaka jana, hayamo hayo kwenye matumizi. Kwa hivyo, sasa bajeti ya mwaka huu imepangwa kwa ajili ya kununua hivyo vitambaa vya plastiki ili kuyashonea yale magodoro. Kwa hivyo kama bajeti itapita na nafikiri mtaipitisha basi tutayashonea mifuko tuyatie na kuweza kulazia wagonjwa, lakini kwa hali ile iliyo baada ya muda mchache tu yataharibika, ndio maana hayajatumika kwa sababu ya huo utaratibu tulio usema.

Vile vile Mhe. Mjumbe alizungumzia suala la dereva wa Mdhadini kupewa shilingi 80,000, lakini watu wenye dhamana hawapewi. Ndio katika mtiririko huo huo ninaosema kwamba huyu dereva yeye kwanza utaratibu wao uko tofauti. Nafikiri umeelezwa hapa kuwa madereva wamelipwa na masekretari wamelipwa, aliingia kwa utaratibu huo, kwa sababu Mdhadini wa afya ndiye kiongozi mkuu wa pale, kwa hiyo dereva wake alilipwa kwa hivyo. Lakini posho la dhamana ni moja katika maposho ambayo tunayafanyia kazi na hilo tumeliona. Katika posho ambazo tunazitengeneza, posho la dhamana na sio kwa hao tu ni kwa Unguja na Pemba, baadae zitapatikana. Lakini mambo kidogo kidogo.

Pia alizungumzia suala la sera ya afya na mazingira. Amejaribu kuvinukuu, MKUHUMI na vyenginevyo. Nakubaliana naye, kwa sababu mazingira yakiharibika kweli *cancer* ya ngozi, *ozone layer* ikiharibika yapo nakubaliana nayo. Lakini hili sio suala la moja kwa moja, tukizungumza suala la MKUHUMI, ukitizama kwa upande wa afya hili haturuhusu sana. Lakini madhara yake yatakuja kujitokeza yataishia kwetu, tunakubaliana nalo kwa hivyo, tutajitahidi na wenzetu wajitahidi kwa upande wao. Lakini adhari itakayojitokeza hiyo ndio itakuja kwa upande wetu sisi. Kwa hivyo, wengine wakitengeza mazingira ikiwa hawatoyaharibu, ina maana kwamba *ozone layer* itabaki vile vile, hata hizi *cancer* itapungua.

Kwa hivyo, tutajipanga kwa sababu kitengo cha *cancer* katika hospitali ya rufaaa kitafunguliwa, hivyo tunategemea kwamba tutaweza kulikabili iwezekanavyo. Lakini tujitahidini tusiharibu mazingira, kwa sababu *cancer* sio kitu chepesi, hivyo tusijinufaishe sisi hapa leo kwa kujikimu tukawasababishia wengine au pamoja na sisi wenyewe kuja kuishia kwenye matatizo. Kwa hivyo, hilo nakubaliana nalo.

Vile vile katika vitu ambavyo amevifurahia ni Redio ya Afya FM. Katika kazi moja kuwba ambayo tumeambiwa tutowe ni taaluma ya afya. Nataka niwaambieni kama kuna bajeti kubwa iliyowahikwisha kutengwa katika wizara ya afya, maisha yote niliyokaa pale kwa ajili ya afya, basi ni mwaka huu ndio kitengo ambacho kimepewa umuhimu wa kwanza. Ni pesa nyingi mno zimetengwa kwa ajili hii.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, redio hiyo itafanyakazi vizuri na mengine yote yanayostahiki yatafanywa. Lakini sio hivyo tu, sasa hivi kuna *focal person* kila *district* ambayo ni *head officer* ambaye atahakikisha kutoa elimu ya afya katika wilaya yake. Kwa hivyo, tunategemea kwamba baada ya muda mfupi mambo yatabadilika kuhusu elimu ya afya.

Pia aliulizia hospitali ya Vitongoji inajengwa lini? Nafikiri hilo nimeshalieleza kwa Mhe. mama Asha Bakar Makame. Kwa hivyo, jawabu langu litabaki lile lile kwake pia.

Mhe. Mwenyekiti, kazi nyengine niliyopewa nimeambiwa nimjibu Mhe. mama Mwanajuma Faki Mdachi. Alizungumza na akaeleza *cancer* zake kuhusu malaria na mambo mengine, akatupa na shukrani na sisi tunamshukuru. Lakini kuna suala la maradhi ya moyo, kisukari na akasema kifua kikuu na ukoma. Kama malaria tumeweza kusema kwamba labda tuna malaria iko chini ya moja. Kwa nini sasa kwa haya maradhi mengine nayo hatuwezi kusema kwa utaratibu huo, ili tukajielewa kuwa hali yetu iko vipi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri ningemjibu hivi kwamba suala la moyo na kisukari, kitengo kimeshafunguliwa cha maradhi ambayo sio ya kuambukiza ni kipya. Tunachojaribu kufanya tulipata taafiti za mwanzo, ili kuelewa labda tatizo lina ukubwa wa kiasi gani ili tuone jinsi gani tutakavyoweza kujipanga. Kwa vile tutakuwa tunalifanyia kazi katika programu maalum, tutaweza kujua watu wangapi kwa mwaka tumewapata. Hivyo hao ndio watakaotuwezesha kupata hizo takwimu na tutawatibu wangapi, labda wangapi watakuwa wamepata nafuu, hapo tutaweza kuchanganua. Lakini kwa sasa hivi, huyu anatibiwa huku, kule anatibiwa kule kwa kweli takwimu kama hizo tutashindwa kuwa nazo kwa upande huo.

Kwenye upande wa Kifua Kikuu na Ukoma hilo linahitaji angalau tuwe na zile za msingi tuwe nazo. Hiyo ni *project ya prevalence survey* ambayo ni kubwa kwa ulimwenguni, huwa kwa ulimwenguni wala Afrika haijawahi kufanyika. Kitu ambacho ninachoweza kukwambia kwamba Kifua Kikuu na Ukoma ni maradhi ya muda mrefu, unaweza ukaambukizwa leo ukaugua una miaka 70, kwa sababu ya kinga yako ikiwa itashuka kwa zee au kwa lolote lile. Hatuwezi tukasema kwamba huyu hatougua au huyu ataugua.

Ukitizama karibu sote tumeambukizwa. Kwa sababu wale wamoambukiza wamo mote, lakini nani anaugua ni yule ambaye kinga yake iko chini. Maradhi kama hayo ni tofauti na malaria ambayo unawapima watu wakati huo huo, unatibu wakati huo huo, unachukua hatua unauwa mbu, unawapa dawa, una – *spray* katika majumba. Kwa upande ule kule inawezekana lakini kwa haya mama angu inakuwa ngumu. Haya ya sukari tutajitahidi lakini haya mengine kwa kitaalamu si kitu cha hivyo. Nilikuwa naomba uangalie hivyo.

Suala jengine lililokuja ni upasuaji ukasema kwamba katika kitengo cha upasuaji kina madaktari wachache. Nafikiri tumezungumza hapa kwamba jamani kama kuna kitu kinatupa shida Wizara ya Afya ni *human resources* na naomba wale wote ambao wanalizungumzia suala la upungufu wa wafanyakazi wa afya watufahamu. Sio kwamba sisi tunataka iwe hivyo, tunataka, tunajitahidi, tunasomesha na tutapenda kufanya kila liwezekanalo wanzetu warudi tufanye kazi pamoja.

Kitengo cha upasuaji hivi sasa kina madaktari, huyo Dokta Maliki anafanya kazi, dokta Yunus ndio *incharge*, kuna Mchina pale, kuna Mquba pale, kuna madaktari kama watatu wapo wakati wote pale. Dokta Maliki yeye anakwenda kwa baadhi ya wakati.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa hapa ni suala la maabara, kufanya kazi asubuhi lakini ukenda jioni halifanyi kazi. Suala la maabara katika hospitali zote kwa kawaida kuna kazi zinazofanywa za *routine* na kazi ambazo zinafanywa kwa dharura. Kazi za *routine* kwa kawaida huwa zinafanywa kuanzia asubuhi mpaka saa 8, ndipo wanapokusanya, kuna nyengine zinafanywa hapo hapo nyengine zinachukua muda baadaye. Baada ya hapo wao waliobakia pale jioni ndio wanafanya *analysis* ya zile walizozikusanya asubuhi. Ukenda usiku anabakia mtu mmoja ambaye ni wa dharura kwa hiyo ukenda na malaria, ukitaka kuchunguzwa mkojo au akitakiwa mgonjwa kutiwa damu huyo ndio anakuwepo usiku. Huo ndio utaratibu wa kawaida katika maabara zote, watu hawafanyi kazi saa 24 kwa *routine* wanafaya kazi saa 24 kwa dharura.

Pia alizungumzia kuhusu suala la majengo ya Abdalla Mzee Hospitali anasema yamezeeka. Tunakubaliana naye, ndio maana tunaambiwa kwamba Wachina wanakuja kuyajenga majengo yale upya na Hospitali itakuwa mpya itafanyiwa ukarabati na majengo mengine mapya yataongezewa. Nafikiri *project* hiyo ikiwa itakamilika mambo yatakuwa ni mazuri.

Halafu mwengine ni Mhe. Mohammed Mbwana, namjibu Mheshimiwa huyu kwanza nakubali kwa pongezi alizotupa tunamshukuru kwamba angalau anaona juhudi zetu. Lakini hakuna kitu kinachomuudhi kama wanawake kuzalishwa na wanaume. Hilo halimpendezi mtu yoyote, si weye kuna wengi pia wamesema. Lakini bahati mbaya hapa kwetu Zanzibar wale madaktari waliochukua mambo ya wanawake wote ni wanaume. Kuchukua *specialties* ni hiyari ya daktari mwenyewe hatuwezi tukamlazimisha mtu ukamwambia chukua hiki.

Mheshimiwa mimi katika wanaweke niliyeambiwa na nakumbuka nimechelewa kwenda kusoma digrii ya pili kwa sababu kiongozi aliyekuwepo aliniambia nikachukua ambo ya uzazi. Mimi hayo sikuyapenda, ingawa nimefanya kazi katika wodi ya Wazazi sikatai, lakini si kitu ambacho nilikipenda. Kuna kingene ambacho nilikipenda zaidi. Wakati nasoma hicho kitu ambacho nakisoma hakikuwa kipa umbele. Kwa hivyo waliyokwenda na vipaumbe walisoma na mimi nilibaki nikafanya kazi mpaka ulipofika wakati wa kwamba lile ninalolitaka kulisoma ni kipa umbele na mimi nikapewa nafasi nikenda nikasoma kwa sababu wakati ule ilikuwa ni kipaumbele cha Wizara ya Afya.

Kwa hivyo wanaume tulionao pale madaktari ndio walioamua kuchukua udaktari. Wanawake tulikuwa tunao wawili, mmoja kapata kazi AU, hatuwezi tukamzuia mtu aliyepata nafasi asiende. AU ni chombo chetu na yeye kapata nafasi, tu akifanya vizuri akipata nafasi muachie tena usikae ukamng'ania ukamwambia kaa hapa, na kwa maana hatokaa. Wa pili wa kike kaondoka kwa sababu mumewe alichokisomea hapa Unguja hakipo. Sisi hatuchimbi madini na mumewe kasomea mambo hayo kwa hiyo yupo Bara, kaondoka kamfuata mumewe, hatuwezi tukamzuia asende. Waliobakia ni wanaume dokta Zakaria, dokta Juma, dokta Hassan, tufanye vipi. Hatuna jinsi hivyo. Nafikiri mmetufahamu.

Baada ya kusema hayo pia wamesema kwamba hakuna wafanyakazi hili nafikiri tumelizungumza lakini tumezungumzia afya ya wafanyakazi. Akasema kwamba wafanyakazi wa afya wanapimwa pale tu wanapotaka kuingia kazini. Lakini baada ya hapo tunawaachia mpaka wanaugua. Mimi nilikuwana nataka niseme kama kwenye nchi zilizoendelea mfanyakazi yoyote katika kitengo chochote wanafanyiwa uchunguzi kila mwaka. Sisi

tuliosoma nje tulikuwa tunapimwa kila mwaka, huo ni utaratibu. Sasa ni sisi tu kujiwekea kwa sababu maradhi hayapatikani tu pale katika Wizara ya Afya kuna maradhi mengi yanapatikana katika kazi nyengine ambazo zinawaza zikasababisha maradhi. Wafanyakazi na wao pia wanahitaji kuchunguzwa ni suala la utamaduni. Kupima Afya ni jambo la khiyari lakini pia linahitaji pesa. Afya pale hatupimi bure, kama kuna wizara itataka tuwapimie sisi tutashukuru maana tutapata *revenue* tutawapima wafanyakazi wetu.

Mhe. Naibu Spika, vitengo vile ambavyo vina maradhi ya kuambukiza kama vile Kifua Kikuu, wale wanapimwa kila mwaka. Kwa sababu ni lazima kufanyiwa vile ili kuhakikisha kwamba wao wapo salama na kwa kuwa wapo katika sehemu ni hataridhi. Ndio maana watu wanasema tupeni *risk allowance* mtu kama unamuhudumia mgonjwa wa kifua kikuu, wanaopata hawafanyi kazi hospitali na wanapata, seuze mtu kila siku anakukoholea. Kwa hivyo wale kupewa *risk allowance* ni haki yetu wafanyakazi wa Wizara ya Afya kwa sababu tunakaa na watu ambao wako hatarishi katika maisha yetu.

Mhe. Naibu Spika, kupima ikiwezekana watu wote wapimwe na sio wafanyakazi tu jamani, watu wote wanatakiwa kupimwa afya zao kila mwaka. Maradhi yakigundulika mapema ni vivuzi tuisubiri mpaka tukaugua. Naomba tupime afya zetu, Wawakilishi nakukaribisheni. Kila ukiingia kila mwaka twendeni tukapime, nitaandaa huo mpango ili tucheki afya zetu maana nyie ndio mliokaribu yangu ninaokuwezeni.

Mhe. Naibu Spika, nililokabidhiwa limebakia moja au mawili. Hapa nimepewa jukumu la kumjibu Mama Shawana, dada angau, mama angu kama yeye alivyosema. Huyu alikuwepo Wizara ya Afya na anayajua vizuri mambo ya Wizara ya Afya. Alichokisema ni cha kweli, aliyoyaona ni ya kweli, na anachotwambia kwa sababu yeye amekipitia. Akisungumza suala la kuwajibika, akizungumza suala la fedha chache ni kweli sote tunaliona. Lakini uwajibikaji wa wafanyakazi wetu tunaambiwa tuliangalie.

Mhe. Naibu Spika, sasa nasema hivi Wafanyakazi wa Wizara ya Afya nataka mnisikilize sisi tunatendewa yale yote na tunajitahidi kuhakikisha kwamba haki zetu tunapata, lakini waki zinakwenda na wajibu. Atakae kuwa kapata haki zote halafu hakuwajibika hakuja kazini kwa wakati, hakuwa msikivu kama alivyotakiwa, sijui kamnyonyoa mtu hakumbakisha kwa sababu eti hakuzaa, wananchi tutawapa fursa na namba zetu ya simu tutaziweka pale watwambie nani na tunawaruhusu waje kwa sababu hatua itabidi zichukuliwe. Tuwe kama kweli wafanyakazi wa afya.

Mtu anapokuja na mtu wake mgojwa mfikirie yupo katika *depression* ya kiasi gani. Au mgonjwa mwenyewe halafu badili ya kumnasihi au kumbeba vizuri, leo unaanza kumfanyia mambo siyo si vuzuri nakuaseni naomba tuyaache. Kitu changine ambacho hapa Mama Shawana alichotuomba mwisho wake akasema kwamba ana vituo vyake vitatu kwa kweli vituo vyote vilivyokuwa vimeshaanza kujengwa Unguja na Pemba tumepewa amri na Rais hivyo tuvimalize na tutavimaliza, isipokuwa sasa tusijenge vyengine mpaka tukubaliane. Tukiona kwamba panastahiki kujengwa tutajenga. Kwa sababu kuna sehemu kweli tutaziangalia kama kweli zinastahiki kujenga tutatoa ruhusa, lakini kwanza tuacheni tumalize ambavyo tumeshavijenga.

Aliyebakia ni Mhe. Salim Hamad yeye alizungumzia kuhusu malaria waliyopoa ni asilimia 85. Hilo ndilo lilikuwa lengo la mwanzo, asilimia 85 ilitimia. Sasa hivi asilimia 15 watapelewa waliobakia kwasababu vifaa vipo isipokuwa kunafanywa utaratibu ili waweze kupewa waliobaki. Pia alishauri kwamba shughuli nyengine kama maji, maziwa tukatiwe dawa kwa sababu huko ndiko kwenye matatizo.

Tabia ya mbu inabadilika kulingana na utaratibu vipi unaotumika kwa kuwa *control* mbu na kuya *control* malaria. Kama zamani walikuwa wakila ndani sasa hivi wanaona nje watahama watahamia nje, inategemea jinsi gani unavyowashughulikia. Yanayofanyika huwa yanafanyika baada ya kufanya utafiti na kufuatilia mwenendo huo na ndivyo tunavyochukua hatua. Naomba mtuelewe kwa sababu hayo ni mambo ya kitaalamu.

Pia alizungumzia kuhusu afya Bandarini hasa kuhusu homa ya manjano. Hilo nataka niwatoe wasi wasi kwa wale ambao wanatoka nchi ambazo hazina homa ya manjano. Kama mtu anapotoka hakuna hilo tatizo na tunahakikisha kwamba katoka moja kwa moja kwao kafika kwetu bila ya kupitia popote huyo kwa kweli hatuna haki ya kumdai cheti. Lakini kama katoka akapita kwenye nchi nyengine ambapo pale pana tatizo lile, hata kama kule alikotoka hakuna tatizo huyo inabidi na yeye achanja kwa sababu kapitia katika nchi ambayo kuna lile tatizo.

Lakini kwa Tanzania yetu hii likiwepo tatizo Unguja au likikuwepo Bara kwa hiyo utaratibu unachukuliwa kama ni nchi. Mtanzania anayetoka Bara akija hapa kwa sababu hapa kwetu tuna uhakika hatuna sababu ya kuwapima eti kwa sababu kwao ni kukubwa kwetu ni kudogo. Hili ni swala la kitaalamu nchi yetu huwa inalichukulia kama nchi na sio Unguja, sio Pemba, sio Tanzania Bara, hivyo ndivyo ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, hayo ndiyo niliyokabidhiwa ili niweze kuyajibu. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na nawashukuru Wajumbe kwa kunisikiliza, ahsanteni.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru kwa kuniruhusu ili nisaidie baada ya Mheshimiwa wangu hodari kuliko mimi kufanya uchambuzi kwa mambo kadhaa wa kadhaa yanayohusu hoja zilizowasilishwa na Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, nimejipangia nifanye kazi kama tatu au nne. Kwanza ni kuweka sawa juu ya hili dudu kubwa ili tunapokuja kupitisha vifungu sote tuwe pamoja. Naomba kila mmoja anazo hizo basi tufuatane ili niwaongoze mjitayarishe kwa kuja kupitisha vifungu. Kwenye hili dudu *vote* yetu siye ni Nam. 24 lakini kwa sababu ya masahihisho na baadhi ya makosa na ili tusiwababaishe wajumbe zile zilizosahihi tulizosahihishiwa na tulizozithibitisha pamoja na Kamati ya Mhe. Bi Amina ni hizi. Sasa naomba niwaongoze kuwaeleza ili mujiweke sawa.

Kwanza kuna karatasi ambayo ina vikurasa nadhani vitatu tu inayohusu makadirio imeandikwa “makadirio ya mapato yatakayokusanywa kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2011 ni jumla ya shilingi mia tisa na tisini na tano milioni na laki tano (995,500,000), hii ni baada ya kudirusiwa. Kwa hivyo hii ndio sahihi mtakapokuja kutupitishia mtupitishie hii.

Document ya pili ni lile kubwa kidogo nalo ni fungu la 24, nalo vile vile ukurasa wake wa juu umeandika “Makadirio ya Fedha zinazohitajika kwa mwaka unaoishia tarehe 30 June, 2013 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ni jumla ya bilioni kumi na nane, mia mbili na thalathini na nne milioni (18,234,000,000) ilikuwa imesahihishwa kwa hivyo hii ndio sahihi. Hii imeishia kikurasa kidugu cha mwisho kinachoeleza hivyo shilingi bilioni kumi na nane, mia mbili na thalathini na nne (18,234,000,000). Kwa hivyo yale masahihisho yote yaliyokuwemo humu yameshasahihishwa yamo humu. Kwa hivyo hii ndio sahihi tutakapokuja kupitisha vifungu.

Mhe. Naibu Spika, ya mwisho katika hizo hizo *documents* kuna *page* kule mwisho katika *documents* mbili hizo sasa hiyo ya tatu mliyopewa ina mambo ya maendeleo nayo ina vikurasa vitatu. Imeanzia Idara ya Mipango sera na utafiti Makusanyo halafu ikaendelea Miradi imeendelea mpaka mwisho ina bilioni ishirini na moja, mia tisa na thamanini na mbili milioni, mia mbili na tano elfu (21,982,205,000). Tukapokuja kukaa pale tutatumia hizi badala ya dudu hili. Lakini simzuii mjumbe kutizama hili kama aliweka alama zake kutaka kupiga buti.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hilo la pili nishukuru kwamba wachangiaji waliochangia ni wengi kidogo. Hii inanipa moyo kwamba kila mmoja anajua umuhimu wa afya. Mimi nilioweza kurikodi ni 43 inawezekana Waheshimiwa mmoja au wawili nikawa nimewasahau. Kwa sababu nililetewa karatasi nyengine za maandishi dakika ya mwisho nilijitahidi zote kuziweka kwenye kumbukumbu. Kwanza naomba nitambue michango ya wawakilishi wafuatao:-

- 1) Mhe. Amina Iddi Mabrouk
- 2) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
- 3) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
- 4) Mhe. Mohammed Said Mohammed
- 5) Mhe. Abdalla Mohammed Ali
- 6) Mhe. Asha Bakari Makame
- 7) Mhe. Omar Ali Shehe
- 8) Mhe. Nassor Salim Ali
- 9) Mhe. Marina Joel Thomas
- 10) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
- 11) Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa
- 12) Mhe. Ali Salim Haji
- 13) Mhe. Abdalla Juma Abdalla
- 14) Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)
- 15) Mhe. Asha Abdi Haji
- 16) Mhe. Rashid Seif Suleiman
- 17) Mhe. Abdi Mosi Kombo
- 18) Mhe. Farida Amour Mohammed
- 19) Mhe. Thuwaibah Edington Kisasi
- 20) Mhe. Hamza Hassan Juma

- 21) Mhe. Mgeni Hassan Juma
- 22) Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
- 23) Mhe. Panya Ali Abdalla
- 24) Mhe. Asha Abdu Haji
- 25) Mhe. Viwe Khamis Abdalla
- 26) Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk
- 27) Mhe. Ashura Sharif Ali
- 28) Mhe. Hassan Hamad Omar
- 29) Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi
- 30) Mhe. Subeit Khamis Faki
- 31) Mhe. Shawana Bukhet Hassan
- 32) Mhe. Salim Abdalla Hamad
- 33) Mhe. Rufai Said Rufai

Sina hakika wengine sikuyaona majina pengine nitakapoanza kujibu yatajitokeza. Baada ya kutambua michango yao hiyo kuna sehemu kubwa ya wale waliohoji mambo nimesaidiwa na Naibu Waziri wangu na namshukuru kwa hilo. Wale waliobaki nitajaribu kujibu mimi katika kunusuru muda pengine sitojibu kila kitu kwa sababu vyengine vimejirudia mumo kwa mumo.

Mhe. Naibu Spika, nianze na Mhe. Jaku Hashim Ayoub yeye ameuliza na amesema mambo mengi. Kwanza ametushukuru na sisi tunamshukuru. Ametupongeza na kutupa sifa, pale penye wajibu tunapongezwa na pale tulipoharibu tunakatazwa au tunagombwa, tunashukuru. Lakini suala kubwa alilosema Mhe. Jaku ni suala la uwajibikaji na uchafu na ubovu wa vifaa.

Mhe. Naibu Spika, uchafu au usafi ni tabia ya mtu. Lakini mara nyengine ni mazingira yanayolazimisha usiwajibike kufanya yale mengine. Kwa hivyo Hospitali ya Mnazi Mmoja kweli sio safi kama inavyosemwa. Lakini tunahitaji vile vile kuthamini juhudi tulivyofanya angalau ikawa hali hiyo iliyo sasa. Tulivyoikuta na ilivyo sasa hivi ni tofauti. Kuna mambo mengi ya kufanywa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nieleze tu kwamba mwenyewe nilishiriki katika kutaka kuona hospitali ile iko safi. Nikamuomba Mkurugenzi anipe makisio ambayo hospitali ingekuwa safi kwa kila mwezi akaniletea makisio ni milioni 14 kwa kila mwezi. Nikayachambua makisio yale nikapata milioni kumi kwa kila mwezi. Nilipochungulia karatasi ya bajeti ya Mnazi Mmoja ya usafi kuna milioni 14 kwa mwaka. Hata uwe mzimu wa kule kwetu Mwana wa Mwana, basi ndio mashetani basi hawawezi kusafisha Hospitali ile kwa pesa hizo.

Juhudi gani tulizofanya mimi na mwenzangu Naibu Waziri wa Afya na wengine. Tukatafuta wasamaria wema, tukawambia hakuna mtu anayetaka kutoa sadakatu rizki, akatokea mmoja anayetaka kutoa sadakatu rizki akatupa pesa. Kila mwezi milioni 10 nikimkabidhi Mkurugenzi kwa usafi na kila mwezi nikimwambia aniletee *retun* wakati ule watu walikuwa wakisema “alaah ukenda Hospitali Mnazi Mmoja kunanukia *detol* bwana, babu Juma anajitahidi” lakini ilikuwa kwa msaada ule, ulipokwisha mwaka sina uwezo tena na msamaria mwengine hajatokea, mambo yakaanza kurudi.

Sasa kinachofurahisha katika hizi juhudi nilizokwambieni zimerekebishwa kifungu cha usafi kina milioni 89 kwa mwaka Mnazi Mmoja. Angalau kwa wastani 89 ukigawa kwa 12, $12 \times 8 = 96$, $21 \times 7 = 84$ kwa hivyo angalau wataweza kujikimu kwa hilo. Sasa wale wanaotupenda basi kama wanazo watuletee.

Lakini vile vile kuna tatizo la wale wanaosafisha wenyewe ndio maana nikasema mara nyengine usafi ni tabia lakini mengine hata ukitaka uwe safi. Hospitali ile ni kubwa bwana, makisio ya kuendesha hospitali kama taasisi, mana nyinyi mnakwenda kama hospitali lakini ile ni *institution* inahitaji *three billions* ili iendeshwe iwe kama taasisi na tunataka kumpa mwenyewe ile tunamtayarishia sheria. Wale wazee ma-*orderly* wengi wao ni watu wazima na uwezo wao unazidi kupungua na wamekuwa wachache. Tunawasiliana na Wizara ya Utumishi watusaidie tupate watu wengine kuajiri, lakini ndio kama mnavyojua huwezi kupewa wewe tu na kilimo wanataka na elimu wanataka na wengine wanataka.

Kwa hivyo, ninachoomba suala la uchafu wamezungumza watu wengi tunakubali tunanuka, lakini angalau uso tunanawa. Kwa hivyo, tunaomba hilo tulifahamu hivyo nisichukue muda mrefu.

Lakini uchakavu wa majengo hospitali ile jamani ilipojengwa mimi na nyinyi hatujazaliwa na ilijengwa ile wakati *population* ya Zanzibar ni laki tatu. Sasa waliokuwa wanakwenda pale mimi nilikwenda pale niliugua *tetanus* nilikuwa mdogo, lakini ilikuwa kila mmoja na kitanda chake, kila mmoja na *nurse* wake, sasa wingi wa wanaotaka kuhudumiwa na *frequency* ya vile vyoo ni kubwa kuliko uwezo wake. Kwa hivyo, ile hospitali yenyewe inataka kwa kizungu tunasema *over whole* Mhe. Mtando anaweza kujua inataka makope

nje ndani ile, inahitaji mabadiliko makubwa, zinahitajika pesa nyingi tutafanya kidogo kidogo.

Lakini Mhe. Jaku Hashim pamoja na hayo suala jengine ambalo ni muhimu alilosema ni kwamba labda kulikuwa na usiri wa matumizi ya zile pesa za michango na zile za *fast track* na wengine wengi wamesema hivyo.

Uchangishaji wa huduma za hospitali ulianza muda mrefu tangu wakati wa Mhe. Salmin Amour Juma na wakati huo wote mpaka tumekuja sisi kina Juma Duni ilikuwa wanachokusanya wanatumia hawapeleki Serikalini. Ni Baraza hili mwaka jana ndipo liliposema aa, zipelekwe Serikalini. Kwa hivyo muda wote huo ilikuwa inaishia kule kule wanatumia wao.

Mwaka jana tumeanza tukapeleka na hiyo mwaka jana yenyewe tulichelewa kwa sababu baada ya kumaliza bajeti hapa mpaka nadhani mwezi wa Novemba ndio tukaanza kupeleka. Hakuna usiri na nadhani hata Mhe. Mtando kule swali lake alisema anataka hesabu za miaka mitatu za *fast track* zipo hizi hapa bwana na kama unataka kumleta *auditor* vile vile mlete kule ndani aje aangalie ziko kila kiti na rikodi. Kwa hivyo, hilo tunataka kusema kwamba hakukuwa na usiri wala hakukuwa na kinachofichwa zote hapa zipo Waheshimiwa kwa kila kifungu kwa kila *section*, wazazi wakikusanya Julai ni kiasi gani, Agosti kiasi gani na kadhalika.

Mhe. Jaku Hashim masuala mengine yalikuwa kwa jumla ni yale yale ya *X-ray* mbovu imetengenezwa na kuharibika vyombo hivi ni sawa kwa sababu kila mara vinatumika. Alipokwenda kwenye skena kuna madudu yale yamekusanywa, tutayaondoa yale yote Mheshimiwa na tushakubaliana na vile vitanda vibovu kwenye barabara vyote vitaondolewa. Kuna watu wengine mle ndani gari zao wamegeuza ndio *park* basi itabidi walipe au tutazitoa. Nadhani kwa jumla Mhe. Jaku yale ambayo mengine sikuyasema unaweza ukaniuliza wakati mwengine.

Kuna Mhe. Mohammed Said Mohammed amesema mengi naye ni hayo hayo ya *X-ray* na nini, ameeleza *X-ray department* maposho ya kulipwa na nini. Tunashughulikia mambo hayo, lakini moja ambalo ndio nasema katika kupunguza wakati alilosema ni kwamba Hospitali yake ya Mpendae kama haikujengwa hatopiga kura naye atatoka nje.

Unajua Mhe. Naibu Spika, kuna vitu vingine sisi tulivyofundishwa utawala ni kwamba unsaema funika kombe. Sasa suala hili limekuwa likizungumzwa hata katika ziara za viongozi na mara nyingi limekuwa likisemwa. Sisi kama Wizara baada tu ya kuamua tujenge Hospitali ya Mpendae na Kwamtipura ya Mhe. Hamza Hassan Juma ambayo nadhani inamalizika na kaniletea hapa

katika mchango wake wa maandishi na kunambia kwamba nakupongeza babu kwa kutimiza ahadi yangu, ilikuwa nikamilishe na ya Mpendae lakini Hospitali ya Mpendae nikaambiwa kuna mgogoro wa kijamii pale kwenye jimbo.

Mbunge aliyepita zamani si vizuri kumtaja hapa aliifanya ile hospitali baada ya kuijenga ikawa ni yake na akawapa watu, viongozi wa eneo lile sijui jimbo, sasa kila kinachotaka kufanywa pale aa hii hospitali yetu, kila kinachotaka kufanya aa, hii hospitali yetu, sasa mimi nikasema sina watu mwenye watu ni Mkuu wa Mkoa, ni Mkuu wa Wilaya, mwenye watu ni watu wa jimbo.

Nimeonana na uongozi huo mpaka viatu vyangu vimemaliza soli na bahati nzuri nikamwita Mheshimiwa akiwa Mwakilishi kwa baraka ya Mwenyezi Mungu akawa Mbunge, nikamwita na Mbunge Mhe. Turki nikawaambia sina pesa hivi sasa kujenga hii hospitali lakini nyinyi ni wabunge wawili na mwakilishi mmoja he jamani taire, wakaseama babu tutaijenga, lakini kila wakitaka kujenga wanasema aa, hii hospitali yetu sisi tungefanya nini. Matokeo yake wakaiacha hospitali ile wakenda kujenga ile nyengine ya Jang'ombe ya ghorofa ile.

Kwa hivyo, si kwamba Mhe. Mohammed hatukutaka kutimiza wajibu wetu, tulitaka kutimiza wajibu wetu na suala letu kubwa lilikuwa moja tu Mhe. Naibu Spika, wale wenye ile hospitali watwambie hivyo hii mmeikabidhi Serikali au yenu, kama yenu endeleeni *Laila Hailallah*, lakini kama ni ya Serikali basi sisi ndio dhamana mpaka siku Naibu Waziri wa Afya, Dr. Sira na Waziri Mhe. Juma Duni watakapoondolewa wakaja wengine, tuacheni tufanye tunachotaka kufanya.

Makisio pale nimefanya mwezi wa Agosti mwaka jana baada ya bajeti mnajua zinatakiwa *three hundred million* kumaliza ile *floor* ya juu na kupandisha. Lakini sasa tulikuwa tumefungwa hatuwezi kufanya vyenginevyo tungetumia nguvu na ingekuwa Mswahili kutumia nguvu kitu si changu. Kwa hivyo, Mheshimiwa usitoke nje nipigie kura bajeti yangu na kama utanisaidia na viongozi wa Mkoa na Wilaya wananisikia mwakani sisi tutaijenga hatujakataa. Na kwa kweli ile itatusaidia kupunguza hili zogo la Mnazi Mmoja.

Mhe. Hamza Hassan Juma ikimaliza hospitali yake vichopocho vilioko pale Mwembeladu vyote tunapeleka pale Kwamtipura Hospitali ya Mwembeladu inakuwa *fully* Hospitali ya Wazazi kama ilivyokuwa zamani. Kwa hivyo yeye ametusaidia na sisi tumemsaidia na huko kwenu fanye hivyo.

Masuala mengine aliyoyauliza ambalo ni muhimu mengine yatajieleza baadae. Pale Maruhubi tumeruhusiwa tumepewa bohari na halafu tukapewa na eneo la Mkemia. Sasa pale Mhe. Mohammed anasema pameletwa Kiwanda cha Uchapaji kwa nini mmechanganya mchele na choroko na mpunga. Mheshimiwa tatizo letu moja tu, sisi tulikwenda kuomba na wenzetu walikwenda kuomba tukakutana chini ya mkunazi kila mmoja na balaa yake, sasa hatuna uwezo kukwambia bwana wewe mwenye *factory* utatufanyia ghasia hapa ondoka. Sisi tulipewa na wao wakapewa, sisi wenzetu tungependa tuwe pekeetu pale, lakini hali ya ugawaji wa majengo ni madaraka ya taasisi nyengine hatukuweza kubadilisha hivyo. Sasa madhali tutakuwepo pale tutashirikiana.

Mheshimiwa alizungumza habari ya *emergency room* kwamba ipo pale na kwa kweli inakuwa na matatizo, ndogo, kitanda kibovu, hata akija mtu hujui alazwe wapi. Siku hizi nashukuru nina mawasiliano mazuri baada ya mwaka mmoja na wenzetu walioko nje huko wanaitwa DIASPORA, nadhani nimeshaeleza kwa msaada huo wa makontena mawili ya vitanda vimejazwa pale Mnazi Mmoja, ukienda baadhi ya wodi zinaonekana kwamba sasa ni wodi. Hivi leo pia nimetia sainsi barua kuna msamaria mwema kutoka Uingereza katuletea kama 20 vyengine. Sasa tutajigusa gusa pale palipokuwa papaya tuondoe tuweke hicho kitanda cha *emergency*.

Lakini tumekubaliana ile *project* ya *ICU* kwamba na ile *emergency room* pale itiwe angalau *system* ya *oxygen* akija pale jamaa hata pumzi hana angalau tuweze kum- *resuscitate* aweze kupumua. Kwa hivyo, tunakwenda hatua kidogo kidogo, lakini tunatoka mbali.

Kulikuwa na suala nadhani mengine nitazungumza baadae kwa sababu ya muda, kuna Mhe. Abdalla Mohammed Ali huyu alizungumza mambo ya likizo nadhani Mhe. Naibu wangu ameyaeleza. Akasema suala kubwa kwake yeye ni suala la Chuo cha Afya Mbweni kwamba gharama kubwa ya mafunzo. Tulivyolinganisha na wenzetu gharama hii si kubwa kuliko wenzetu na tuisahau kwamba kile chuo kinataka kuendeshwa, kuna masuala ya utawala, masuala ya vifaa, masuala ya kila aina ya mambo yanakwenda pale. Sisi hivi ni kama shilingi laki sita lakini kuna wenzetu shilingi laki tisa, Chuo cha Uchumi shilingi laki tisa na wengine.

Na kwa sababu zamani walikuwa wanatoa shilingi 250,000/-, kwa sababu hiyo kwamba vile vipesa tunavyopata kwa wanafunzi havitoshi tumekwenda kwa Mhe. Waziri wa Fedha huko ametuelewa ndio maana akatupa ile ruzuku ya kiasi cha shilingi 556 milioni angalau tujishikeshike. Na tuisahau kuna majengo tuliosaidiwa na wenzetu wa Oman yanakaribishwa, maana yake huduma zitakuwa kubwa zaidi, umeme utakuwa mwingi zaidi, shughuli

zitakuwa nyingi zaidi. Kwa hivyo, nilitaka kusema tu kwamba hatukuwa na nia mbaya ya kutaka kuwabinya masikini na sisi tunajua kama masikini tunatoka huko huko na siku moja hapa Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika alinisikia sisi tumeuishi hasa huo umasikini sio kama tunajua tumeuishi. Kwa hivyo, hatukuwa na nia mbaya ya kuwasalimisha wagonjwa.

Kulikuwa na hoja ambayo ameisema Abdala Mohammed na yule Mheshimiwa wa mwisho niliyemtaja, kwamba kumekuwa labda kuna upendeleo juu ya wagonjwa wanaokwenda nje. Mhe. Naibu Spika, naomba hili nichukue muda kidogo kwa sababu dhana ni kitu kibaya sana.

Suala la wagonjwa kwenda nje tangu kuingia mimi pale hakuna hata mgonjwa mmoja aliyekubaliwa kwenda nje mimi nikamzuia, lakini kuna mfumo ambao lazima uwepo vyenginevyo kila mmoja atafanya vyake. Mgonjwa anatoka kwenye idara tuchukue mfano ametoka Idara ya Macho, Daktari wa Macho kwenye idara atasema huyu sisi hatuhisi kwamba tunamuweza anakwenda kwenye jopo la madaktari ambalo linaitwa bodi, bodi wanasema huyu sisi tunahisi anaweza kutibiwa Dar es Salaam taratibu zinafanywa na watu wetu wanapelekwa Dar es Salaam. Bodi inasema aa, chuma hiki kama hakijafika India hii ni balaa, bodi inasema kwamba huyu aende India, ikitoka hapo inakuja kwa *DG* wanamwita Mhe. Dr. Malik yeye akishaitizama akaridhika yeye ananambia mimi, Mhe. Waziri baada ya uchunguzi wa bodi na mimi sioni wala sina pingamizi kwa mgonjwa huyu kupelekwa matibabu India.

Mimi nikishaisoma ile saina ya Dr. Malik mana yule mtaalamu kule siwezi kujidai ni mshamba wa mambo yale naweka mkono wangu inatoka. Kwa hivyo, sikumbuki hata siku moja labda iwe nimesafiri kama kuna karatasi ya mgonjwa pale ikakaa zaidi ya masaa mawili kwenye meza yangu.

Na sisi tunapeleka kwa Mhe. Waziri wa Fedha na kuna wakati fulani tulikuwa tuna matatizo pesa zinazotengwa kwa wagonjwa wa nje ni chache, sisi tumezikuta shilingi 11 milioni nadhani. Tukashauriana na wenzetu vikapanda mwisho tukafika Serikalini tukaeleza tukaambiwa basi tutaweza *vote* kabisa na sasa kama mmeona kwenye makisio yetu kuna *vote* ya kiasi shilingi 336 milioni kama hivyo. Lakini Serikali ikasema nimesema kwenye bajeti yangu hakuna bei ya uhai, mimi sijawahi kusikia kwamba uhai bei yake ni shilingi bilioni moja watu wangukuwa wakinunua hasa wale wanaopenda kuishi zaidi wafanye dini, lakini hakuna bei ya uhai. Kwa hivyo, Serikali ikatwambia pale ambapo fungu lenu la wizara limemalizika hamna sababu ya kusema wagonjwa wasiende, kutaneni na wenzenu Wizara ya Fedha na wao watafute njia ili wagonjwa wende. Hilo likapata ufumbuzi.

La pili ikawa kuna malalamiko kwamba wagonjwa wanatelekezwa kwamba haya nenda yatakyokukuta huko wewe na Mungu wako. Imeamuliwa pia na Serikali kwamba asipelekwe mgonjwa wa daraja hiyo bila ya msindikizaji. Kwa hivyo, suala la kupeleka wagonjwa nje limeshasimama vizuri na linaendelea halina matatizo. Suala inategemea uwezo, uwezo kama haupo ndio mnakuta kama haupo ndio unakuta wengine wanapata wengine hawapati, lakini hakuna kwamba wa mwaka jana hakwenda wa mwaka huu kenda kama hiyo ipo itakuwa labda mimi sijui, lakini mimi nasindikizwa na watu wangu kwamba hali ni hiyo.

Naomba niseme kwamba wanaokwenda pale wengine ni washamba kuliko Juma Duni mara mia. Kama mnakumbuka tumepewa msaada na Serikali ya Oman watato 62 wamepelekwa India kwa huduma ya Serikali ya Oman vitoto vichanga vigonjwa vya moyo hatujashika hata senti moja, tena nimewaambia watu wengi aa, *procedures* ndege tiketi kila kitu wanakata wenyewe wanakutana India huko India kuna watu wao wa Oman huko huko wanawamanager wenyewe huko huko, alisema tu apelekwe mtu wetu mmoja daktari ili ende akaona na aje kuzifuatilia zile kesi hapa na akapewa mpaka na mashine akambiwa kaa hapa ujifunze huko huko.

Kwa hivyo, jamani anakuja bimbubwa pale samahani kutumia Matemwe, bibi wa Matemwe kuandika hajui, nini *visa* hajui, nini cheti za kuzaliwa hajui, nini *passport* hajui, zote tumefanya sisi, seketari na katibu wangu ndio walioshughulikia, wanakwenda Mambomsige kutafuta vyeti vya kuzaliwa, wanakwenda *Immigration* mpaka wakahakikisha wale wanapanda ndege *Alhamdulillah*.

Wamekwenda wamerudi hakuna tatizo lililotokea, labda kuna jamaa yangu mmoja sijui wa wapi ile hospitali anavyoogopa amefanya matatizo kweli huko India, mwisho akawa mtoto wake hataki kutibiwa nikapigiwa simu nikawambia mfungeni kamba mtieni kwenye ndege mtoto atibiwe. Lakini ni hali hiyo *Hamdulillah*. Kwa hivyo, hakuna kuchakachuliwa pale bwana. Watoto wawili wamepelekwa Israel kwa taratibu hizo hizo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niendeleee. Mhe. Omar Ali Shehe suala lake la kwanza alilosema ni suala la Mdhibiti na bahati mbaya kumekuwa na sifa maalum tumetiwa lakini tunaomba jamani muifute, kwamba Wizara ya Afya ndio masugu katika kutokujibu hoja. Nimewauliza wenzangu siku ile baada ya kuipata ile ripoti nikaichukua nikenda kumwambia Mhasimu Mkuu wangu hiki, hiki vipi? Akasema Mheshimiwa hizi zote tumezijibu, kulikuwa na hoja mbili zinazotoka kwenye *ADB* na moja *UKIMWI* kidogo ilikuwa zimechelewa lakini mwezi wa Septemba 2011 walikutana kwenye kamati pamoja na timu ya *auditor* pamoja na wale Wazngu wenyewe wanaohusika

zikasafishwa na zikafikishwa hatuna deni. Kwa hivyo, kama ni ripoti kweli ilieleza hivyo lakini tulishasafisha *audit query* zote.

Tumekuwa kidogo tunapata matatizo kwamba ile *audit query* inapokuja na kuzipata risiti. Kuna watu wengine wanakwenda Dar es Salaam hawa tunaowapeleka hawa, unamwambia boshi wee ukirudi huko basi pita hapa utuletee angalau zile tiketi ulizotumia tuwe na kumbukumbu, akishatiliwa huko huko cha mbele, sasa umpate wapi inakuwa balaa, *auditor* anakujia anakwambia mbona hakuna hapa safari hiyo lakini kwa vyovyote vile tunaomba kuthibitisha kwenu kwamba hayo yalitekelezwa kama yalivyotakiwa na naomba Waheshimiwa Wajumbe waniamini kwamba mimi mwenyewe ninajua ABC ya hayo mambo.

Suala la pili Mheshimiwa alilolisema ambalo nalo ni muhimu ni kwamba alisema Hospitali zisijengwe zaidi mana tunazo nyingi, lakini akaja akatoa mfano wa Mkanyageni kwa Mhe. Haji Faki Shaali na wengine walikuja kutoa hivyo. Kuna vituo vingine pale tulivikuta vya zamani kuna kimoja viwili vipya, lakini kuna vyengine vinajengwa nje ya amri ya Wizara. Kwa mfano, Mbunge Mhe. Makame Mnyaa na yeye kasema akajenge kwao si kapewa shilingi 50 milioni, sasa kenda kukiweka pale pale penye vyengine sasa kumwambia usijenge boshi anasema hapa ndio jimboni kwangu, tafuta kitu kingina anasema aa, afya. Kwa hivyo, nadhani huo ulikuwa ni mfano lakini sio mfano mzuri sana katika ile hoja yetu ya msingi.

Hapa Mwera kipo kikubwa, kuna Kinuni tunakaribia kukimaliza, kuna chengine kule kwao Mhe. Karume kipo, lakini vyote hivyo ukipiga *circle* hakuna panapotimia kilomita tano. Kwa jumla hali ya vituo inatoshwa, vingi vibovu, vingi havina zana, vingi vinataka matengenezo hilo tunalikubali.

Suala la madaktari nadhani Mhe. Naibu Waziri amejitahidi na ameeleza jinsi tunavyohitaji kuchukua hatua na kwamba tutashirikiana na wizara ya mwenzetu. Kulikuwa na ushauri ambao nao ulitolewa na Wajumbe wengi kwamba tujenge *ICU* Pemba na hata Mhe. Hamza Hassan naye alisema hivyo. Hatukatai ni suala la msingi lakini linahitaji maandalizi. Kwa sababu wale wanaohitaji kuitunza ile *ICU* yenyewe kuiendesha inahitaji wataalamu, kuna wale wenye kunusa nusukaputi, kuna wale watu wa *ECG* wanaotizama ule moyo ukifanya kwiti, kwiti, kuna watu wa aina kama nane hivi ambao inabidi kwanza uwatayarisha na uwafundishe. Sasa kama hapa aliposema Mhe. Rashid Seif kama hapa Mnazi Mmoja kofia imeroa kwa hivyo mjue hali ilivyo, lakini tunalifikiria hilo.

Kumekuwa na suala hapa vile vile na la msingi kwamba *public health (PHL)* je, inapata fedha, inasaidiwa fedha au ikoje. *PHL* inafanya *research* na ile ni

research institute inayojulikana dunia nzima, watu kutoka duniani kote bwana kote wanafanya *research*. Sasa wakija pale wakishirikiana na watu wetu huwa vinaachwa visenti pale, sasa vile visenti wanavyopata wao pale ilikuwa sisi Serikali nasi tuwachangie, lakini vile wanavyovipata vinatosha mara nyingi wanawasaidia na Hospitali ya Chake Chake, wanasaidia vifaa, wameweza kujenga jengo jengine pale la utawala. Kwa hivyo, si kwamba sisi tupeleke lakini wao wanatuonea huduma mara nyengine wanasema basi vitu fulani tutahudumia. Kwa hivyo hilo linakwenda hivyo.

Hapa hapa nadhani nilieleze la Mhe. Rashid Seif Suleiman yeye alisema taasisi ile ina sheria, inakwenda kienyeji au inakwenda vipi. Taasisi ile ilijengwa kwa mashirikiano na *foundation* fulani kutoka Italy na kamishna wake ni pamoja na wawili kutoka Zanzibar, wawili kutoka Italy na mtu wa WHO. Lakini halijawa na sheria, tunauchukua ushauri wako sasa tulitayarishie sheria liwe linakwenda kisheria kama ulivyotuzindua. Mheshimiwa nashukuru naomba niendele.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi wa Rahaleo pale rafiki yangu mwana michezo yeye aliuliza sana masuala ya watu wanaokuja kuwatizama wagonjwa kwamba wawe na mahala pa kujificha. Nililieleza kwamba ni moja katika tatizo mrundikano wa hao watu na nimezungumza na Mkurugenzi wetu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja amenieleza kwamba kwa kweli tulishapiga mpaka ramani, tuna kila kitu kilichobaki ni kutafuta fedha, sasa tutatizama hali ya mfuko wetu utavyoendelea tunaweza kujibana bana mwakani tukaanza kujenga, la tukipata muhisani ambapo tunajitahidi kwa sababu banda lenyewe sio kubwa hata hivyo nadhani kama sijasahau ni kama shilingi 25-30 milioni ili watu wapate sehemu nzuri. Tutafikitia kufanya hivyo kama mlivyoshauri Waheshimiwa.

Pia alisema habari ya vyakula vibovu kwenye *super market*. Watu wetu wamesema wanafuatilia kama wanavyoweza katika kila kichocho na pale ambapo wanavikuta vibovu ndivyo wanavichoma moto au wanavikusanya au wanavichukua kuviharibu. Hilo linashughulikiwa.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala ambalo linasema kwamba ukipita pale Mnazi Mmoja unaingia hospitali penye wale vijana wa mlangoni pana mashimo na wazazi wengine huzaa kabla hawajafika *maternity*. Tulikuwa tulishashirikiana na wenzetu wa Mwasiliano Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mwasiliano pale, akanambia wanapokuja Kikwajuni watu wake kujenga zile barabara na pale watatengeneza, nimeambiwa kwamba nalo limeshachukuliwa hatua. Tunakushukuru Mhe. Naibu Waziri na Wizara yako kwa msaada huo ulioweza kuchukua hatua.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu alizunguza habari ya *audit report*. Kwa sababu Mhe. Omar Ali Shehe tumeshamuelezea nadhani alikubali hilo kwamba nalo tumeshalishughulikia.

Mhe. Naibu Spika, chengine alichotushauri Mhe. Jussa ambacho ni kizuri na kwa kweli ni cha kawaida ni mpangilio wa kwamba ukifika pale hospitali ujue unakwenda wapi. Leo Mheshimiwa mmoja alisema tungekuwa na vitambulisho, nadhani Mhe. Nassor Ali nakushukuru bwana, unahitaji kuona jinsi wapi pa kwenda. Hiyo ni moja katika kazi ya mtu anayeitwa *Public Relation Officer*, tulishawaagiza watu wetu wa hospitali awepo mtu huyo na vitu hivi avishughulikie na hata yale makelele ya watu wanaolalamika wakitaka kulalamika wanajua wanakwenda wapi na mahali gani, hilo tutalichukulia hatua.

Kwa hivyo, ukichanganya ile *procedure* ya vielekezo ukija ukichanganya na ile ya vitambulisho gekuwa tuna vitambulisho mtu anayetoka *X-ray* ajulikane kwamba katoka *X-ray* na kwa kweli kumeshafika hatua tunaingiliwa pale na wizi usiku. Kwa sababu ya lile jengo lilivyojengwa liwazi sana, sasa anaingia mtu unaona huyu anakwenda kwa mgonjwa kumbe anakwenda kuwaibia wagonjwa. Kwa hivyo kuwa na vitambulisho inasaidia na vile vile tunaweza tukabagua nani. Bila shaka sare ni kitu muhimu nalo ni suala la kidogo kidogo.

Mhe. Jussa vile vile alisema masuala ya uchafu wa hospitali ambao nimeshauleza. Lakini vile vile aligusia akasema pia kuna uchafu mjini, marikiti, kuna mheshimiwa mmoja alisema kule pwani. Naomba niseme mambo mawili.

Kuna suala la *Public Health Law* ambapo Mhe. Othman Masoud na sisi tunakamilisha, nimesema humu imeshatoka BLM. Lakini ile *Public Health* ni mtambuka, kila mmoja ana sehemu yake. Sasa mambo ya uchafu wa sokoni na pwani na wapi ni masuala ya Manispaa na Mhe. Mwinyihaji ananisikia hapa.

Sisi tunachofanya kwenda kuona uchafu sokoni akipata mtu ugonjwa inakuwa ni balaa. Kwa hivyo ni sisi hatuwezi kuona uchafu upo sokoni kwa sababu unatuongezea kazi ya hospitali. Kwa taarifa yenu juzi *registrar* wangu Dr. Burhan aliniletea picha nikampelekea Dr. Mwinyihaji hali ya kutisha ya soko la kuku.

Ukiiona ile hali kuku humli lakini ukimkuta juu ya meza utakula mwanzo kuliko wali. Hee! bwana pachafu pale sijapata kuona na watu habari hawana. Nilichoagiza Dr. Burhan kawapa wiki moja, akaniambia baada ya wiki moja

tunafunga. Nikamwambia fungu wacha watu wasile kuku na nikampelekea Mhe. Mwinyihaji zawadi yetu hii mimi na wewe, akaniambia na mimi ninalichukulia hatua.

Kwa hivyo yanayohusu mjini sisi yanatugusa kwa suala la usafi mgonjwa akiuguwa, wakipata kolera tayari, dawa hakuna, tumekwenda tumekaa muda wa saa mbili, mgonjwa anahariana lakini uchafu hakuona kama ndio uliosababisha. Kwa hivyo tunaomba tushirikiane hilo.

Matibabu ya nje aliyoyasema na akasema hasa kuwa mgonjwa wake kwamba vile vile alitelekezwa. Sisi wanaokwenda nje, tunasema kama mgonjwa tumemuandikia dola elfu tano au zaidi. Zinapoongezeka hatujawahi kusema kama mumrudishe au asitibiwe. Lakini kuna hatari vile vile ukiziacha *loose* ikawa japo hapana sababu, ikawa matibabu yakipata pesa matumizi yakaongezeka. Lakini kama ilitokea hiyo basi halitokea tena. Maana kupelekwa wanasindikizwa na matibabu tunayasimamia vile inavyostahiki kama inavyotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, niende haraka haraka kuna Mhe. Mtando. Mhe. Mtando ameeleza mambo mengi, akasema dawa hakuna za kutosha hospitali ya Kivunge na mahospitali mengine. Akazungumza mambo ya matibabu ya nje, kwa hivyo linajirudia. Kazungumza maslahi ya wafanyakazi, kasema huduma dhaifu.

Ninachoweza kumjibu ni mambo mawili makubwa. La dawa Mwenyezi Mungu akitujaalia litakuwa halina tatizo tena. Kwa sababu kama tulivyosema bilioni moja nukta tano tunapewa na Mhe. Waziri, bilioni moja nukta tano tunapewa na DANIDA na kuna pesa zinaweza zikaja kutoka kwa wafadhili wengine, zote tunazitia kwenye mfuko mmoja. Tunaitisha tenda, tunatafuta yule mwenye uwezo, akishakuja tunamwambia bwana badala ya kila tenda tunataka tukubaliane kwa masharti haya. Aidha kila baada ya miezi mitatu unaletewa *amount* hii na pesa zinalipwa. Hilo ni moja.

La pili utaratibu wa zamani ni kwamba sisi tunachukua dawa kutoka *Medical Store Dar Es Salaam (MSD)*. Tunakwenda dawa hazipo, tunafungwa viboksi vishafungwa kasoro, nyengine tunazipata muda wake wa kumaliza ni mchache hazikutimia. Tumeomba Serikali tukasema hizi haziwezi kuwa sisi tukasumbuliwa na watu wetu kwa makosa ya mtu mwengine. Serikali imeturuhusu, kwa hivyo ikilazimu hatutochukua tena dawa kutoka MSD, kwa hivyo suala hili litakuwa limekwisha.

La tatu ni kwamba dawa ilikuwa tunapeleka ziliopo. Utaratibu mpya ni kwamba hospitali itatwambia, Mkwajuni hapa maradhi aina haya ndio

makubwa, maradhi ya aina haya ndio yanayotokea kila mara, maradhi ya aina haya ndio tunahitaji dawa za aina hiyo. Kwa hivyo dawa zitakazopelekwa ni zile ambazo hospitali itatwambia. Kwa hivyo suala la upungufu litapungua sana.

Suala la mafungu, kuna baadhi ya mafungu yameambiwa kwamba mafungu haya yanataka maelezo kwa nini mengine ni makubwa kwa sababu ni suala la jumla naomba nije nilijibu kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala ambalo ametaka Mhe. Abdalla Juma Abdalla, alieleza mengi lakini mwisho akaishia kusema kwamba si vizuri wanawake kutibiwa na wanaume na hili Mhe. Sira ameshalijibu vizuri sana.

Mhe. Mahmoud ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni alieleza mengi lakini kubwa alisema kwamba mwaka jana alizungumza suala la *research* ya *Non Communication Diseases* kwamba maradhi haya yanaongezeka lakini mukasema kwamba labda mungeweza kufanya *research* mukatueleza.

Tulifanya *research* na sababu zilipatikana na ripoti ipo na imeonesha ni matatizo gani yanayosababisha maradhi haya kuongezeka. Moja ni mfumo wa maisha wenyewe, tabia yetu ya kula vinono. Juzi nilikwenda kufungua chanzo cha mradi huo, tunapiga vinono, semina ukifika pale pana mapochopocho unapiga, saa nne kuna viburudishaji unapiga, mchana kuna *lunch* unapiga, ukifika nyumbani ubwabwa uliopikiwa na bibiye unaupiga halafu unalala.

Matokeo yake kilo zinaongezeka, kwa hivyo moja ni hilo *pattern* ya maisha. Tatu ni aina ya vyakula tunavyokula. Sisi hizi kila tunapopata nafasi yule anayekaa naye *informal* huwa ninamwambia aah! sukari basi inatosha, niache bwana sukari balaa, wacha sisi tuliyekuwa tunakimbiza huko saa kumi na moja huko. Lakini bila shaka kumekuwa na watu wanasema labda vyakula vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi labda vina matatizo. Taasisi yetu inajitahidi na tutaendelea kuliepuka lile lililokuwa na matatizo na ndio maana vyakula vibovu tunavirudisha au tunapeleka mwituni. Mengine yalikuwa ni yale ambayo yameshazungumzwa na watu wengine.

Mhe. Rashid Seif Suleiman ameuliza mambo mengi kidogo. Kwanza alitaka Wizara iitwe Afya na Ustawi wa Jamii lakini tumepunguziwa hilo. Alikuwa na lawama kwamba mchango wa Serikali wa bajeti ni mdogo na kuna makubaliano ya kimataifa yale ya Abuja Nigeria tufikie asilimia 15 by 2015.

Suala hilo ni kweli lakini nimelieleza uwezo wa Serikali. Kuna sababu tatu kwa nini wanashindwa kusukuma hilo. Kwanza ongezeko la maradhi

nyenyewe. Pili hali ya uchumi na tatu ni uwezo wa kuzigawa zile raslimali nyenyewe kwamba unaweza kusema upewe afya tu vyengine havipewi.

Lakini kila mara tukiwa na Mhe. Waziri wa Fedha na tunapokuwa Serikalini tunalisema hilo kwamba tuna-*obligation* ya dunia kama vile tulivyokuwa na *obligation* ya MDG ya *Millenium Goals* na hili nalo linastahiki. Kwa hivyo tunasogea lakini kuna maelezo mengine tuliyoupewa kuhusu suala hili ni kwamba inawezekana kabisa ile keki ya afya ikawa ni ndogo. Lakini kuna vitu vinavyohusiana na afya ambavyo havipo kwenye Wizara yetu, tukapewa mfano kwamba kituo kipo Matemwe ambapo Mhe. Wa Jimbo la Matemwe kule Kijini mwisho karibu Mhe. Rais alikwenda.

Sasa kule kuna kituo lakini kituo kile pamoja na kuwa kule kutoka hapa Matemwe kufika kule hakuna barabara. Sasa itakapojengwa barabara ile ikawa laini pamoja hazikutiwa kwenye Wizara ya Fedha lakini kule kuondoa tatizo la barabara, linaruhusu masuala mengine ya urahisi kufikia kile kituo. Huo ni mfano mmoja.

Mfano wa pili tukaambiwa maji. Haya tushajenga hicho kituo, maji hapana lakini maji si suala la afya, maji ni suala la Wizara nyengine. Kwa hivyo kutayarishwa mradi wa maji ikawa maji yanapatikana itakuwa *indirectly* kuleta huduma hiyo. Kwa hivyo mara nyengine *percentage* haiwi sawa sawa kwa sababu ya mahusiano ya masuala hayo.

La tatu alisema kuhusu mpango na sera kwamba zina kazi moja. Naomba kumwambia kwamba hazina kazi kazi moja zina kazi tofauti na bahati nzuri ramani hizo za *structure* tuliletewa na Serikali, kuna *department of administration and human resources*, ina-*administrative human resource division* na *record management division*.

Sasa utawala na uendeshaji, majengo kuyatunza ni utawala. Kitengo cha sheria kipo chini ya utawala, *human resources* ni *division* inayoshughulikia na wafanyakazi. Mipango kazi yao kutayarisha mipango ya afya, kutayarisha bajeti, kufanya ripoti za afya, kukusanya takwimu za afya, kufanya *research* za afya na mambo mengine. Kwa hivyo sisi tunavyoiona haingiliani, ingawa mmoja anaweza kumuhudumia mwengine.

Mhe. Naibu Spika: Babu Juma muda.

Mhe. Waziri wa Afya: Ndio maana mhesimiwa ninachukua zile hoja zilizo nzito kwa sababu nikenda moja moja inakuwa kidogo mushkeli.

Sasa baada ya hapo nilikuwa na mheshimiwa gani ambaye ameleta changamoto. Mhe. Rufai suala lake kubwa lilikuwa ni kuchakachuliwa, Mhe. Mohamed Mbwana alitaka masuala ya usalama wa wafanyakazi ninadhani Mhe. Sira amelieleza.

Akalizungumza suala la wakunga wa kienyeji. Wakunga wa kienyeji kwa kawaida hawatakiwi wafanye kazi bila ya kufundishwa, tunatakiwa tuwafundishe lakini hatuna uwezo wa wote wazazi kuwapeleka hospitali inabidi wafanye, sasa inapobidi wafanye wanapewa mafunzo kwa wale wanaostahiki kufanya na wanapewa shahada za kushughulikia na vijisenti hupeleka. Kwa hivyo hilo si tatizo ambalo kubwa.

Upungufu wa madaktari ni la jumla. Akasema kwamba Kituo cha Chambani hakijafunguliwa. Kituo kile kimetengenezwa lakini kimetengenezwa kwamba kinaonekana ni kipya hakina haja ya kufunguliwa kinaendelea kufanya kazi.

Mhe. Subeit Khamis Faki ambaye yeye ameeleza mengi ambayo mengi yalikuwa ni yale ambayo yamerudiwa na watu wengine. Moja alilolisema ni kwamba hospitali za vijiji zile wodi ni ndogo. Ni kweli ndogo lakini kwa sasa hivyo ndivyo zilivyo hospitali zote na hapo tutakuwa tunaendelea na upanuzi kuelekea huko tunakotaka basi tutajenga hizo wodi kubwa.

Mhe. Shawana ameshajibiwa, Mhe. Salim Ali Hamad ameshajibiwa na Mhe. Sira na Mhe. Rufai nimemueleza na mengi yalikuwa yanastahiki hivyo. Kuna waheshimiwa wengine wamenipa kwa maandishi lakini nilipoyashughulikia nikakuta mengi yanarudiwa, kwa hivyo nitakuwa tumeeleza pale panapostahiki.

Kuna mmoja Mhe. Hassan Hamad Omar wa Kojani alilizungumza suala la wagonjwa wa akili kutembea ovyo. Ni kweli hayo mengine yanatokea lakini tunategemea kwamba na jamii nayo ina dhamana yake ya kulishughulikia suala hili. Sisi anapofika hospitali ni mgonjwa wetu lakini anapokuwa kwenye jamii anakuwa ni mgonjwa wa jamii, aidha kwa kijiji, jimbo au familia. Familia ikichukua hima ikimleta mgonjwa yule hospitali ni dhamana yetu lakini hatuwezi kuwa madaktari wetu tukawatunafukuzana na wagonjwa wa akili barabarani, huyo mkamate haiwezekani. Sisi tunamngoja aje pale hospitali ili tumshughulikie.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mlinde alizungumza matatizo ya kule Kiongwe na Mhe. Bi. Ashura hivyo hivyo aliniambia hilo. Tumeshaliandika nalo kama tutalimaliza wakati utakapowadia, kwa sababu vituo vyote Mhe. Sira ameshaviorodhesha kwamba tuitengeneze na kuvimaliza vile vilivyokuwa

vipo. Lakini tunaomba tusijenge vipya, mutatumaliza sisi kwa sababu hatuna fedha.

Mhe. Mohamed Ali Khalid yeye amehimiza kwamba suala la afya bila ya malipo ni la kiserikali. Bado tunamwambia kwamba hilo ni dhamana yetu lakini tutalichukua taratibu kama vile inavyostahiki kujenga kidogo kidogo.

Mhe. Mohamed Mbwana alisisitiza mambo mengi lakini akasema vile vile masuala ya kuzalisha wakunga wanaume kwa wanawake, Mhe. Sira amelisema hili na kama kuna jengine ambalo hatukulijibu basi ni vizuri tukaeleza.

Mhe. Naibu Spika, namalizia Mama Kissasi alitupa shukurani lakini akasema tumsaidie kituo chake cha kule Fuoni. Tumeahidi hicho tutashughulikia.

Mhe. Naibu Spika, suala la mwisho maana naona waheshimiwa wameniambia wameshasikia, suala la mwisho ambalo nimesema kwamba nitalijibu kwa pamoja ni suala la vifungu.

Kuna vifungu vimeonekana vimevimba hasa vile vinavyostahiki kwenye *sitting allowances* sijui na viburudishaji na nini. Ukilichukua hili buku ukipitia Wizara zote utakuta mafungu hayo yamebadiliko *across the board*. Kwa hivyo si suala la Wizara moja.

Sasa wengine walikuwa wanasema kuna nini huko, hakuna nia mbaya waheshimiwa. Suala la kwanza ni kwamba posho wenyewe limebadilika na nyinyi wenyewe munajua. Si vizuri kueleza zaidi lakini munajua kwamba posho limebadilika. Kwa hivyo lazima vifungu vitaongezeka.

Lakini suala la pili ninajitolea mfano mimi sisi kila mwezi inabidi tukutane Kamati Tendaji na watu wowote ni hivyo hivyo. Kila miezi mitatu sasa tutengeneze bango kitita ambalo ni nusu ya ule MTEF. Kila miezi mitatu lazima tukaeleze turudi tena, kwa hivyo kwa jumla zile shughuli za serikali hivi sasa zimechangamka, activities ni nyingi sana.

Ninakumbuka nilimwambia Mkurugenzi wangu wa Mipango hapa lakini ninadhani tumekosekana atuletee lile dudu linaloitwa MTEF, *volume* kama hizi ni mbili mpaka tatu. Siku moja niliwatania lakini nyinyi munazaa maana saa zote muko kwenye kiti. Ni dudu kubwa linalochukua muda. Mara nyengine inabidi watu wajitenge waende nje ya Makao Makuu ya Wizara ili kujipa muda ya kulishughulikia. (*Kicheko*).

Bahati nzuri waheshimiwa naomba wanistahamilie mimi mwenyewe mara hii nimeshiriki, nimekwenda Jambiani mimi na Wakurugenzi na vijana wangu. Mhe. Naibu Spika, amini usiamini tunaamka baada ya kusali alfajiri tunaingia kwenye *hall* hatutoki mpaka kusali saa saba na kula *lunch*, tunarudi kwenye *hall* hatutoki tunasali laasiri, tunarudi kwenye *hall* tunakuja kula *dinner* mpaka sita ya usiku, wiki nzima, ndio munarudi mjini ndio munasema kuna kitu cha kuwasilisha.

Kwa hivyo mambo mengine yanavyoonekana yanaonekana kama kuna nini, hakuna kitu. Mheshimiwa Mkurugenzi hapa wa hospitali ameniletea mfano wa jinsi ya kifungu cha matumizi ya petroli. Maombi tuliomba matumizi ya petroli, tuliomba *seventy two million* na pale tuna *ambulance* mbili na jenereta moja.

Munajua hospitali ikizimika umeme lazima jenereta, ikizidi siku tatu tu umeme hakuna ni balaa, maana kifungu cha petroli kimekwisha. Hivyo ndivyo ilivyo kwa mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka hilo lieleweke kwamba hakuna matatizo ya vifungu hivi kwa nia mbaya isipokuwa ni kwamba shughuli zenyewe zimechangamka na vifungu vya matumizi hivi vinakuwepo.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, watu watofautishe kati ya *sitting allowance* na kiburudishaji. Kuna mheshimiwa mmoja alifanya *joke* isiwe kiburudishaji maana yake ni kucheza mziki. Kiburudishaji maana yake ni ile chai ya saa nne tunayotoka baada ya kupumzika kwa semina ambapo tunapata chai na kikeki na *sitting allowance* ndio kile kibahasha.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 24

Wizara ya Afya

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	shs.1, 000,000/=
Kifungu 0601 Idara ya Kinga Unguja	shs.29, 000,000/=

Kifungu 0701 Idara ya Tiba Unguja
Kifungu 0801

shs.20, 000,000/=

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nilikuwa nipate ufafanuzi kwa Mhe. Waziri kwenye hili fungu 0801 vote 142221 – malipo ya X ray na uchunguzi wa damu. Naona huku mwaka jana makisio yalikuwa kwenye milioni 15 na mara hii yameshuka sana, nilikuta ninataka ufafanuzi kwa hili kwa nini.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza wakati ninajadili masuala haya ni kwamba kunakuwa na matatizo ya X ray kuharibika, mara hiki hakuna. Sasa tunapoweka bajeti kubwa halafu tusitamilize tunaonekana kama vile tumedanganya. Kwa hivyo tumeona tuweke ambazo tunaweza kuzikusanya wala si kwa sababu nyengine yoyote.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, sijasikia vizuri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ninasema kwamba makisio tuliyoweka hapa ni yale ambayo *realistic* hatukutaka kuweka makisio makubwa halafu tusiyakusanye ukaonekana kama vile tumedanganya. Lakini la pili matatizo mara ya X ray kuharibika ndio moja katika mjadala mkubwa ulikuwa upo hapo. Kwa hivyo ninasema nitapata mapato kutoka X ray kiasi hiki mara Mkoani, Micheweni au Chake-Chake imeharibika, kwa hivyo kuharibika kwake ndio maana yake hupati mapato. Kwa hivyo tumejiwekea makisio ambayo yanaweza kupatikana badala ya kuweka makubwa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendeleo.

Kifungu 0801 Idara ya Tiba Pemba
Kifungu 1501

shs.45, 000,000/=

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake na ufafanuzi kuhusiana na vifungu mbali mbali nilivyovichangia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo katika mchango wangu niligusia fungu hili la mapato kwamba palikuwa na mapato haya ya mia moja na tisini milioni ambayo yapo vote 145003 – Kitengo cha Huduma za Haraka. Nikasema ukilinganisha lilivyokuwa na buku kubwa na haya marekebisho ulikuwa huzioni, kamati imefanya kazi nzuri ikataka ziingizwe.

Sasa nimemsikiliza Mhe. Waziri katika hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba sawa zimerejeshwa lakini nikasema hapa zimerejeshwa

baada ya kamati kuingilia kati. Hata ukiangalia hii karatasi iliyokuwa imefanyiwa marekebisha miaka iliyopita kweli utakuta ziro ziro huku Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo nikasema sawa zimeonekana kamati ikachukua hatua zimerejeshwa, lakini nikamtaka Waziri atusaidie kwamba wale watendaji ambao walikuwa hawazioneshi mpaka kufika kamati idai atawachukulia hatua gani ili vitendo kama hivi visirejee tena.

Sasa hilo Mhe. Waziri katwambia tu kama zilikuwa zinaingia lakini ninataka kusema hata katika kamati tunapewa taarifa kwamba Mhasibu mwenyewe wa Wizara hakuwa akizijua pesa hizi matumizi yake na utaratibu wake. Sasa nilikuwa ninasema hebu atusaidie Mhe. Waziri hapa palikuwa na pesa si kiasi kidogo zilikuwa hazionekani, sasa kamati imesaidia zimeonekana zimerejeshwa lakini yeye kama Waziri na uongozi wa Wizara utachukua hatua gani kwa watendaji ambao walikuwa wanaficha mapato haya kiasi hiki ambacho hayaonekani katika mapato ya Serikali.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikieleza hapa nilisema kwamba utaratibu wa kukusanya mapato ulikuwa hawendi Wizara ya Fedha, ilikuwa pesa za michango wanazikusanya wanazitumia, na hiyo tangu utawala wa Mhe. Salmin Amour.

Mwaka jana Baraza hili ndio likaanza kusema kwamba sasa ndio zipelekwe. Sasa ule utaratibu wa kupelekwa ndio uliokuwa unaonekana kama vile pesa zinafichwa, ilikuwa hazifichwi. Sasa katika kukusanya pesa hizo ikaonekana *first tract* pesa zake hazijapelekwa basi tulipoagizwa na tume tukazichukua nazo tumeziingiza kwenye mfuko.

Lakini hakukuwa na suala kama kuna mtu kafanya kosa, ulikuwa huo utaratibu wa zamani uko hivyo. Sasa utaratibu huo umesema tupeleke zote zimepelekwa. Tunaishukuru kamati kwa kuziona kwa hivyo pesa zote zinaingia mkono wa Serikali halafu zinarudi tena hospitali, yaani zinapita kulia zinarejeshwa kushoto.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa Mhe. Waziri hoja yangu ilikuwa na kaeleza vizuri kwamba Baraza hili mwaka jana, naomba nimnukuu vizuri Baraza mwaka jana iliagiza mapato haya yote yawe yanapelekwa Hazina. Halafu ndio yanafuata utaratibu wa kawaida kutumika.

Sasa hata baada ya mwaka jana Baraza hili kuagiza hilo, Kitengo cha *First Tract* hakikupeleka mpaka kamati mwaka huu, sio mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, kilipozihoji ndio zilipoingizwa. Wajumbe wa kamati

wanatwambia na wapo hapa wanaweza kusaidia ukiwapa hiyo nafasi kwamba hata Mhasibu wa Wizara alikuwa hazioni.

Mimi kidogo ninapata wasi wasi kwamba inawezekana kwa sababu ya hiyo chaka lilivyokuwa tangu hizo zama hizo alizozisema Mhe. Waziri kwamba zikitumika bila ya kuingizwa Wizara ya Fedha lakini labda atusaidie hapa kwamba yeye kama msimamizi mkuu wa Wizara kwa mujibu wa Katiba yetu, kwa sababu yeye sina wasi wasi naye hata siku moja, nimefanya naye kazi na Mhe. Waziri ninamjua sana uaminifu wake katika masuala ya fedha, lakini ninataka nisaidie kwamba kwenye masuala haya kawahi kufuatilia kwamba kweli pesa hizi zilikuwa zikitumika ipasavyo na kuna kumbukumbu za matumizi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwenye mchango wangu hizi fedha wanaokwenda kukamuliwa ni wananchi maskini wasiokuwa na uwezo, anataka kutibiwa huku anaambiwa lipa hiki anakwenda mbio mpaka analipa anatibiwa. Sasa tuone kile kinacholipwa kinafika kule kulikokusudiwa katika kuchangia huduma au kinaishia mifukoni mwa watu. Ninataka suala hilo anisaidie Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Umemfahamu.

Mhe. Waziri wa Afya: Nimemfahamu Mhe. Mwenyekiti, naomba kumthibitishia kwamba fedha hizi zilitumika kama zilivyokusudiwa, zilikuwa zinatumika katika kitengo cha *first tract*. Mimi mwenyewe baada ya kuambiwa kwamba kuna fedha fulani hazijaenda ambao hao watendaji wangu walikuwa wanaona kwamba hizi zinatumika kwa *first tract* haziwezi kuongojea, anakuja mtu pale anatibiwa katika hiyo *first tract* ni *different time* na hii ya huku. Nikawaambiwa aah! zote ziende.

Kamati ikatwambia zote ziende. Utaratibu wa kuzirejesha kwa haraka tutakuwa sisi na Wizara ya Fedha. Mimi nimeita *bank statement, cash book, statement* zote zilizofanywa kwa miaka mitatu iliyopita. Ndio maana nikasema pale zipo hapa ambapo Mhe. Mtando vile vile aliuliza hizo, zipo hapa na zipo clear na bahati nzuri mimi nina (a), (b) (c) ya mambo haya nimejitosheleza.

Sasa kama kuna mtu anahisi kwamba ziliingia mikononi mwa mtu, basi sina matatizo kuja kuchunguzwa na *auditor*. Lakini mimi naomba kuwathibitishia ma-*auditor* na wale Waheshimiwa kwamba nimeziona, nimezipitia na naomba waamini kwamba tunazijua jinsi zinavyosomwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwa sababu uzuri wake Mhe. Waziri yuko wazi kabisa, kasema anakaribisha hata ukaguzi. Kwa hivyo, mimi niombe kwamba kwa sababu Baraza hili kwa mujibu wa sheria ile ya CAG inayo uwezo wa kumtaka akafanye ukaguzi. Kwa hivyo, tuombe kwamba CAG akishirikiana na PAC kwa upande wao, waende wakajiridhishe kwa miaka hii iliyopita kwamba fedha hizi kweli zilikuwa zikitumika, kuna kumbukumbu sahihi na kwamba kweli zilikuwa zinatumika kwa makusudi yaliyokuwa yamefanyika.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nafikiri ukifanyika ukaguzi baadae tutakuja kupata nafasi, tuko hapa hapa mwaka sio mwingi tutakuja kuzihoji tena. Naruhusu tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 150

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, tunaomba tuweke kumbukumbu sawa tu. CAG hashirikiani na mtu yeyote. CAG anafanya kazi peke yake, halafu ripoti itakapokuja PAC wanaweza wakaenda. Sasa tukiweka *on record* hivyo, kwamba CAG ikishirikiana na PAC, itakuwa sivyo.

Kwa hivyo, CAG waende wakafanye *auditing* baadae waletе *report* yao, wakishaleta *report* yao kama PAC hawajaridhika basi wanaweza wakenda. Naomba tuweke *record* sawa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani hatukukosana sana, CAG itafanya kazi yake na PAC itafanya utafiti kwa njia ya taasisi inayohusika. Tunaendelea.

Kifungu 1501	Hospitali ya Mnazi Mmoja	900,500,000
	Jumla ya Fungu	995,500,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 24 – WIZARA YA AFYA

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nimuhoji Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilielezea umuhimu wa kuwa na huduma maalum ya ICU Pemba. Lakini kwa kweli

jawabu lililotolewa halikuniridhisha. Sasa naomba Mhe. Waziri atumie nafasi hii anipe jawabu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, sikusikia vizuri. Lakini katika

Mhe. Mwenyekiti: Anasema alipochangia alisema kuna haja ya kuwa na ICU Pemba, lakini majibu uliyoyatoa hayakumridhisha anataka ya ziada.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, majibu ya kumridhisha ni kwamba ijengwe, lakini kusema nitajenga nitakuwa namdanganya. Kwa hivyo, ninachosema tumelisikia hilo suala, tutalifanyia kazi, kwa sababu sio kitu cha mara moja kinahitaji maandalizi makubwa, kwa sababu kama ile ICU ya kwetu hapa hatujaweza kutimiza yale mahitaji, hasa ya wataalamu. Vifaa tumeshapata kwa juhudi za Waheshimiwa, lakini wataalamu.

Kuna Mhe. Mjumbe mmoja juzi kasema kwamba kuna daktari pale hasa anayejua kushughulikia ICU, ni kwamba hata yule aliyekuwepo anahisi kwamba uwezo hana. Sasa hatuwezi tukaweka ICU kule tukamuweka *orderly* kusimamia ICU. Wamesema hapa kwamba wataalamu na madaktari hakuna, wale madaktari wa kwenda asubuhi wakamtazama mgonjwa hawatoshelezi. *ICU ni Special duty special work.*

Kwa hivyo, kama ni kulizingatia tunalizingatia na kwetu sisi ni muhimu kwa sababu huwezi kumrusha mtu katika mkondo wa Nungwi kama anaweza kutibiwa Pemba, lakini sio suala la hapo kwa hapo, ni suala linalo maandalizi. Nimesema pale kwamba tumelipokea na tutalishughulikia, lakini sio suala la mara moja. Sasa sijui nimtosheleze vipi zaidi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwanza kwa kuniambia amelipokea. Kwa sababu jambo lolote lile kwanza hulipokea, na hatua ya pili ni kulikubali, maana yake unaweza ukalipokea usikubali. Kwa hivyo, nashukuru kwa kuniambia amelipokea na naamini kwamba amelikubali.

Lakini katika hapo nataka niseme kwamba katika mipango yetu, kwa sababu suala hili halitakuwa ni la leo na kesho, lithahitaji maandalizi na maandalizi hadi kukamilika kwake yatahitaji muda, basi angalau hatua ya kwanza ametuambia, lakini tungefurahi zaidi kwa sababu bajeti hii ndio katuambia ametupokea, basi tunaamini kwamba bajeti ya mwakani angalau angesema tuko mbioni, na bajeti nyengine tunaanza mchakato wa jengo. Maana yake kama Wawakilishi tunahitaji kuona kitu kikisogea kuelekea mbele. Lakini ukituambia tu kijumla jumla, kwa kweli tutakuwa hatufahamu.

Kwa hivyo, nashukuru kwamba angalau amepokea, na naamini bajeti ya mwakani atasema kwamba amekubali bajeti, na bajeti ya mwaka ujao atasema wanaanza mchakato, kitu kama hicho angalau kutupa matumaini, ili siku moja tuone kwamba Pemba kunakuwa na *ICU*.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, tuendelee.

Mhe. Omar Ali Shehe: Ndio nasema, kwa vile keshapokea na kukubali kwa hivyo tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilisema kuna kilio kikubwa sana Pemba cha madaktari. Je, kuna hatua gani ya dharura ya kupelekwa kule na baadhi ya wagonjwa wakatolewa kule na kuletwa hapa na matibabu yenyewe ni dhiki. Mhe. Waziri naomba anisaidie.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Jaku, kuna Waheshimiwa wengi kutoka Pemba walilitaja suala hili la madaktari. Suala hili la madaktari kwa kweli tusiseme tutaweza kujitosheleza kwa muda mdogo. Nililiezea kama ni changamoto katika wizara, lakini hata mara hii nimeshaambiwa kamati yangu ya *deployment* ni kwamba katika watoto waliomaliza Mbweni mara hii, 71 wanapelekwa Pemba. Mhe. Mwenyekiti, ni kawaida sana kukuambia mbona wewe hili hufanyi. Waheshimiwa hawa hawa mwaka jana niliwaambia, moja katika tatizo la vijana wanaotoka Unguja wakija Pemba hawana pa kukaa. Wakanipa ahadi lukuki hapa, kwamba wewe walete tu tutawapatia nyumba. Walipokwenda vijana hawana pa kukaa, ikarudi *bill* sisi tulipe wizara, wakati tulitegemea watatusaidia katika kulikabili suala hili.

Kwa hivyo tunaomba na wao watusaidie katika mashirikiano ya kutatua tatizo hili, isiwe hakuna tulettee. Sawa, nakuletea lakini basi tusaidie angalau pa kukaa, ile lawama ya kwamba wengine wamerudi ni kwa sababu wameshindwa na pa kukaa, wengine wakikaa chumba watu watatu na Mhe. Mkasha akalazimika kuchukua fungu lake la OC kukodi nyumba, wakati ahadi ya Wawakilishi ilikuwa watatusaidia. Kwa hivyo, tutaendelea kulipunguza suala hilo kila haja inapokuwepo. Wanaotoka nje baada ya kurudi masomoni, wakija wanaostahiki tutawapeleka Pemba. Sasa hivi nashukuru nina *deployment committee*, ambayo inashirikisha wote kutoka Pemba na kutoka Unguja, wanakaa pamoja wanatizama wapi ni *serious*, wanasema hapa tupeleke, sio suala la mtu mmoja sasa na bahati nzuri waziri wala siingilii wanamaliza wenyewe wataalamu, wakishamaliza mimi wananiarifu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tuendeleo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia kwa sauti kubwa nilizungumzia katika hospitali ya Chake Chake, lakini sasa hivi nitajitahidi kwa sauti ndogo sana, nipate ufafanuzi juu ya mambo yafuatayo. Pamoja na Mhe. Naibu Waziri kunijibu kwamba masponji yale mia yaliyotolewa na mfadhili, hayajawekwa kutumika kwa sababu hayajatiwa kava. Lakini hakunijibu ile hoja yangu ya msingi kwamba ilikuaje masponji yale pamoja na kwamba hayajatiwa kava, yasifae kwa wagonjwa lakini yafae kwa watu wa mwenge. Hoja hii hakujibu Mhe. Naibu Waziri.

Vile vile nilizungumzia madaktari na wafanyakazi wengine pale Chake Chake jinsi wanavyolipwa *night call*. Mtu anaweza kufanya *night call* siku 14, 20 mpaka 30, lakini akalipwa siku 10 tu tena baada ya miezi sita. Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili mtaliondoa lini jamani, ni tatizo na tunawavunja moyo madaktari, halafu wakiondoka kule Pemba tuanze kunung'unika kwa sababu hamuwashughulikii.

Kwa hivyo, naomba nipatiwe ufafanuzi wa kutosha kwamba ni lini hawa madaktari pamoja na wafanyakazi stahiki zao wanapotoka usiku kwenda kutibu wagonjwa watalipwa kwa wakati, tena inavyostahiki kwa mujibu wa taaluma zao. Wewe unamchukua *MO* anakwenda kutibu unampa shilingi 2,000/- inakuwaje? Naomba ufafanuzi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ile hoja ya kwanza ya magodoro sijaifahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja ya kwanza ni ya magodoro yamepelekwa kwenye mwenge.

Mhe. Waziri wa Afya: Kwenye mwenge?

Mhe. Mwenyekiti: Eeh. Au sivyo Mhe. Mjumbe (*Makofi/Vicheko*).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba nifafanue zaidi, labda Mhe. Waziri hoja zimemzidi hizi alizopewa, hivyo naomba hii aisikilize vizuri zaidi. Kuna mfadhili sikuwahi kumtaja jina lake, ametoa masponji, baada ya kwenda pale hospitali ya Chake Chake akaona vile visponji vimemaliza, basi akatoa masponji 100. Mhe. Mwenyekiti, masponji 100 yale yanafika karibu miezi sita nyuma, wagonjwa hawajatandikiwa kwa sababu serikali mlitakiwa muweke *plastic cover* juu, ili yasidondokewe na mambo mengine.

Sasa wakati tunasubiri serikali iweke *plastic cover*, juzi ulipokwenda mwenge, yale hawakuweza kulalia wagonjwa, lakini watu wa mwenge wanalalia. Kwa nini mufanye hivyo na yale hayakutolewa kwa watu wa mwenge, yalitolewa kwa wagonjwa. Hiyo ndio hoja yangu ya mwanzo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, taarifa niliyopewa na watendaji wangu kutoka Pemba, ni vile ambavyo Mhe. Naibu Waziri wangu amejibu. Ni kwamba masponji haya tutayatumia, lakini kwa sababu masponji haya hayakukusudiwa, basi yanahitaji yatiwe kava. Sasa kama kuna mmoja kayachukua na kuyapeleka kwenye mwenge. Sisi hatuna taarifa hiyo, na kama hilo limetokea basi tatalifuatilia ili tujue nani kafanya hivyo na suala la nidhamu litachukuliwa.

Suala la pili la *night call* nimeeleza kwa urefu kwamba jamani, tumeanza kuwalipa madaktari *night calls* zao na hao waliolipwa ni pamoja na madaktari wa Pemba. Waliobaki wengine tumekubaliana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuanzia mwaka huu ambao leo mtanipa pesa, tulifanye suala hilo kwa pamoja, na nimeunda kamati inayoshirikisha kila kundi, wakiwemo *orderly*, *ma-nurse*, madaktari na wafanyakazi wengine ambao nao ni lazima wawe wanaonekana kwamba wanawasaidia hao madaktari. Kwa hivyo linashughulikiwa Mhe. Mjumbe na ni mwaka huu, mwaka ule ndio umeshapita.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya kazi zetu sisi Wawakilishi ni pamoja na kuangalia matumizi mazuri ya *public assets*, sio tu waje hapa waombe pesa tukawapitishia, sio hiyo tu kazi yetu. Ni pamoja na kuangalia matumizi mazuri ya *public assets*. Kwa sababu mfadhili ameshapeleka masponji, tena pamoja na yale *ma-double sheet* kwa kila kitanda.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba juzi nilipita pale Hospitali ya Chake Chake hayapo wala yale mashuka hayapo. Je, kabla sijakubali kuwa tuendeleo, Waziri anaweza kuniambia ni lini zitawekwa zile *plastic covers*, pamoja na yale mashuka kwa kila kitanda zilizotolewa na mfadhili, mashuka mawili mawili kwa kila kitanda kwa wagonjwa. Kwa sababu nilipopita juzi wana vishuka vingine vinafika vitovuni na wengine hawana kabisa namna hii.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja umeiongeza hiyo, lakini kwa faida ya wote, Mhe. Waziri msaidie.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hoja ipi ya magodoro bado.

Mhe. Mwenyekiti: Ya magodoro eeh.

Mhe. Waziri wa Afya: Nilisha ahidi kwamba nitalifuatilia na atakayehusika nitamchukulia adhabu.

Mhe. Mwenyekiti: Ya *cover*, sasa anauliza ni lini yatatiwa hiyo *cover*.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, sasa kusema lini nitamdanganya tena. Nitalifuatilia baada ya bajeti na niko tayari kufuatana na yeye kwenda kusimamia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, hii bajeti ya Wizara ya Afya ni ya kwangu. Nataka sana niunge mkono na kuipitisha hapa. Lakini vile vile nimechaguliwa na wananchi na walipa kodi wa nchi hii na hizi ni pamoja na kero zangu.

Kwa hivyo, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendeleo.

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	66,000,000
--------------	-----------------	------------

Kifungu 0401	Idara ya Mipango	
--------------	------------------	--

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa wema ulionitendea sasa hivi. Kwa kuwa nimepewa majibu ya wakati nilipokuwa nikichangia, nilikuwa nikichangia hospitali ya Jimbo la Mpendae ambapo hospitali ile inataka kumalizwa, lakini pamoja na maelezo mazuri aliyonipa Mhe. Waziri, bado nilikuwa nataka kujua, kuwa ile hospitali ni ya serikali, ili iweze kutukabidhi na wananchi wafaidike na huduma ile kuondoa msongamano pale Hospitali ya Mnazi Mmoja au ni ya watu binafsi. Nataka kupata maelezo kidogo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hospitali ile ni ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Hospitali ni ya Serikali.

Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka sasa kujua ni kwamba tulitaka sisi tukabidhiwe ile hospitali mimi pamoja na Mhe. Mbunge kuweza kujenga wakati serikali haina pesa za kujenga. Sasa mpaka sasa hivi hatujakabidhiwa hospitali ile na katika maelezo yake Mhe. Waziri amesema pana kikundi kidogo kinazuia. Hebu kwa faida ya wananchi naomba aeleze ili wananchi wangu wa Jimbo la Mpendae wapate kujua, ni faida gani ambayo

serikali inashindwa sasa na kikundi kidogo kuchukua hospitali ile ikatukabidhi sisi. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa najibu nilieleza, kwamba waliokuwa wanahusika kwenye jimbo ni wale ambao Mbunge aliyepita aliona hiyo hospitali na aliwakabidhi. Mimi kama mtu mwenye uzoefu wa utawala, niliona nipate taratibu za utawala, huwezi kuingia nyumbani kwa watu bila hodi. Ndio maana nikaona niwaone Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na wanaohusika ili tulimalize kwa taratibu za kiutawala.

Lakini kwa sababu sasa mwaka umepita, na wote wanaohusika wana habari. Maana hata huyo aliyekuwa Mbunge vile vile alishaitwa nyumba kubwa akaelezwa hivyo, kwamba mwakani suala hili nitalimaliza kama Waziri. Kwa hivyo, kama kuna mtu ana kikundi tutakutana chini ya Mkunazi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri sana ya Mhe. Waziri, lakini bado sikubaliani na yeye kwa nini mpaka leo hatujakabidhiwa hichi kitu na wakati ni cha serikali, kwa nini serikali ishindwe na kikundi kidogo cha watu ambao wanaweza kulishikilia. Mimi naomba maelezo ili niweze kuridhika na suala hili.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kama alivyosema Mhe. Waziri wa Afya kwamba, hii hospitali ni hospitali ya serikali, na sidhani kama kuna umuhimu tena au kuna kikundi cha watu ambao wao wanataka ku-*argue* kwamba ni ya kwao. La msingi ni kwamba sisi tushirikiane na uongozi wa Jimbo uliopo ili serikali tuweze kutekeleza yale majukumu yetu na kuendelea kuikamilisha ili kuweza kuwahudumia wananchi. Hakuna njia nyengine. Tushirikiane na uongozi uliopo ili tuweze kufanya kazi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo ameyatoa hapa, pamoja na kwamba mwaka jana niliahidiwa ni kipindi kabla hatujafika bajeti hii hospitali hii itajengwa. Sasa naomba niambiwe ni lini hospitali hii itajengwa au nitakabidhiwa ili tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani Mhe. Waziri kasema vizuri, kwamba mtashirikiana na uongozi wa serikali na uongozi wa Jimbo kusimamia ujenji kwa kipindi tunachokwenda nacho.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, *concern* yangu iko hapa kwamba, ni lini tutapewa au tutashirikiana naye, kwa sababu *time limit*,

nipewe *time frame* ni lini. Kwa sababu naweza kuambiwa itajengwa. Mwaka jana niliambiwa kabla haijeshwa bajeti hii na *Hansard* ninazo hapa. Kabla haijaingia bajeti ya mwaka huu hospitali ile itakuwa imejengwa. Sasa bado naambiwa kama mtoto wa kuku kesho au keshokutwa sikubaliani naye. Naomba maelezo ya ziada ili niridhike.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimueleze tu Mhe. Mwakilishi kwamba tumalize au tupitishaje bajeti hii, sisi Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tukishirikiana na Wizara ya Afya, tuite uongozi wa Jimbo na uongozi wa Mkoa tupange ratiba, ili tuone bajeti tuliyonayo, halafu tuanze kuiendeleza hospitali hii. Kwa sababu kukamilika kwa hospitali hii kwanza kutakuwa kuna faida nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, faida ya kwanza ni kupunguza idadi ya watu wanaokwenda katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini faida ya pili wananchi wa jimbo lile la Mpendae watafaidika kwa sababu watakwenda katika hospitali ambayo iko katika masafa mafupi. Ushauri wangu ni kwamba Mhe. Mwakilishi atuvumilie ili tumalize bajeti hii, tutaitisha kikao cha pamoja, tuandae programu ya pamoja ili tuweze kulikamilisha hili jengo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake mazuri sana. Kwa kuwa hospitali ile haitibu wananchi wa Mpendae peke yake ni pamoja na vitongoji vyake, Tomondo, Kwarara na mpaka kwengine, na ni hospitali kubwa kabisa. Kwa heshima kubwa sasa nasema tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba kidogo alipokuwa akijaribu kuchangia Mhe. Naibu Waziri katika kunijibu hoja yangu ya vifaa vya uchunguzi wa saratani, akatoa barua ya kueleza kuwa vile vyombo vilikuwa vimekwaruzika. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kusema hivi, naomba kidogo Mhe. Mwenyekiti, ninukuu *Hansard* inasema hivi.

“Mhe. Naibu Spika, wakati walipofungua hao wenyewe vifaa kutaka kuvifunga, wakakuta baadhi ya vifaa havimo, wakaandika barua kuwaambia jamani humu kuna vitu vimepungua”. Hilo moja.

Lakini la pili, hiyo hiyo *Hansard*, anasema tena Naibu Waziri,

“Kwa maneno niliyoyasikia jana alipopigiwa simu mwenyewe, huyo bwana akasema wiki ijayo vigae vitatoka Dar es Salaam vitakuja na kuwekwa pale”.

Mhe. Mwenyekiti, *Hansard* hii sikuandika mimi Mshimba. Kwa hivyo, mimi ningependa ili niridhike na haya maneno ya Mhe. Waziri wangu madudu, maana yake amesema Waziri madudu na mimi nakubali hivyo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikuoneshe picha ambazo niambie vitu vilivyokuwa *steel*, halafu uniambie vinakwaruzika. Hichi ndio kitu ambacho nashangaa. Mhe. Mwenyekiti, picha hizi hapa na kuna vitu ambavyo vimekuwa pungufu. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri anieleze, je nikubaliane naye hivyo hivyo kuwa vimekwaruzika, na kama vimekwaruzika haoni kama anakubali kuwa wizara yake au watu wanaohusika ni wazembe au kapigwa changa la macho. Mimi naomba anifahamishe hapo tu ili niweze kupitisha bajeti hii.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kujulikana kuwa havimo vimepungua, mawasiliano na wahusika yamefanyika na wameahidi kwamba watavileta. Tatizo ni kwamba ilielezwa wiki mbili. Siku zote nasema hapa sio Juma Duni vua kofia vaa. Ni masuala ya utaratibu wa utawala. Lakini hivi vitu tumeahidiwa vitakuja, na wametuhidi wenyewe vitakuja. Suala la kwamba vimekwaruzika, mimi na Mhe. Mshimba hatuwezi kuviona maana ni kitaalamu.

Kwa hivyo, kama waitwe wataalamu waje waweke *screen*, aoneshwe ule mkwaruzo ndio huu, ndio ataamini, hilo sina jibu. Lakini ni mambo ya kitaalamu, hiki ukikiweka *screen* itakuwa hatupati picha nzuri. Kama vile *screen* ya kompyuta inapovunjia ukaingia ule wino, basi huoni yale maneno hata kama ile kompyuta inaeleza. Sasa ile imelezwa kitaalamu kwamba hii *screen* imekwaruzika itafutwe nyengine na hivi vifaa navyo tutavileta. Sasa hilo tumeahidiwa kwa maandishi na ndio maana na sisi tukamwambia vitakuja, sasa lipi zaidi tumueleze, mimi sina utalamu huo. Kama ni lazima ashiriki kwenye kutizama kwamba *screen* imechunika, basi tuko tayari tuwaite hao wataalamu waje wamuambie hii haifai, lakini vyenginevyo maelezo tunayoweza kumwambia ni haya.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Babu yangu Waziri wangu, sitaki niwe mkaidi sana. Mimi cheo changu ni *professional*. Nataka nikuambie, kuna taaluma nyingi. Nimesema kuna kitu kinakuwa *steel*, hata wewe Mhe. Mwenyekiti, kama utaviona. Sasa mimi nataka anichagulie kauli moja tu, ili nisikupotezee muda babu yangu, kwa babu namuheshimu. Chombo hiki *steel* yake ananiambia vimekwaruzika na wakati kimo ndani ya *package*. Hebu tuoneshe jamani, hebu mimi anikubalie tu na akishakubali basi mimi nitamuambia Mhe. Waziri basi tuendele umekwisha mchezo, kwa sababu ni kitu ambacho kinanishangaza mimi. Aniambie vimekwaruzika au vimepungua. Kwa sababu nina orodha ya vitu ambavyo vimepungua ninavyo.

Kwa hivyo, mimi anijulishe moja tu babu yangu ili niweze kumrahisishia leo, na hilo suala la wataalamu akishakubali, mimi niko tayari tuunde hiyo tume sijui, alisema atakuja na wataalamu, niko tayari na mimi niwepo kwa sababu tayari wataalamu wameshakuja kutoka Dar es Salaam yeye mwenyewe hajui, wamekuja pale Muhimbili kuangalia hivyo vitu, yeye hajui. Kwa hivyo, mimi niko tayari.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti,

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu anijibu Waziri sio Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani sio lazima, kwa sababu daktari yeye ana utaalamu zaidi. Kwa hivyo na kanuni pia inaruhusu. Kwa hivyo, daktari tupe majibu. Endelea.

Daktari sema na Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili kutoa ufafanuzi

Mhe. Mwenyekiti: Sauti kidogo ongeza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hii ndio barua aliyoleta, kopi nimepewa na nikaifuatilia. Katika vifaa vilivyoletwa mbali ya vifaa *screen*, kuna vifaa ambavyo ni vya kuchungulia hizo *tissues* zenyewe, kuna *lens* mule. Sizungumzii hayo makopo na madoo. Nazungumzia *lens* zilizoko kwenye zile mashine za kuangalia *tissues*. Barua inasema hivi, naomba kunukuu.

“Considering the length of the time passed after the delivering it is no longer our company’s accountability for this missing part or accessory and scratches”, nasisitiza “scratches”, scratches maana yake ni michubuko au mikwaruzo kwa Kiingereza, sasa sijui kwa lugha nyengine ikoje. “Of the item as mentioned in your letter”.

Hivi ndivyo ilivyoandikwa na huyo bwana, kwamba vile vyenye mikwaruzo kwanza anasema hawajibiki na hili kwa sababu limechukua muda, na nilieleza kuhusu hili kwamba vifaa vililetwa maabara ilikuwa inatengenezwa, kwa hivyo havikuweza kuwa *installed for the right time*. Walipomaliza maabara

muda wa ku- *install* umemalizika, walipoitwa kuja kuvi- *install* vifaa, ndipo walipokuta vifaa vingine havimo na vingine vimekwaruzika. Wakasema kwa kuwa muda umepita, sisi hatuwajibiki kwa hilo, tunaloweza kuwajibika ni kuhakikisha kwamba tutawaleteeni vifaa vyengine na baadae tuvi-*install*. Hivyo ndivyo walivyosema na ndivyo karatasi inavyosema. Sasa hiyo *scratches* anayosema yeye kwamba sio mkwaruzo, kwa lugha nyengine labda atufahamishe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, sijakubaliana na yeye

Mhe. Mwenyekiti: Barua ya maelekezo ipo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ngoja. Mheshimiwa Barua ya maelekezo na maneno aliyosema yeye humu. Kuna barua yeye kaelekezwa, lakini hii Hansard. Hiyo barua kaelekezwa, hii katamka mwenyewe humu, amekiri. Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, niende wapi. Tuundeni tume sasa tukahakikishe, kifungu nambari 120 ili tukajiridhishe. Kwa sababu mimi nilikuwa nimeshamaliza, achague lugha moja tu anijibu, yeye anakwenda kunisomea yale yale madudu. Kwa sababu anasema yeye kaletewa barua. Mimi nawaambia hivi vitu nani kipofu, hebu niambieni, ina maana sisi tumekubali utumbo kama huu. Maana tukubaliane kitu cha msingi, mimi nilikuwa nimeshamaliza, lakini ile barua yake ndio imezidi kumuangamiza.

Mimi nilikuwa nimeshamaliza Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu humu muna lugha yake mwenyewe na yeye ni *professional* ni daktari. Ndio maana nikasema Mhe. Mwenyekiti, tutazidiana vyeo humu na mimi sijui Kiingereza, *no speaking English*, lakini Kiswahili yes. Kiswahili ni lugha yangu hii humu ndiyo ilivyoandikwa na yeye kaandika humu. Kwa hivyo, hii ni Hansard afute Hansard yake aweke sawa, moja akubali.

Mhe. Mwenyekiti: Nasema hivi, nadhani hamkupishana sana. Waziri kakubali muende mkatizame vifaa na vitakavyoletwa mtshirikiana na wataalamu tatizo liko wapi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Umemaliza.

Mhe. Mwenyekiti: Eee. Mimi nimemaliza.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningekubali kama angekwenda moja kwa moja. Yeye mwenyewe tu. Ndio maana nikapinga pale mwanzo. Lakini ukamnyanyua na kumwambia aendelee. Lakini hukufahamu kumbe kumnyanyua ndio umemzamisha. Nilikuwa

nimeshakubaliana naye aende sambamba na mimi Mhe. Mwenyekiti, ndio utaratibu ulivyo. Kwa hivyo, naomba anijibu Mhe. Waziri ili nimalizane na yeye.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, na iundwe tume. Iundwe tume ili ikachunguze.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani bado, kwa sababu mlikuwa mmeshakubaliana tume ya nini tena.

Mhe. Waziri wa Afya: Aah si anakataa.

Mhe. Mwenyekiti: hapana, yeye kasema kama hamkuelewana na mlikuwa mmeshaelewana. Kwa hivyo, anataka jibu lako tu kwamba vikifika muende mkaangalie pamoja na wataalamu mambo yemekwisha.

Mhe. Waziri wa Afya: Aaa, nilifikiri anashikilia kuundwa tume, ndio maana nikakubali.

Mhe. Mwenyekiti: hapana, hakuna tume. Kwa hivyo, mwambie tu kwamba vitakapofika, wewe utashirikishwa, utaangalia na wataalamu hayo matatizo utaoneshwa itakuwa kazi imekwisha.

Mhe. Waziri wa Afya: Sawa Mhe. Mwenyekiti, nakubali.

Mhe. Mwenyekiti: Umemsikia Waziri, kakubali hivyo ulivyomshauri kwamba na wewe utashirikishwa, mtakwenda kuangalia vilivyoletwa na hivyo vitu vilivyoathirika utaoneshwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, sitaki kufanya tabu. Nikushukuru tu na wewe kwa taaluma zako na kama nilivyosema babu Waziri amekubali, kwa hiyo tume, ina maana hii Hansard haijafutika bado itasimama pale pale. Nakubaliana na babu itakapokuja hiyo tume na mimi nishirikishwe, ili niende nikahakikishe kama vitu vimekwaruzika, halafu kikao chengine tutakuja. Tuendeleo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, wakati nilipokuwa nikichangia. Sasa hivi tupo Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Wakati nilipokuwa nikichangia hoja, niliuliza kuhusu *legal status* ya *public health laboratory* iliyoko Wawi Pemba.

Namshukuru sana Mhe. Waziri amejibu kwamba ameiona hiyo *concern* na wataishughulikia. Lakini kwa sababu kuna masikitiko kwamba kutokana na

kutokuwa wazi ile taasisi baadhi ya misaada mingi inakosekana kutokana na kwamba haiko katika *legal status*.

Namuomba Mhe. Waziri atueleze ni lini wataanza mchakato wakishirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, ili kuhakikisha kwamba ndani ya bajeti hii mwaka 2012/2013. Sheria ile inafikishwa katika Baraza la Wawakilishi ili taasisi ile iweze kuwepo kisheria. Ni nili utanza mchakato huo naomba Mhe. Waziri anieleze.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mchakato utanza baada ya kumalizika bajeti

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Namshuru Mhe. Waziri lakini naomba atueleze kuwa ipo tamaa ya katika bajeti hii yaani mwaka huu 2012/2013 kuhudhurishwa katika Baraza Sheria hiyo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Pamoja na majibu aliyotoa Mhe. Waziri naomba kidogo kuongezea majibu ili kumsaidia Mhe. Rashid Seif. Naelewa *concern* yake kuhusiana na taasisi ile kwa sasa hivi inavyoendesha. Naomba akumbuke kwamba ile taasisi kuna watu ambao sio wa Serikali na ambao wana maslahi katika taasisi ile yaani *foundation* ambayo ilijenga ile taasisi baada ya kujenga Serikali ikaendesha kwa mashirikiano. Kwa hivyo wao wana sehemu yao na sisi kama Serikali tuna sehemu yetu. Kwa hivyo hatuwezi kusema moja kwa moja tuichukue tuifanye iendeshe chini ya sheria.

Labda nimuahidi na mimi kwamba tutashirikiana na Wizara ya Afya kuangalia mfumo bora ya kuiendesha taasisi ile. Lakini hatuwezi kusema kwamba tutaleta sheria moja kwa moja kwa sababu ile sio taasisi ya Serikali 100% kuna sehemu ambayo bao inashikiliwa na *foundation* ya Wataliana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nimeridhika sana na majibu ya Mhe. Waziri na Mhe. Mwanasheria Mkuu. Nawaombea kheri katika mchakato tunaotaka kuanza.

(*Baraza lilirudia*)

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa kazi yetu ya kupitisha vifungu haijeshwa na muda wetu wa kawaida umekuwa unakaribia kumalizika namuomba Mwanasheria Mkuu atenge kanuni kando ya muda ili tuweze kumaliza shughuli zetu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa vile shughuli iliyopo mbele yetu haijamalizika na kwa sababu muda uliopo wa kumaliza shughuli hii hautotosha naomba Baraza kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likubali kutenga kando Kanuni ya muda hadi hapo tutakapomaliza kupitisha hoja ya Mhe. Waziri wa Afya. Ahsante.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: (Anaendelea) chakula cha wagonjwa pana milioni 24, nilikuwa nataka ufafanuzi hichi chakula cha wagonjwa ni kwa ajili ya Hospitali Kuu Mnazimmoja au zile hospitali za vijiji. Kwa sababu kuendesha hospitali za vijijini naona nako kuna ziro. Hebu atusaidie hapa Mhe. Waziri hapa pana ziro kabisa, hospitali zinajiendeshaji vipi ikiwa pana ziro.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuna suala moja la utaratibu, mimi sina hakika kama Mhe. Mtando alichangia kwenye kifungu hiki sikumbuki kama alichangia. Halafu ameendelea na hivyo vyengine. Ninachokumbuka kifungu alichochangia na kuhoji vilikuwa ni mambo ya Kamati na viburudishaji. Sasa kama hivi hakuchangia katika utaratibu sina hakika. Niko tayari kumjibu lakini ni utaratibu? Muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani kama unao uwezo jibu tu wafahamu na wengine.

Mhe. Waziri wa Afya: Kupungua kwa matumizi kunategemea na *activities* na *activities* hizi nimesema zina *reflect* na MTEF. Nakumbuka hapa jana walisema Waheshimiwa kwamba ni vizuri mwakani wakashirikishwa kwenye MTEF. Kule ndio tunaeleza kwa nini zipungue au ziongezeke. Shughuli hizi hii ni idara ya tiba *it means* kwa eneo hili *activities* zimepungua ndio maana mahitaji hayakuwa makubwa. Kule kwengine ilikoongezeka ni aidha kwamba zilizotolewa mwaka jana hazikutosha au *activities* zimeongezeka.

Kwa mfano hapa vifaa vya usafishaji wajumbe wote hapa waliochangia wanatwambia tunanuka, tunaongezewa vipesa tusafishe, mnatwambia vingi. Sasa jamani tusikilize lipi?

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, bado sijapata maelezo mazuri kutoka kwa Mhe. Waziri, sjaridhika nayo kwa kweli hasa katika hili fungu la gharama za mafuta na vilainisho. Hoja yangu nilianza na hapo kwamba ukiangalia hapa gharama za petrol ni milioni moja na laki sita (1,600,000) kwa mwaka mzima, ukipiga hesabu ya haraka haraka ni mafuta kidogo mno. Mwaka jana tulikuwa tuna bajeti ya milioni 5 na zaidi.

Sasa ndio maana nilikuwa nauliza sababu kutokana na kuwa hii ni Idara nzima Idara ya Tiba. Mimi nilitegemea kutokana na huu upandaji wa mafuta hili fungu litakuwa linaongezeka badala yake limeshuka mara dufu kabisa. Ndio maana nimepata wasi wasi Mhe. Mwenyekiti, kwa nini isiwe inapanda ishuke, sasa nilikuwa nataka maelezo ya ziada kwa nini ishuke kiasi hichi, kutoka milioni tano mpaka milioni moja.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Kanuni ya 98 inatueleza vizuri kuhusiana na sula hili. Nilitegemea Mhe. Mtando angesema kwanza kama kweli alichangia na kweli alitoa indhari ya kuondoa shilingi kama inavyotuongoza kanuni ya 98 lakini hakufanya hivyo. Nadhani tunavifungu vingi vya kupitisha.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tungehesimu kanuni zetu tungeendelea na hoja nyengine sio hii ya Mhe. Mtando.

Mhe. Waziri wa Afya: Mheshimiwa lazima tuseme kweli watu wa Idara ya Tiba hawana hata hiyo gari ya utawala hawana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kama hii Idara haina hata gari, sasa haya yaliyotiwa ya kazi gani, haya mafuta yaliyowekwa ya kazi gani kama haina hata gari. Basi si bora tuyaondoshe yote au tuyafute tu yote iwe ziro, ziro.

Mhe. Mwenyekiti: Wameweka hakiba huenda wakaazimwa pahala. (*Vicheko*)

Kifungu 0701	Idara ya Tiba Unguja	shs 435,000,000
Kifungu 0801	Idara ya Tiba Pemba	shs 213,000,000
Kifungu 0901	Idara ya Kinga Pemba	shs 99,000,000
Kifungu 1401	Mkemia Mkuu wa Serikali Unguja	

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia Idara ya Mkemia Mkuu nilisema ni *sensitive area* au ni *sensitive laboratory* ambayo iko pale na vitu vya hatari na vingi ambavyo vinaweza kuchunguzwa katika Idara ile. Lakini sikupata maelezo mazuri kwa sababu

kifungu hichi kimetiwa pesa kidogo kwa idara ile. Si kukaribisha rushwa katika Wizara ile. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi mwaka uliopita kilipata milioni 50 mara hii kimepata milioni 99 na hizi ni za utawala mbali ya mradi ambao unaendelea Maruhubi. Kwa hivyo limeongezeka fungu kutizama na hali ilivyo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru nilipokuwa nikichangia niliuliza swali kwamba hii Idara ya Mkemia Mkuu mbali ya Mkemia Mkuu Mwenyewe kuna wafanyakazi wangapi waliokuwa si wa utawala katika Idara ile, lakini sikupata jawabu katika maelezo ya Mhe. Waziri najua alikuwa ana mengi. Namuomba anambie.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nasikitika kwamba sikuweza kujibu kwa kukimbilia muda lakini jibu lipo. Kuna wafanyakazi wasiopungua 5 ambao ni wataalamu mali ya wale watawala. Alitaka vile vile ajue kwamba je, wanakwenda kwenye mpango wa mafunzo, wamepangiwa mafunzo. Katika hao *infact* wapo 12, wale 5 wa *labor* na 7 wanaofanya uchunguzi mbali ya wale wa utawala na kuna mpango maalum kila miezi mitatu wanakwenda kwenye mafunzo ya kujiendeleza. Mhe. Mkemia Mkuu amepangiwa ratiba kwenda *Turky* na kwenda Misri, kwenda kujifunza maendeleo ya vitengo kwa shughuli hii.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nashukuru Mhe, Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 1401 Mkemia Mkuu wa Serikali Unguja shs 99,000,000
Kifungu 1501

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia hapa nilikwenda kwenye hichi kiambatanisho Nam. 10 ambacho kinaonesha hali halisi ya wafanyakazi katika Hospitali ya Mnazimmoja, tumeona kuwa hospitali hii ina mapungufu ya wafanyakazi wasiopungua 383. Tumeona kuna kada 11 zenye wafanyakazi 168 hazina hata mmoja, niliuliza, kwa sababu hii ndio Hospitali Kuu ya Zanzibar na hali yake ndio kama hii. Nilitaka kujua kwa zile kada ambazo hazina mfanyakazi hata mmoja wanapotokea wagonjwa wanatibiwa vipi wakati hospitali haina mfanyakazi hata mmoja. Hapo naona sikupata jibu la kuridhisha naomba nipewe maelezo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu kama hivi narudia tena sikuweza kujibu swali kwa swali kwa sababu ya kunusuru muda.

Ni kweli kuna idara ma- *specialist* hawapo lakini moja katika utaratibu wa madaktari, kuna daktari wanaosoma masomo yote kwanza kabla hawaja *specialize*. Kwa hivyo mgonjwa yoyote wanapokuja wanamfanyia uchunguzi na wakishajua maradhi haya hawana utaalumu nayo ndipo yanapokuwa *referred*. Ndio maana sasa tukawa tunapeleka Dar-es-Salaam ambapo kuna wataalamu au tunawapeleka India.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nauliza tena kutokana na hilo jibu lake ndio kada zote zile ambazo hazina daktari hata mmoja ndio wamo kutokana na hivyo alivyoeleza. Yaani kuna madaktari 168 hata mmoja hayupo ndio hao anaosema kuna *specialist* wa mambo yote ndio wanaingia katika sehemu zote au kuna sehemu nyengine hazina hata mmoja hasa.

Mhe. Waziri wa Afya: Mheshimiwa narudia tena kuna madaktari wanaopata *general practioner* wanaitwa *internal medicine* hao sio lazima kuwe na vitengo na sisi tumekusudia kufungua vitengo vyengine ambavyo hivi sasa hata kuwepo havipo. Maana yake kuwa hakipo maana yake *specialist* hata mmoja hayupo. Kwa hivyo, hilo tunalifahamu na ndio maana tukasema tunaendelea kutayarisha vitengo ili Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe Rufa kwa sababu vyengine havipo. Sasa vikiwa havipo ndio tunataka kuviunda kuna vile vya moyo, kuna vile vya *dialysis* ya matatizo ya mkojo. Kuna matatizo ya mapatu. Vyengine hivyo haina wataalamu lakini mgonjwa anatambulikana kama huyu ana matatizo ya *dialysis* kwa wale madaktari waliokuwepo sasa. Baada ya hapo ndio tunapeleka kunako wataalamu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mheshimiwa jibu ndio hilo hilo. Tuendeleo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Nilipokuwa nikiichangia Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia suala la uhaba wa wafanyakazi katika *hospital* hii. Ingawa hoja yangu ilikuwa tofauti kidogo na ya mjumbe ambaye amemaliza hoja yake.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema katika hotuba ya Waziri alitwambia wanahitaji wafanyakazi 502 walioomba kuajiriwa ili kuiwezesha Wizara kuweza kukamilisha mahitaji yake hasa katika *Hospital* hii Kuu ya Mnazimmoja. Jana niliomba katika mchango wangu kwamba Serikali kwasababu inawajibika kwa pamoja, kupitia Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, itoe *commitment* ya kusema mahitaji haya ya wafanyakazi 502 kutokana na umuhimu na uzito wa sekta hii ya afya kwamba Serikali inatoa *commitment* kwamba itamruhusu Waziri wa Afya aweze kuwapata watu hao. Mhe. Waziri hayupo sasa nilikuwa naomba kwa uzito wa sekta hii na inavyowagusa wananchi. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atupe ahadi hapa kwamba Serikali itaridhia kuwaajiri wafanyakazi 502 wa Wazira ya Afya, ili

Hospitali ya Mnazimmoja na Hospitali nyengine ziweze kujitosheleza kwa wafanyakazi zifikie malengo ya kutoa huduma zinazostahiki kutoka kwa wananchi wenyewe. Naomba *commitment* ya Serikali ili tuendelee.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Jussa swali lake la kuajiriwa wafanyakazi wa afya. Kwanza tumepewa hiyo nafasi ya 502. Lakini kwenye hotuba yangu nilisema kwamba Waziri wa Utumishi, tulipokuwa katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi na nimetaja kwenye hotuba yangu. Kaambiwa kwamba hakuna sababu yoyote atakapokuja Waziri wa Afya kuajiri madaktari au wataalamu wa afya kukawa na kisingizio chochote. Imekuwa kama tumepewa *blanket* ni suala la kuwapata tu. Kama watakuwepo tukipeleka Mhe. Haji Omar Kheri hawezi tena kuzuwia na Waziri wa Fedha nasikia na visenti vilishatengwa.

Kwa hivyo nategemea haihitaji *commitment* ya Makamo wa Pili wa Rais ni kwamba Waziri na Baraza la Mapinduzi limesha agiza Waziri husika kwamba asitafute visingizio vya kuzuia madaktari kuzuiwa Wizara ya Afya. Nadhani hilo ndio jibu halisi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, labda Waziri wa Afya anisaidie zaidi. Kwa sababu majibu yake nimeyasikia. Tukisema madaktari na wataalamu wa sekta ya afya inaweza kuwa hajumuishi mahitaji ya wafanyakazi ambao wengine wanahitajika, kama alivyozungumza katika hotuba yake kwa usafi na mambo ya maeneo mengine. Kwa sababu nadhani kuna tofauti baina ya madaktari na wataalamu wa sekta ya afya na hao wanaotoa huduma nyengine. Kama atanambia kwamba hiyo *blanket* alilopewa na Baraza la Mapinduzi linajumuisha wafanyakazi wote wa sekta ya afya anaowahitaji na kwamba ndio tunaichukua ndio *commitment* ya Serikali na mimi nitalichukua hilo na nitakubali kwa sababu nitapata nafasi ya kuja kumuhoji tena tukijaaliwa mwakani. Kwa hivyo naomba anisaidie tu kwamba je, maana yake siamini kwamba tunahitaji madaktari 502 au wataalamu wa afya 502. Mimi naamini ile ilikuwa ni jumla ya mahitaji yote.

Sasa kama hiyo *approval* aliyopewa inajumuisha wote sina matatizo, nitasema sasa hivi tuendelee Mwenyekiti nikae kitako. Lakini kama hajumuishi naitaka *commitment* ya Serikali kwa sababu sekta hii ili uhudumie haitaji madaktari na wataalamu tu, lakini wanaotoa huduma nyengine katika sekta hii kuwasaidia hao madaktari na wataalamu. Ahsante sana Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu na katika hili 502 kuna kila *category* sio aina moja tu ya wafanyakazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kafanya haraka kukujibu, hakunifahamu. Mimi nimefahamu kwamba 502 inajumuisha wote. Hoja yangu ilikuwa ridhaa, idhini iliyotolewa na Baraza la Mapinduzi kwa Mhe. Haji Omar Kheri kwamba wote watakaokwenda asipata visingizio. Inajumuisha wote kwa sababu katika majibu yake ya awali kataja madaktari na wataalamu wa Sekta ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nasema inajumuisha wote hiyo *approval* ya Baraza la Mapinduzi, ikiwa hiyo *approval* ipo na idhini hiyo ipo kwa wote 502 watakaohitajika sina matatizo. Lakini kama inahusu madaktari na wataalamu wa Afya tu bado nitakuwa sijaridhika Mhe. Mwenyekiti. Naomba nataka kauli yake.

Mhe. Waziri wa Afya: Narudia tena Mheshimiwa katika 502 tuliopewa kuna madaktari, kuna manesi, kuna *assistance medical officer*, kuna *orderly*, kuna hata wale wababa magunia pale *pharmacy*.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendeleo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika Hospitali ya Mnazimmoja nilitaja baadhi ya vifaa au mazingira ya Hospitali ya Mnazimmoja ikiwemo *lamp operation*, *floor*, vyoo na *floor* iliyokuwepo ICU, anataka kunambia ni lini Mhe. Waziri vile vitu vitatiwa hali ya kuwa hazina gharama. Baada ya kukaa mtu akakaa chooni na kumsubiria mwenziwe kama mtu anakuja au haji.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nimesema kama ni suala kutengeneza kila kitu bajeti haitoruhusu kakini kama ni kutengeneza katika hatua tunayoweza kutengeneza, tutatengeneza na tunaendelea kutengeneza hatua kwa hatua. Naomba wajumbe wazingatie kwamba hichi kibahasha chetu cha Mnazimmoja mara hii kidogo kimevimba kidogo kuliko kilivyokuwa kwa miaka ya nyuma na kila siku kinaendelea kuwa kizuri zaidi. Kwa hivyo tutafanya tutakapoweza Mhe. Jaku Hashim na tutahakikisha vile vyoo vibovu visiwe vibovu tena na vyenye kuziba bomba tutavizibua.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hivi vitu havina gharama kubwa na hivi vitu vimeshaka karibu mwaka mmoja na nusu sasa hivi. Kamati tumeshakwenda kukagua milango tu na haipungui milango 15 au 20, watu wanazidi kuteseka Mhe. Mwenyekiti. Mimi anipe kauli ni lini tu, sina tatizo mimi namuheshimu Waziri wangu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mheshimiwa tutatengeneza tukimaliza Bajeti tukipewa fedha tutatengeneza hasa ya ICU.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kutokana ushauri wake sina tatizo Mhe. Mwenyekiti, tuendeleo.

Kifungu 1501	Hospitali Mnazimmoja	Shs 642,000,000
Kifungu 1601	Mkemia Mkuu Pemba	Shs 20,000,000
Kifungu 2001		

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa wakati nikichangia nilielezea wasi wasi wangu juu ya utata uliopo juu ya majukumu kati ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Idara ya Uendeshaji. Nashukuru Mhe. Waziri amejaribu kujibu swali hili. Lakini bado sikuridhika nalo kwa sababu hii ifuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, ukinukuu kitabu cha Mhe. Waziri kifungu 911 utaona kwamba kwa kushirikiana na vitengo husika Wizara kupitia kitengo cha Sheria imeweza kuzipitia sheria mbali mbali zikiwemo sheria ya chakula, dawa na vipodozi na mambo mengineyo yanayofuata hapo na kuandaa sheria nyengine.

Mimi nauliza Mhe. Waziri, wakati Idara ya Mipango Sera na Utafiti ndiyo iliyokabidhiwa mambo yote ya sera na ndivyo ilivyoelezwa. Itakuwaje kuwaje tena sheria ije iandaliwe na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na Uendeshaji. Hapa ndio penye kitendawili. Kwa sababu ile Idara ya Mipango na Sera ina jieleza wasi wasi, kwamba ile ndiyo yenye jukumu kwa wasababu ndio inayopanga sera na ndio jukumu la kufuatilia upatikanaji wa sheria. Sasa hapa kuna mgongano, halafu idara nyengine ya utumishi na ndio inayokabidhiwa mambo ya sheria, huku sera ni watu wengine ambao sera inapatikana mwanzo halafu inapatikana. Hapa kidogo tuna wasi wasi, hebu tueleze Mhe. Waziri namuomba atoe maelezo ya ziada kidogo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikitoa maelezo nilisema kwamba mambo yote yanayohusu usimamizi wa utawala yanafanywa na Idara ya Utumishi na uendeshaji. Kifungu au maafisa wanaohusika na utayarishaji wa sheria kiutawala wapo chini ya Idara ya Uendeshaji na Idara ya Sera na Mipango ni kutayarisha Sera na Mipango. Lakini ukitaka kuishughulikia sheria ni lazima uiende kwenye utawala. Unapotaka kushughulikia masuala ya mipango na sera utakwenda mipango. Hiyo ndivyo tulivyoagizwa na Wizara ya Utumishi na *structure* hizi hapa tumepewa. Labda nazo nisisome. Mheshimiwa Idara ya Utawala ina Division tatu nazo ni:-

- 1) *Administrative Division*
- 2) *Human Resource Division*
- 3) *Record and Management*

Kwenye *Administrative Division* kuna *Office Supervisor, Transport, Estate Management, Maintenance and Store*.

Kwenye *Human Resource Division* kuna *Resources Plan, Training Development, Remuneration and Kalamazuu*

Kwenye *Record ni Confusion Registry, General Registry and Record Center*. Kiutawala sehemu ya Maofisa wa Sheria wanasimamiwa na Idara ya Utawala. Sasa kama tunaona aende kwenye Sera basi tutashauri Wizara ya Utumishi ikihamishe kifungu hicho. Lakini wakati wote maswali yanayohusu utawala lazima yawe chini ya Idara ya Uendeshaji na Mipango.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, sisi tunapoingia kwenye Kamati huwa tunauliza. Serikali mara hii imekuja na mfumo mpya wa Wizara zote. Kitengo hichi cha Mipango Sera na Utafiti ni kitengo kipya. Sasa tunaomba msaada wa Mwanasheria Mkuu ili atufafanulie kwamba ushughulikiaji wa sheria hasa katika Wizarani utakuwa chini ya Idara gani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati sisi tunavyohusika na Wizara katika utayarishaji wa Sheria sisi tunajua Wizara. Mara nyingi tunawasiliana na Katibu Mkuu, suala la nani anashughulikia ndani ya Wizara ndio *management* ambayo nadhani Mhe. Waziri amelieleza vizuri kwamba huu ni muongozo wa Wizara ya Utumishi na Utawala Bora. Hiyo ndiyo inatoa mifumo ya miundo ya taasisi ndani ya Mawizara. Kwa hivyo nadhani kama alivyosema Mhe. Waziri kama huo ndio muongozo ambao Wizara zote mtapata kutoka kwa Wizara ya Utumishi.

Sasa kama Mhe. Rashid Seif anaona kwamba huo sio mfumo mzuri wa kushughulikia masuala ya sheria basi mawazo yake tutayachukua na sisi tutayazingatia na kushauriana na wenzetu wa utumishi kama kuna haja ya kurekebisha tulirekebisha. Lakini uhusiano zaidi wetu sisi unakuwa ni kwa Wizara kwa kupitia Katibu Mkuu au Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Uendeshaji ndio ambaye tunawasiliana naye mara nyingi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na Mwanasheria Mkuu kwamba tutizame mambo ya baadaye. Lakini utatanishi upo kwa sababu kitengo kile cha Mipango, Sera na Utafiti kimetajwa wazi. Lakini kwa sababu kuna muongozo mwingine tutakuja kuona hizo siku za mbele katika mambo ambayo yatafuatia. Tuendeleo Mheshimiwa.

Mhe. Shawana Bukheti Hassan: Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kuzuia hili fungu nilikuwa nataka maelezo tu ya ziada. Naheshimu sana majibu aliyonijibu Mhe. Waziri, Naibu Waziri, lakini sikufahamu kidogo. Kwa

sababu nimeelezea katika suala zima la vituo vya afya vyote kwa jumla ambavyo tuende navyo lakini hata hivyo nilikuwa nina *specific issue* ya kituo cha Bumbwisudi. Kituo hichi ahadi ilitolewa mbele ya Makamo wa Rais. Nimewafahamu kwa kuwa vituo vyote vya Kianga, Kinuni vyote vitamaliziwa, lakini hichi cha Bumbwisudi ambacho ni cha mwanzo kuliko vyengine vyote. Hichi ndio nataka kauli.

Mimi ninavyosisitiza hili jambo sipendi wenzangu kuwakaba lakini na mimi nimekabwa. Kwa hivyo naomba hapa nitoke na jibu. Kwa sababu ya hii ya jumla kusema tutavijenga, ndio hata baada ya miaka mitano, sita lakini ni lini hasa cha Bumbwisudi vyengine vitafuatia, lakini cha Bumbwisudi. Ningeomba nipate maelezo ili nitoe kauli ya kuruhusu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwamba tulishaahidi kwamba tutakijenga, sasa lilikuwa nini zaidi. Tumesharodhesha vyote vilivyokuwa vimebaki nusu vinataka kumalizwa. Tunachosisitiza watu wasijenge vyengine vilivyokuwepo vinatosha. Lakini vyote vilivyokuwa havijamalizika tutavijenga. Kama kutoa *priority* basi tutampa Bi Shawana aliyekuwa Waziri wetu hapa. Ni baada ya bajeti sasa hivi sina pesa. (*Vicheko*).

Mhe. Shawana Bukheti Hassan: Mhe. Mwenyekiti, kitajengwa baada ya Bajeti, *Ishallah* Mungu akitujaalia leo *Hansard* inaandika bajeti hii leo ndio tunaipitisha na bajeti itakayokuja itarudi tena hapa. Mimi nakubali kwa kuwa nimeambiwa baada ya bajeti, mwanzo nilisema siungi mkono hoja, sasa kwa kuweka sawa *Hansard* sasa hivi naiyunga mkono hoja hii.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kutoa hoja ya mwisho na Ishalla kwa leo pia itakuwa ndio hoja yangu ya mwisho vile vile ya kunyanjuka.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia swali moja *specific* kwa Mhe. Waziri, ndio maana nimeingojea katika Idara hii kwa sababu ndio muhusika. Nilisema kwamba katika vifungu vya Wizara yake, kajitahidi sana na ndio maana leo maswali mengi yanahusu Sera kuhusu masuala ya vifungu vya matumizi. Lakini kasema katika ripoti zilizopita, Kamati ya PAC kwa Baraza la Wawakilishi la Mwezi wa Machi/April katika Wizara ambayo iligundua kwa lugha ya Mheshimiwa Waziri kwamba madudu mengi moja ilikuwa ni Wizara yake. Nilivitaja vifungu mbali mbali pale ambavyo vilikuwa vimeibua maswali na mpaka PAC imekwenda bado hakuna majibu. Yameibuliwa katika ripoti ya Mkaguzi na yameibuliwa katika ripoti ya PAC nikataja mfano kuna matumizi, vifaa ambavyo havikuinzwa kwenye daftari shilingi milioni 12.

Lakini labda nitoe mfano unaoelewika zaidi katika fedha za nje. Kuna pahala kuna kwanza shilingi milioni tano, mradi wa *Zanzibar Control* shilingi milioni tatu, lakini kwenye mradi wa kuzuwika vifo vya mama na watoto kuna malipo yaliokuwa na vilelezo US\$ 35,928. Halafu vile vile katika Mradi wa Afya Kitengo cha Mama na Mtoto malipo yasiokuwa na vilelezo shilingi 10,843,000, halafu kuna na malipo mengine chini ya mradi huo US\$ 51,600.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilitaka Waziri anambie kwa sababu CAG wamegundua, PAC imefuatilia bado hakuna maelezo baada ya hapo ndio kazi ya Baraza hili inaishia kwamba imepokea ripoti tufunge tungoje mwaka mwingine na matumizi mengine yasiokuwa na vilelezo nikataka kujua kutoka kwa Waziri, atachukua hatua gani kwa watendaji wake wanaosimamia miradi hii ambako kuna matumizi haya mengi ya mafungu mengi, tena mengine fedha za kigeni nyingi ambayo hakuna maelezo kutoka kwa watendaji wake naomba maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa najibu nilieleza kwamba hizi hoja zilijibiwa zote mwezi wa Septemba na zikapelekwa, hiyo anayosema ya 35,000 ilikuwa ni malipo ya kulipwa wanafunzi Mombasa na ilipelekwa kwa TT hazikupita kwa mkononi mwa mtu, lakini walipokuja CAG mara ya kwanza ikawa zile *document* hazijaja, lakini mwezi wa Septemba wakakutana hao watu wa nje na wa ndani kina Mhe. Omar Ali Shehe kwa pamoja tena ilikuwa hapa hapa nilivyoarifiwa na barua nimepewa hizi hapa tumesha *clear*. Kwa hivyo, nilizijibu labda kama sikujibu kile kidudu kimoja kimoja, lakini zimeshakuwa *clear* watu wangu wamenithibitishia kuwa zimejibiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hao watu wa nje kama hujajibu hoja hawakupi nyengine. Kwa hivyo tuna adabu wenyewe kwa wenyewe na hivyo zimeshajibiwa Mhe. Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mhe. Jussa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sina hakika na hii hoja kwa sababu kwanza moja katika hoja ya msingi iliyoibuliwa katika ripoti hizi ni kwamba kumekuwa na utaratibu huu, Sheria ya Manunuzi ya Umma na Sheria ya Fedha nataka wakati ule wa ukaguzi kama kuna vilelezo vitolewe kwa sababu kama ulikwishafanya matumizi vilelezo utakuwanavyo wakati ule, lakini kumekuwa na utaratibu ambao Kamati ya PAC wanaulalamia hapa kwamba anapokwenda Mkaguzi wa nje ambaye ndiye anayeanza hapati vilelezo, lakini akishaviibua sjui hua vinapatikana wapi, ikienda PAC huwa tayari vishapatikana wakiilalamikia ile.

Sasa mimi sitaki tubishane na kaka yangu Mhe. Waziri, ninachosema mimi nimuombe tu, na wakati ule nakumbuka nilipochangia katika kikao cha Machi

alisema anakwenda kuifuatilia. Mimi nimuombe tena avipitie vifungu vilivyokuwa vimetajwa humu vya Wizara yake, kwa sababu hata akitwambia wahisani Mhe. Mwenyekiti, wahisani pia wanadanganywa hawa si kama Mzungu hadanganyiki. Kwa hivyo, ninachosema mimi anambie tu kwa sababu vimetajwa atakwenda kuvipitia kwa kina humu akae na watendaji wake aangalie na pengine baadae anaweza kupata ushauri wa PAC wamwambie yale ambayo wameyagundua ili mambo kama hayo tusione yakirejea katika wizara hii Mhe. Mwenyekiti wakati tunapokuja tukipokea ripoti ya CAG na PAC. Naomba hilo tu Mhe. Mwenyekiti halafu tuendelee ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe . Mwenyekiti, tutayazingatia maagizo ya Mhe. Jussa.

Kifungu 2001 Idara ya Uendeshaji na Utumishi Unguja Shs. 9,998,034,000/-
Kifungu 2002

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Natoa shukurani kwa Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri kuhusu umalizaji wa vile vituo ambavyo vilikwishaanza kujengwa. Lakini kwa bahati mbaya tena najua si kwa makusudia ni kwa bahati mbaya tu, kasahau kukitaja kile kituo cha Bwagamoyo katika hali gani. Kwa hivyo, naomba maelezo yake.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri wangu alikitaja lakini kama vizuri anisikie mimi Mheshimiwa basi cha Bwagamoyo kimo.

Mhe. Salim Abdalla hamad: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 2002 Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba Shs. 4,247,046,000/-
Kifungu 2003

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti nikushukuru, kwanza nitoe pongezi kwa Wizara ya Afya walivyoweza kutambuliwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Zanzibar ikawa ina uwakilishi maalum, hiyo ni changamoto kwa wizara nyengine ziige hivyo.

Lakini jengine nipongeze kwamba mchango wa Serikali katika ununuzi wa madawa ni mzuri na vile vile wafadhili kama *DANIDA* wanaendelea kutusaidia. Baada ya pongezi hizo sasa niseme kwamba Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilielezea umuhimu wa Wizara hii kutoa *circular* kwa wananchi ya kuwafahamisha kwamba wananchi mahospitali yetu dawa fulani, fulani na fulani zinapatikana bila ya matatizo, hii itatupunguzia wale wajanja

wachache kuweza kuzichukua na kuzifanyia magendo. Sasa sikupata jawabu zuri hapa namna serikali inavyoji-*commit* katika hilo. Kwa hivyo, naomba sasa Mhe. Waziri wanijibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa Mheshimiwa ni mzuri na tutauzingatia na kuchukua hatua.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, ikiwa ushauri unachukuliwa unafanyiwa kazi ni imani kwamba katika kipindi kifupi baada ya kupitisha bajeti hii wananchi wategemeo kwamba watapata sasa muongozo rasmi kutoka Wizara ya Afya juu ya upatikanaji wa dawa hizo. Kama hivyo ndivyo basi naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kukubali shauri hilo kwanza hizo dawa ziwepo siwezi kutoa *circular* tu. Na la pili nimeeleza kwamba tunabadilisha utaratibu badala ya kuwa-*push* kwamba tunapeleka tu, itakuwa ni *pull* hospitali zitatwambia. Sasa labda baada ya zile orodha za vituo zitapotwambia kwamba sisi tuna dawa hizi halafu ndio tuweze kusema kwamba wananchi kumekucha mbiu ya mgambo, maana yake ndio baada ya hapo tuwaeleze lakini kwanza zipatikane hizo dawa. Kwa sababu kuna utaratibu wa kufungua *tender* tuzipate hizo dawa, hivi sasa *tender* imeshawekwa iko njiani inaendelea, tukizipata Mheshimiwa tutafanya hivyo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu nadhani tunakubaliana kwamba hata ikapatikana *panadol* wananchi waelezwe kwamba wanachi hospitalini kwetu panadoli ipo msinunue, hilo tu, nashukuru tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 2003 Bohari Kuu ya Madawa Shs. 556,920,000/-
Kifungu 2004 Chuo cha Taaluma ya Afya

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, Kituo hiki kutokana na umuhimu wake ni kituo kinachotutolea watu ambao wanaziba mapengo katika shughuli nzima ya afya katika sehemu mbali mbali. Lakini chuo hiki kwa bahati katika kuangalia kiambatisho nambari 19 kilioko ukurasa wa 115 ni kuwa mimi kuna mambo sikuyafahamu. Kuna baadhi ya masomo unaona kuna wanafunzi kwa mwaka wa mwanzo hawako mwaka wa pili wala wa tatu lakini utawakuta wako mwaka wa nne, kuna wengine hawako mwaka wa pili lakini wako mwaka wa tatu mwaka wa nne hakuna. Kwa hivyo, ukiangalia utaona kuna mazeru mengi huku mara hapa pana wawili watatu huku maziro. Kwa hivyo, nilisema kuwa kiambatisho hiki hakifahamiki hivyo nilipenda kupewa maelezo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya taarifa hii ni kwamba mwaka 2009/2010 hakujachukuliwa wanafunzi kutokana na uhaba wa nafasi za madarasa. Kwa mwaka ule wa nne hakukuwa na fani nyengine isipokuwa wauguzi tu na ndio maana wanasoma miaka mine, kwa fani ya *PNHB* ni ya wakunga vijijini tu hawa hawakuchukuliwa wanaume. Hayo ndio masuala uliyouliza na hii ndio taarifa niliyopewa na wenzangu kutoka chuoni, kwamba hapo anapooka ziro ilikuwa hakuchukuliwa mtu mwaka huo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ni sawa lakini tuangalie kozi nambari moja ya *nursing*, huku mwisho mwaka wa nne au bora nieleze vizuri. Mwaka wa mwanzo kulikuwa na wanaume 32, wanawake 47; mwaka wa pili ilikuwa hakuna; mwaka wa tatu kulikuwa na wanaume 29, wanawake 69; mwaka wa nne ni wanawake 13 tu, wanaume wote hatukuwajua walipokwenda. Pia na hili naomba nipate maelezo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, labda sikuelewa kinachotakiwa labda nitafute hicho kitabu, lakini maelezo niliyopewa ni hayo kwamba ule mwaka wenye ziro ni kwamba hawakuchukuliwa watu kwa sababu tulikuwa hatuna nafasi na wale wengine hawasomi miaka mine wanasoma miaka mitatu ndio maana kulikuwa na *forth* ya wengine na wale wengine ikawa ni *PNHB* ni wakunga vijijini tu hawachukuliwi wanaume. Unapokuta wanawake watupu ujue kwamba kozi hiyo ni ya kinamama tu hakuna mkunga wa kijijini mwanamme.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ikiwa majibu ndio hayo mana nimeona katika hii kozi kwa mwaka wa kwanza na mwaka wa tatu wanaume wamo, lakini mwaka wa nne ndio hawamo, lakini ikiwa majibu ndio hayo tuendeleo.

Kifungu 2004	Chuo cha Taaluma ya Afya	Shs. 556,920,000/-
Kifungu 2101	Mfamasia Mkuu wa Serikali	Shs. 1,547,000,000/-
	Jumla ya Fungu:	Shs 18,234,000,000/-

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0401

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, hili ni fungu la Mipango ya Maendeleo, nilipokuwa nikichangia niliuliza utaratibu wa ununuzi wa vifaa vya matibabau unakwenda kinchi, kihospitali au kwa utaratibu gani ili vile vinavyokuja vijulikane kwamba vinakuja kwa nchi nzima au vinakuja maalum kwa hospitali fulani. Nafikiri kutokana na muda Mhe. Waziri hakupata nafasi ya kunijibu swali hili naomba nijue tu taarifa hiyo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba amefahamu kuwa ni sababu ya muda mara nyengine ilitufanya tukate. Kuna uagizaji wa namna mbili, kwa madawa ya mahospitali yote na vifaa hivyo vinanunuliwa na Mfamasia Mkuu na ndio maana ile bajeti yake iko juu. Lakini kwa matumizi mengine ya vitu vya kawaida ni idara ambazo hushughulikia zenyewe na kupeleka *document* zao kwenye Kamati ya *Tender*.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, sehemu niliyoulizia mimi ni hivi vifaa vya mashine za uchunguzi wa matibabu kwa mfano, mambo ya *X-rays* hayo, hizo *CT-Scan*. Nilisema kwamba Wizara inashughulikia kwa umoja au ni hospitali hospitali zina *order* kwa mujibu wa mahitaji yao. Nataka kujua hapo tu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hizi zinafanywa na Makao Makuu na zikeshapatikana huwa zinagawiwa zinakohusika hasa hizo *X-ray*. Lakini vingi ya vitu hivi huwa tunasaidiwa kwa sababu huwa ni ghali vile vinavyobaki vyengine hununuliwa, lakini kama *CT-Scan* na vitu vingine huwa tunasaidiwa. Kwa kawaida tunapitisha kwenye *tender* vinanunuliwa ndio vinapelekwa kwenye mahospitali.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa katika kompyuta kuna lugha moja inaitwa *up grading* na Mhe. Waziri amekiri kwamba Makao Makuu ndio inayoshughulikia uagizaji wa vifaa hivyo, namuomba sana kwamba wakati vikiletwa hivyo vifaa aweze kuzi *up grade* hospitali zote kwa mujibu wa uwezo wa wizara. Naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Sh. 21,982,205,000/-
Jumla ya Fungu	<u>sh. 21,982,205,000/-</u>

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

(*Baraza lilirudia*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko au pamoja na mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale waliokubali Hotuba ya Wizara ya Afya kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya

Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2012/2013 wanyooshe mkono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe tunawashukuru kwa mashirikiano yenu mazuri, kwa michangio mizuri na majumuisho ya Mhe. Waziri na Naibu wake na hatimaye tumepitisha Wizara hii ya Afya. Kwa hivyo, kwa kazi zetu za leo tumemalizia hapo naomba niakhirishe Baraza letu hadi kesho tarehe 12/07/2012 saa tatu za asubuhi.

(Saa 2:30 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 12/07/2012 saa 3:00 asubuhi)